BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Nane- Tarehe 29 Aprili, 2016

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

DUA

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

NDG. NEEMA H. MSANGI – KATIBU MEZANI: Maswali.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 61

Kuongezeka kwa Matumizi ya Dawa za Kulevya

MHE. MARIAM N. KISANGI aliuliza:-

Tatizo la matumizi ya dawa za kulevya linazidi kuongezeka siku hadi siku:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia vijana wetu walioathirika na dawa za kulevya?

NAIBU WAZIRI WA SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU (MHE. DKT. ABDALLAH S. POSSI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inalitambua tatizo la matumizi ya dawa za kulevya hapa nchini na athari wanazozipata watumiaji, hasa vijana ambao ni nguvu kazi muhimu, ambao huathirika kiafya, kiuchumi na kijamii. Ili kuwasaidia vijana walioathirika kwa kutumia dawa za kulevya, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati ifuatayo:-

(i) Serikali kupitia hospitali na vituo vya afya imekuwa ikitoa huduma mbalimbali ya kuwaondoa katika urahibu watumiaji wa dawa za kulevya. Baadhi ya hospitali ambazo zimekuwa zikitoa huduma hizo ni pamoja na Hospitali ya Rufaa ya Magonjwa ya Akili Mirembe - Dodoma, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali za Temeke na Mwananyamala za Mkoa wa Dar es Salaam na Hospitali ya Afya ya Akili Lulindi - Korogwe. Huduma zinazotolewa katika hospitali hizo ni pamoja na ushauri nasaha, kuondoa sumu mwilini na matibabu ya *methadone*.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia inaendelea na programu maalum ya kutoa huduma za upataji nafuu katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Serikali imetoa mwongozo wa uendeshaji wa huduma hizo na inaendelea na ujenzi wa kituo kikubwa cha huduma za matibabu ya utengemao katika eneo la Itega mjini Dodoma na inaratibu ujenzi wa kituo kama hicho mjini Tanga.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa naomba nipongeze juhudi za Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama kwa kutembelea vituo vyote vya utoaji wa madawa ya kulevya katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam. Pia nipongeze juhudi za Madaktari na Wauguzi wa vituo hivi ambao wanafanya kazi kila siku bila kujali Jumapili, sikukuu, kila siku ya Mungu wanafanya kazi ya kuwasaidia vijana wetu. Sasa naomba niulize maswali mawili:-

Kwa kuwa, matumizi ya madawa ya kulevya yanazidi kuongeza katika Jiji la Dar es Salaam siku hadi siku, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vituo vya utoaji wa madawa hayo katika Jiji la Dar es Salaam kwa kuwa sasa hivi vituo vinavyotoa hayo madawa ni vitatu, Mwananyamala, Temeke na Muhimbili. Serikali ina utaratibu gani wa kuongeza vituo hivyo katika Jiji la Dar es Salaam?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa vijana wengi wameingia katika makundi ya madawa ya kulevya kwa sababu ya ukosefu wa kazi au shughuli mbalimbali za kujiajiri au ujasiriamali, je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kituo kikubwa cha walioathirika na madawa ya kulevya ambacho kitawasaidia hawa waathirika wapate mafunzo ya ujasiriamali?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU WAZIRI WA SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU (MHE. DKT. ABDALLAH S. POSSI): Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kuhusiana na mpango wa kuongeza vituo vingine. Serikali inatambua wingi wa wahitaji wa

huduma ya kuondokana na urahibu wa madawa ya kulevya. Wazo la kujenga vituo hivyo ni zuri na pale uwezo utakaporuhusu, basi jambo hilo litafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusiana na uwezekano wa kujenga kituo ambacho kitawapa mafunzo. Katika swali la msingi nilishajibu kwamba tayari Serikali imeandaa mwongozo maalum utakaotumika na vituo mbalimbali vinavyowasaidia watu kuondokana na urahibu na mengineyo, mwongozo ambao bado utapitiwa na wadau, naamini kabisa hilo ni moja ya suala ambalo limezingatiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya nyongeza kutoka katika swali la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu hayo mazuri ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, tatizo hili la dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania, pamoja na kwamba siyo linaweza kujionyesha waziwazi lakini linaendelea kukua na tafiti zinatuambia mikoa ambayo iko katika maeneo ya mwambao mwa Bahari ya Hindi, Tanga, Mtwara, unakwenda mpaka Mwanza, yanaonekana kwamba ni maeneo ambayo tatizo la dawa za kulevya linaendelea kuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pamoja na kuona umuhimu wa kuanza kutumia dawa ya *methadone* kuhakikisha inawatibu warahibu wa dawa hizi za kulevya, inaendelea kutoa wito kwa mashirika mbalimbali ili tuweze kuendelea kushirikiana na Watanzania wote kuhakikisha tunafanya kazi ya pamoja kuwaondoa watoto wetu katika tatizo hili la dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, tatizo la dawa za kulevya bado linapambana na hali ya unyanyapaa kama tatizo la ugonjwa wa UKIMWI lililotangulia. Sasa ni wajibu wa kila Mtanzania tuanze kuondoa unyanyapaa, vijana wetu waweze kujitokeza kwa wingi, wapelekwe katika maeneo hayo yaliyopangwa kuwasaidia ili kwa pamoja tuweze kupambana na tatizo hili kwa vijana wetu na tusiendelee kuwaficha katika nyumba zetu, wale walioko mitaani, Serikali za Mitaa tushirikiane pamoja tuwalete ili waweze kupatiwa huduma hii na tuwarudishe katika hali yao ya kawaida. *(Makofi)*

Na. 62

Waajiri Wanaowakataza Wafanyakazi wao Kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi Nchini

MHE. SAUMU H. SAKALA aliuliza:-

Baadhi ya Waajiri ikiwemo Mashirika binafsi wamekuwa wakiwanyima haki ya msingi wafanyakazi wao kujiunga katika vyama mbalimbali vya wafanyakazi nchini kwa kutishia au kuwatafutia sababu ya kuwafukuza kazi pindi wanapojiunga na vyama hivyo:-

a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka Sheria itakayowabana waajiri wenye tabia ya kuwatishia au kuwafukuza kazi pale wanapojiunga na Vyama vya Wafanyakazi nchini?

b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa waajiri na kuwalazimisha kubandika Sheria hii ofisini kwa wafanyakazi ili wajue haki zao?

NAIBU WAZIRI WA SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU (MHE. ANTHONY P. MAVUNDE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saumu Heri Sakala, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, tayari ipo Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya Mwaka 2004 ambayo kupitia Kifungu cha 9 (1), kinaeleza wazi kuwa wafanyakazi wanayo haki ya kuanzisha au kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi pamoja na kushiriki kwenye shughuli halali za Vyama vya Wafanyakazi. Aidha, Kifungu cha 9 (3) cha Sheria hiyo, kinaeleza kuwa ni marufuku kwa mtu yoyote kumbagua mfanyakazi kwa sababu tu mfanyakazi huyo ni mwanachama wa chama cha wafanyakazi au anashiriki katika shughuli halali za chama.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi yangu itaendelea kuimarisha huduma za ukaguzi na usimamizi wa sheria za kazi, pamoja na kutoa elimu kuhusu sheria za kazi ili kuongeza uelewa wa waajiri, wafanyakazi na umma kwa ujumla ili kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanatumia haki na uhuru huo ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hailazimishi mwajiri kubandika Sheria ofisini ili wafanyakazi wasome haki zao. Hata hivyo, Kifungu namba 16 cha

Sheria hii kinawataka waajiri kubandika haki za wafanyakazi sehemu za wazi ili wazijue haki zao.

MHE. SAUMU H. SAKALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa Waziri anaweza kukubaliana nami kwamba kuna uhaba mkubwa wa elimu juu ya suala la sheria hizi na kwamba muda umefika sasa Serikali iweze kutilia mkazo juu ya kutoa elimu hii kwa wafanyakazi pamoja na waajiri?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, mpaka sasa Serikali imekwishashughulikia waajiri wangapi ambao kwa namna moja au nyingine wamewabagua wafanyakazi ambao tayari wamejiunga katika Vyama vya Wafanyakazi? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU (MHE. ANTHONY P. MAVUNDE): Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la kwanza la elimu juu ya Sheria za Kazi, Wizara yetu imeendelea kutoa elimu hiyo kupitia Vyama vya Wafanyakazi, pia kupitia makongamano na warsha na semina mbalimbali, kuweza kuwaelimisha wafanyakazi, waajiri na umma kwa ujumla namna ambavyo sheria zetu zinaelekeza mambo gani yatiliwe mkazo. Hata hivyo, tunaendelea kutilia mkazo eneo hili na tutakuwa na vipindi tofauti kupitia katika redio na televisheni ili Umma wa Watanzania uweze kufahamu namna gani sheria hizi zinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue wito huu kuwaomba wenzetu wa Vyama vya Wafanyakazi kwa kushirikiana na Wizara, tufanye kazi hii kwa pamoja ili tuweze kuwaelimisha waajiri na wafanyakazi sheria za kazi zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya pili ya swali lake, amezungumzia kuhusu idadi ya waajiri wangapi tumekwishawashughulikia ambao wamewabagua wafanyakazi. Ofisi yetu kupitia Maafisa Kazi ambao wamekuwa wakifanya kaguzi mara kwa mara, wamekuwa wakipita maeneo tofauti kubaini matatizo haya na kuwachukulia hatua wale waajiri ambao wanashindwa kutii masharti ya sheria, hasa hii Sheria Na. 6 ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana ya idadi, nitamtafuta Mheshimiwa Mbunge nimpatie taarifa kamili ni kwa namna gani tumewashughulikia hao waajiri waliowabagua wafanyakazi wao *specifically,* lakini tumekuwa tukifanya kaguzi hizi na tunayo orodha ya waajiri wengi tu ambao wameshindwa ku-*comply* na *orders* zetu ambazo zimefanyika baada ya ukaguzi.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea, Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 63

Kipaumbele cha Upatikanaji wa Zabuni za Kazi kwa Watu wenye Ulemavu

MHE. STELLA IKUPA ALEX aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko la ombaomba au utegemezi kwa watu wenye ulemavu nchini:-

Je, ni kwa nini Serikali isiwawezeshe kiuchumi watu wenye ulemavu kwa kuwapa upendeleo wa zabuni za kazi mbalimbali, kama vile kuzoa takataka, usafi wa vyoo, ushonaji na kadhalika kwenye Halmashauri?

NAIBU WAZIRI WA SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU (MHE. DKT. ABDALLAH S. POSSI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali namba 61 la Mheshimiwa Stella Alex, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua haki za watu wenye ulemavu kufanya kazi kwa misingi sawa na wengine, ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kiuchumi, fursa za ajira na kuwaandalia mazingira wezeshi. Serikali pia inatambua uwepo wa watu wenye ulemavu waliojiajiri wenyewe kupitia makampuni au vikundi mbalimbali ambao wanahitaji kuungwa mkono ili kupambana na utegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha upatikanaji wa fursa sawa kwa watu wenye ulemavu katika fursa mbalimbali, zikiwemo fursa za ajira na za kiuchumi, Serikali itaendeleza kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, Sheria Namba Tisa (9) ya Mwaka 2010 inayoelekeza hatua za makusudi za msingi na wajibu wa kutambua haki za watu wenye ulemavu. Kifungu 34(2) cha Sheria tajwa kinaipa nguvu Serikali kuchagiza upatikanaji wa fursa za ajira kwa watu wenye ulemavu kwa kufuata utaratibu wa kutoa kipaumbele maalum *(affirmative action)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wa pekee Serikali inawasisitiza Watendaji wote kwamba kwa mujibu wa Kifungu cha tatu (3) cha Sheria Namba Tisa (9) ya Mwaka 2010, maana ya neno kubagua inajumuisha, kukataa bila sababu maalum kutoa kipaumbele maalum kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie, kwa mujibu wa Kifungu cha tatu (3) cha Sheria Namba Tisa (9) ya Mwaka 2010, maana ya neno kubagua

inajumuisha, kukataa bila sababu yoyote kutoa kipaumbele maalum kwa watu wenye ulemavu. Hivyo basi, Watendaji wa Serikali wanawajibika kutoa kipaumbele maalum kwa watu wenye ulemavu katika masuala na fursa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 58(2) imeelekeza kutengea asilimia 30 ya tenda zote za utoaji huduma kwenye Halmashauri zote nchini kwa makundi maalum wakiwemo watu wenye ulemavu.

MHE. STELLA IKUPA ALEX: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:

(a) Je, ni lini Serikali itaziagiza Halmashauri na Manispaa, kutenga fungu maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu kama ilivyo ile asilimia 10 kwa wanawake na vijana?

(c) Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kufanya zoezi la utambuzi kwa watu wenye ulemavu, aina ya ulemavu walionao, pamoja na hali zao kiuchumi ili zinapotokea fursa iwe rahisi kuwafikia walengwa? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU (MHE. DKT. ABDALLAH S. POSSI): Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kuhusu kutenga asilimia ya mapato ya Halmashauri kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Kwanza niseme kabisa natambua utaratibu wa sasa wa kutenga asilimia 10 kwa maendeleo ya wanawake na vijana ulifanywa kutokana na kutambua tatizo la kuachwa nyuma kwa makundi haya muhimu. Falsafa hiyo hiyo inajengeka kwa watu wenye ulemavu. Hivyo basi, Serikali kwa kupitia taratibu zake za kiutawala na kisheria itaanza utaratibu wa kuutekeleza mpango huu pale hali itakaporuhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya mpango huo haujaanza kutekelezwa, nitoe wito kwamba katika asilimia hii 10 ya vijana na wanawake, basi kipaumbele maalum kitolewe kwa watu wenye ulemavu kwa mujibu wa Sheria Namba T isa (9) ya Mwaka 2010 kama nilivyoelezea kwa mujibu wa Kifungu cha tatu (3), pia kwa mujibu wa Kifungu namba 34(2), lakini pia kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inasema maana ya kubagua haitoizuia Serikali kuchukua hatua za makusudi ili kutatua matatizo mahsusi katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni wajibu wa Taasisi za Serikali kupitia Katiba na kupitia vifungu hivyo nilivyovitaja kutoa kipaumbele maalum kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili, kuhusu zoezi la utambuzi. Hapa kuna mawili; kwanza, tayari nilishazindua kazidata yenye taarifa za watu wenye ulemavu. Kazidata hiyo itatumika kufanya mambo mbalimbali ikiwemo utambuzi wa watu wenye ulemavu na mahitaji yao na inatarajiwa pale fedha itakapopatikana na hali ya teknolojia itakapoendelea, kazidata hii iunganishwe pia na kazidata nyingine zinazohusiana na taarifa ya hali ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niongeze kitu kimoja, kwamba tayari Serikali imeshatoa maagizo ya kuundwa kwa Kamati za Watu Wenye Ulemavu katika Halmashauri mbalimbali. Kamati hizi ndizo zitafanya kazi nzuri ya kuzishauri Halmashauri kuhusiana na mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu. Hivyo, kupitia Bunge hili nisisitize kutekelezwa kwa agizo hilo la Serikali la kuundwa kwa Kamati Maalum za Watu Wenye Ulemavu katika ngazi mbalimbali za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba sasa aulize swali lake.

Na.64

Malipo kwa Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA aliuliza:-

Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa wana majukumu mengi ikiwemo kuhakikisha amani na usalama katika maeneo yao:-

Je, ni lini Serikali itaanza kuwalipa posho ya mwezi ya Wenyeviti hawa ili kutoa motisha kwa kazi yao?

NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa katika kusimamia shughuli za Maendeleo Nchini. Katika kuzingatia uzito huo wa majukumu, Serikali imeweka utaratibu wa kila Halmashauri kurejesha katika Vijiji na Mitaa asilimia 20 ya mapato ya ndani ambapo sehemu ya fedha hizo zinatakiwa kulipa posho ya Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kuwa baadhi ya Halmashauri hazipeleki fedha hizo katika Vijiji na Mitaa na hivyo kuwanyima haki Viongozi hao kulipwa posho zao. Changamoto kubwa ya Halmashauri ilikuwa ni makusanyo yasiyoridhisha ya mapato ya ndani ambayo yalisababisha kushindwa kulipa posho hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia sasa Serikali inaimarisha makusanyo ya mapato ya ndani kwa kutumia mifumo ya kielektroniki ambapo imethibitika kuongeza makusanyo kwa zaidi ya asilimia mia moja. Kwa njia hiyo, Halmashauri zitakuwa na uwezo wa kulipa posho za Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa ambao sote tunatambua mchango wao mkubwa katika Taifa hili wa kuhamasisha shuguli za maendeleo. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, itaendelea kusimamia suala la makusanyo ya mapato ya ndani kwa nguvu zake zote ili kujenga uwezo wa Halmashauri kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chikota swali la nyongeza.

MHE.ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 20 ni fedha ndogo sana inayopelekwa kijijini na kama wataamua kumlipa Mwenyekiti wa Kijiji, Serikali ya Kijiji haitafanya kitu chochote kingine. Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kubeba jukumu hili la kuwalipa Wenyeviti wa Vijiji?

Swali langu la pili, kutokana na umuhimu sasa wa kundi hili na malalamiko yaliyopo kila kona nchini Serikali sasa haioni ni muda muafaka wa kutoa waraka maalum ambao utatoa maelekezo kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhusu malipo ya Wenyeviti hawa na kuweka kiwango cha chini cha posho hiyo, badala ya kila Halmashauri kutekeleza jinsi wanavyoona wao inafaa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ukiangalia kwa tathmini, maeneo mbalimbali posho hizi huwa hazilipwi na hoja ya Mbunge ni kwamba asilimia 20 ni ndogo. Ina maana ukiirejesha Kijijini, ikimlipa Mwenyekiti wa Kijiji mwisho wa siku ni kwamba fedha ile haitatosheleza hata kufanya kazi zingine za vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu Serikali za Mitaa safari hii ndiyo maana tumeweka *Specification* katika bajeti ya mwaka huu. kila Halmashauri wakati ikipitia mchakato wa bajeti tuione inakidhi jinsi gani itahakikisha mapato

yake ya ndani kwa kupitia vyanzo mbalimbali ili mwisho wa siku iweze kuhakikisha kwamba inapeleka fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tumesisitiza kuanzia Julai Mosi lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba hili jambo tunalolifanya, jinsi gani kila Halmashauri iweze kukusanya pesa za kutosha. Lengo ni kwamba Wenyeviti wa Vijiji waweze kupata posho, hali kadhalika pesa nyingine iende katika shughuli zingine za Maendeleo ya Kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili juu ya kupanga kiwango maalum, ni kweli. Sehemu zingine wanalipa sh. 20,000, sehemu nyingine wanalipa sh. 10,000, tutaangalia lakini, tutafanya utafiti wa kutosha kuona jinsi gani hii hali iende sawasawa. Kwa sababu tunajua wazi kwamba kila mtu hapa katika Bunge hili anategemea kazi ya Mwenyekiti wa Kijiji au Mwenyekiti wa Mtaa katika kufanikisha shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwa ni sambamba na mikutano yetu ambayo tunaenda kuifanya katika Jumuiya hizo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 65

Utoaji wa Elimu ya Kompyuta Mashuleni

MHE. SILAFU J. MAUFI aliuliza:-

Serikali imeamua kutoa elimu ya kompyuta kwenye shule za sekondari nchini lakini vifaa vya kufundishia havitoshelezi na hata Walimu ni wachache katika maeneo mengi ikiwemo Mkoa wa Rukwa, ambapo ni shule mbili pekee za Mazwi na Kizwite Sekondari ambazo zimeshaanzishwa:-

Je, Serikali ina mpango mkakati upi wa kufanikisha ufundishaji wa somo hilo kwa tija?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa elimu ya kompyuta mashuleni umeanza kufanyika kwa baadhi ya shule zenye mazingira yanayowezesha

somo hilo kufundishwa. Changamoto zilizopo ni uhaba wa Walimu, ukosefu wa umeme hususani maeneo ya vijijini na uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Serikali inakabaliana na changamoto hizo kwa kupeleka umeme vijijini kupitia Wakala wa Umeme Vijijini *(REA),* pamoja na kuhakikisha somo la Kompyuta linafundishwa katika Vyuo vya Ualimu ili kuwaandaa walimu watakaofundisha somo hilo mashuleni. Kuhusu upatikanaji wa vifaa mashuleni Serikali inashirikiana na Kampuni ya *Microsoft* ambayo imeonesha nia ya kuwezesha upatikanaji wa vifaa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa muda mrefu wa Serikali ni kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji mashuleni hususani masomo ya sayansi. Kwa msaada wa Kampuni ya *Microsoft* imeanza utekelezaji wa mpango huu kwa shule 50 katika Mikoa 25. Kwa Mkoa wa Rukwa shule zilizochaguliwa ni shule ya Sekondari ya Kizwite na Mazwi. Shule hizi mbili kila Mkoa ni vituo vya mafunzo kwa Walimu ili kuwajengea uwezo wa kufundisha kwa kutumia TEHAMA. Kituo cha Mazwi kinaanza kufanya kazi kuanzia Julai, 2016 ambapo kitapewa vifaa vyote muhimu vitavyohitajika katika mafunzo hayo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maufi swali la nyongeza.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri wa TAMISEMI kuhusu swali langu, nina swali la nyongeza.

Pamoja na jitihada na changamoto walizonazo na kuhakikisha kwamba masomo haya yanapatikana katika maeneo yetu ya Rukwa na hasa katika Mikoa yetu ya pembezoni. Kwa kuwa tumechelewa kupata elimu hii na *speed* ambayo wanakwenda nayo naona kana kwamba haitaweza kuleta mafanikio mazuri kwa mikoa yetu ya pembezoni. Swali langu dogo napenda kuuliza kwa niaba ya Mkoa wa Rukwa, ni lini sasa Wilaya ya Nkasi na Wilaya ya Kalambo masomo hayo yatafikishwa kwani Makao Makuu ya Wilaya hizi umeme umekwishafika? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tukiri kwamba suala la kompyuta sasa hivi na elimu ya TEHAMA ni jambo la msingi sana kama tunataka twende katika maendeleo ya kasi. Tumejielekeza sasa hivi, kama jibu langu la msingi lilivyosema kwamba, tutatumia kila liwezekanalo kuhakikisha tunawezesha vijana katika shule hizi kupata elimu hii ya kompyuta.

Suala la Nkasi na Kalambo ni kweli, katika maeneo mbalimbali ambayo tunataka tuyape nguvu hasa ukiangalia mkoa huu una changamoto kubwa sana, jambo hili hata Mheshimiwa Keissy na Mbunge wa Viti Maalum huwa eanalizungumzia sana, siyo hilo tu na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naomba nieleze wazi katika michakato ambayo tutaifanya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa sababu Mkoa wa Rukwa ni Mkoa wenye changamoto kubwa sana, tunaita mikoa ya pembeni, tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo katika program zetu Wilaya hizi tuwape kipaumbele, kwa sababu maeneo mengine ya mijini kama vile Dar es Salaam, Arusha na Mikoa mingine ni rahisi zaidi vijana ku-*access* mambo ya kompyuta kuliko mikoa ya pembezoni. Kwa hiyo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaupa kipaumbele Mkoa wa Rukwa na hasa katika Wilaya ya Nkasi na Wilaya ya Kalambo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 66

Kurejeshwa kwa Shamba la Mitamba

MHE. SILVESTRY F. KOKA aliuliza:-

Serikali kwa nia njema ilirejesha sehemu ya shamba la Mitamba lililopo Kata ya Pangani, Kibaha Mjini kwa wananchi ambao walikuwa wanaishi katika maeneo hayo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendelea kurejesha maeneo mengine ya shamba hilo ambayo bado yanakaliwa na wananchi?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swali lake namba 66 naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Shamba la Mitamba Pangani linamilikiwa na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Wizara ilipata shamba hili kwa kulipia fidia kwa wamiliki wa asili, ukubwa wa shamba lililokuwa limemilikiwa ni ekari 4000. Hata hivyo, katika kipindi kifupi

baada ya wananchi kulipwa fidia, shamba hilo lilivamiwa na wananchi kutoka sehemu mbalimbali na kuanzisha Mtaa wa Kidimu. Katika kutatua mgogoro huo wa uvamizi mwaka 2004, wamiliki Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Uongozi wa Serikali wa Mtaa huo ziliafikiana kuweka mipaka ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2007 Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ilipima shamba hilo kwa kuzingatia mipaka ya makubaliano yaliyoafikiwa mwaka 2004. Baada ya upimaji kulizalishwa kiwanja Namba 34 chenye ukubwa wa hekta 1037.81 na eneo lililokuwa limevamiwa lilikuwa na ukubwa wa hekta 2963, lilikabidhiwa kwa Halmashauri ya Mji wa Kibaha ili lipangiwe na kupimwa kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na upimaji kufanyika bado kuna mgogoro kati ya wamiliki wa shamba na wananchi wanaodai kutolipwa fidia wakati wa utwaaji wa shamba hilo waliokuwa ndani ya shamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vipindi tofauti Wizara yangu kwa kushirikiana na wamiliki Ofisi ya Mkoa wa Pwani, Ofisi za Wakuu wa Wilaya za Kibaha Mji na Wilaya na wananchi wanaoishi kwenye shamba hilo, tumekuwa tukikutana mara kwa mara kwa lengo la kupata ufumbuzi wa kudumu wa mgogoro huo. Mfano, tarehe 4/3/2016, Timu ya Wataalam kutoka Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Halmashauri ya Mji wa Kibaha na Mkurugenzi wa Upimaji na ramani ukiongozwa na Kamishna wa Ardhi Msaidizi wa Kanda ya Mashariki, ilikutana uwandani kwa lengo la kuhakiki mipaka na nyaraka za walalamikaji walio ndani ya shamba. Kwa sasa tunasubiri taarifa ya utekelezaji ambayo bado wataalam wanaendelea kufanyia kazi na mara itakapokamilika tutakuwa na ufumbuzi wa kudumu wa mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na tabia ya wananchi kuvamia maeneo ya Serikali na Taasisi zake, ili kuepuka hali hii tunaomba Waheshimiwa Wabunge na Viongozi mbalimbali kila mmoja kwa nafasi yake kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuacha mazoea yaliyojengeka ya kuvamia maeneo ya Serikali na Taasisi zake na maeneo mengine.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Koka, swali la nyongeza.

MHE. SILVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Waziri na Serikali kwa kuamua kurejesha takribani hekta 2963 kwa wananchi. Pamoja na kazi hiyo nzuri ya Serikali kwa wananchi ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika urejeshaji huo wa eneo hili kuna eneo dogo la takribani ekari 300 tu, ambalo lina zaidi ya kaya 250 ambalo

halikufikiriwa katika mpango huu na ambapo limewafanya wananchi hawa wanaokaa katika eneo hili sasa wakae kwa mashaka na kujiona kwamba wao ni wanyonge kwa sababu hawakuwekwa katika mpango huu ambao uliwarejeshea maeneo wenzao.

Swali langu la kwanza, je, ni lini sasa Serikali itaamua kurejesha eneo hili dogo ili kuwatendea haki kama ilivyotenda haki kwa wananchi wengine na wananchi hawa wa Vingunguti waweze kujiona kwamba wametendewa haki kama hao wengine.

Swali la pili, kwa sababu Serikali imekuwa na nia njema na imechukua hatua mbalimbali, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri pengine akishirikiana na Waziri wa Wizara ya Mifugo atatembelea eneo hili la Pangani maarufu linaitwa Vingunguti, ili tuweze sasa kukaa na wananchi na kupata ufumbuzi wa kudumu kutokana na mgogoro au tatizo hili la wakazi wa eneo hilo?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri wazi tu kwamba Serikali haiwezi kuendelea kurudisha maeneo kwa wananchi, hasa katika hilo eneo ukizingatia kwamba eneo la awali lililokuwa na ukubwa wa hekta 4000 wananchi walipewa eneo la hekta 2963 sawa na asilimia 74 ya eneo lote. Hivyo kuendelea kulimega ni kufifisha pia azma ya Wizara ya Kilimo na Mifugo, katika kuendelea kuzalisha mitamba bora ambapo tunahitaji kuwapeleka wafugaji wetu katika maendeleo ya kuwa na ufugaji bora na endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili niseme tu kwamba, Wizara imekuwa na nia ya dhati kufika katika lile eneo na kukutana na wananchi na hasa kukutanisha pande zote mbili, ukizingatia mara ya mwisho tumekuwepo kule tarehe 4/3/2016, lakini kama hiyo haikutosha Wizara yangu iko tayari kuendelea kukutana nao ili muafaka uweze kufikiwa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani Mbunge wa Korogwe Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 67

Kutoendelezwa kwa Mashamba Yaliyobinafsishwa

MHE. STEPHEN H. NGONYANI aliuliza:-

Katika Jimbo la Korogwe Vijijini yako mashamba ambayo tangu yabinafsishwe hayajaendelezwa:-

(a) Je, ni lini mashamba hayo yatagawiwa kwa wananchi kwa sababu hayaendelezwi?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuyatoa kwa wananchi mashamba ambayo hayaendelezwi ili kuwapa fursa ya kuyatumia kwa shughuli za kilimo?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba nijibu swali namba 67 la Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeziagiza Halmashauri zote nchini kukagua mashamba na kuwasilisha taarifa za ukaguzi na hatua stahiki. Mashamba yatakayobainika kwamba hayajaendelezwa ilani ya ubatilisho zitatumwa na Wakurugenzi husika kwa umilikishaji. Baada ya kipindi cha siku 90 kumalizika Halmshauri zitatakiwa kuleta mapendekezo ya ubatilisho Wizarani.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi uliofanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, umebaini kuwepo kwa shamba lisiloendelezwa la Mwakijubi *Farm* linalomilikiwa na Ndugu Chavda. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ameanza kufanya taratibu za ubatilisho wa milki kabla ya kuwasilisha mapendekezo Wizarani.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ugawaji wa mashamba kwa wananchi hufanyika baada ya taratibu za ubatilisho kukamilika na kupata kibali cha Mheshimiwa Rais. Taratibu za ubatilisho zinapokamilika mashamba haya hurejeshwa katika Halmashauri husika ili yapangiwe matumizi mengine ikiwemo kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai yetu sasa baada ya taratibu za ubatilisho kukamilika na maeneo haya kukabidhiwa kwenye Halmashauri, Halmashauri watapanga matumizi kulingana na uhitaji wa eneo husika ikiwa ni pamoja na matumizi ya kilimo. Kwa sasa, wakati zoezi la ubatilisho linafanyiwa kazi, tunaomba wananchi waendelee kuvuta subira mpaka hapo mchakato wa ubatilisho utakapokamilika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ngonyani swali la nyongeza.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na yenye maana. Mwaka jana mwezi wa Sita niliomba Serikali iende mpaka Korogwe ikaangalie maeneo ambayo hayaendelezwi na Serikali iliniahidi kwamba ingekwenda kule na kukagua mashamba ambayo hayaendelezwi ili ufanywe utafiti wa kuwagawia wananchi, hadi leo hii na mimi nilienda kwenye mikutano ya hadhara na kuwaambia wananchi kwamba Naibu Waziri atakuja kuangalia mashamba ambayo hayaendelezwi na watu wakakipa sana kura Chama cha Mapinduzi kwa kujua kwamba viongozi wanafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kushangaza mpaka leo hii hawajafika na badala yake nasikitika sana baadhi ya Watumishi wa Halmashauri wanaleta habari ambazo siyo njema, zisizoweza kumsaidia mtu wa aina yeyote. Naomba Waziri, ni lini mimi na wewe tutakwenda mpaka Korogwe Vijijini ukaone huku kudanganywa kwamba ni shamba moja katika mashamba 17 yanayozunguka Jimbo langu hayajapatiwa ufumbuzi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niseme kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kupitia swali la Mheshimiwa Ngonyani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa kama kila Mbunge atataka Waziri afike kwenye eneo lake na kufanya utambuzi wa mashamba zoezi la ukaguzi wa mashamba haya yasiyoendelezwa halitafikia ukomo. Hata hivyo, najua wazi kwamba ni jukumu la Halmashauri zetu husika ambapo na Wabunge ni Wajumbe kuweza kuyatambua hayo mashamba na Wizara inapofika pale, inakuja baada ya kuwa imepata taarifa ili kujihakikishia kwamba kilicholetwa ni sahihi, tutafika pia kukagua, lakini hatuwezi kufanya ile kazi ya mwanzo, unakwenda kila eneo kukagua halafu ndiyo uweze kuchukua hatua, maana utashindwa kuchukua maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Halmashauri husika ilete mapendekezo halafu Mheshimiwa Waziri apeleke kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya ubatilisho. Maamuzi ya matumizi yanafanyika ndani ya Halmashauri kwa sababu ndiyo wenye mamlaka pia ya kugawa mashamba hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu zoezi hili Mheshimiwa Waziri alishalitolea maelekezo na alitoa barua katika maeneo yote, ni jukumu letu sasa kuanza kukagua yale mashamba tuliyonayo ambayo Halmashauri zetu imeyatoa. Hivyo, Wizara inarahisisha kazi baada ya kuwa imeshapata kutoka kwenu, sisi tutakuja kutambua ili sheria zisikiukwe na kuleta malalamiko kwa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Ngonyani iwapo itabidi, basi tutafika, lakini kazi hii ni kazi ya Halmashauri.

Na. 68

Tatizo Sugu la Maji katika Jiji la Dar es Salaam

MHE. SAED A. KUBENEA aliuliza:-

Serikali imetoa ahadi nyingi za kumaliza tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam lakini sasa ni takribani miaka sita tangu Serikali itoe ahadi hizo na tatizo hilo bado liko pale pale:-

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kumaliza tatizo hilo la maji?

(b) Je, ni kwa nini Serikali imekuwa ikitoa ahadi za kuwapatia wananchi wake maji wakati haina uwezo wa kutekeleza ahadi zake hizo?

(c) Je, ni nini kimesababisha kutokamilika kwa mpango wa kusambaza maji toka Ruvu ambao ulitarajiwa kuwa ungemaliza tatizo la maji katika maeneo mengi ya Jiji hasa Jimbo la Ubungo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Jimbo la Ubungo, lenye vipengele (a), (b), (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza ahadi zote ilizoahidi kuhusu kumaliza tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam. Tayari ahadi ya kuongeza uzalishaji wa maji kutoka mtambo wa Ruvu Chini na ulazaji wa bomba kubwa lenye kipenyo cha milimita 1800 kutoka Ruvu Chini hadi Jijini lenye urefu wa kilomita 56 imekamilika. Mtambo wa Ruvu Chini umeanza kuzalisha lita milioni 270 kutoka lita milioni 180 za awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu umekamilika na sasa una uwezo wa kutoa maji lita milioni 196 kutoka lita milioni 82 za awali kwa siku. Kazi za ulazaji wa mabomba mawili kutoka Mlandizi hadi Kimara, ujenzi wa tenki jipya la maji la Kibamba na ukarabati wa matenki ya Kimara zimefikia wastani wa asilimia 98. Uendeshaji wa majaribio umeanza mwezi Aprili, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia inaendelea kutekeleza mradi wa Kimbiji na Mpera ambapo hadi sasa Mkandarasi amekamilisha uchimbaji wa visima tisa kati ya visima 20 vilivyopangwa, kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2016. Visima hivyo vyote vikikamilika vitatoa lita milioni 260 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa ujenzi wa mabomba ya kusambaza maji Jijini Dar es Salaam ulisainiwa tarehe 11/12/2015 na Mkandarasi yuko kazini akiendelea kutambua njia za mabomba na maeneo ya kujenga matanki na kuchukua vipimo yaani *survey*. Matarajio ni kuanza ujenzi mwezi Mei, 2016 kazi hii itakamilika June, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam kwa sasa umefikia lita milioni 390 kwa siku, ukilinganisha na mahitaji ya maji lita milioni 450 kwa siku za sasa. Miradi yote ikikamilika uzalishaji wa maji Jijini Dar es Salaam utafuikia lita milioni 750 ambapo yatakidhi mahitaji hadi kufikia mwaka 2032.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kubenea swali la nyongeza.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza, naomba Mheshimiwa Waziri jina langu amelitamka vibaya naitwa Saed siyo Sadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na tatizo la mtambo wa Ruvu kupatiwa ufumbuzi lakini tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam limekuwa kubwa hasa katika Jimbo la Ubungo, Kibamba, Segerea, Kigamboni, Ukonga, na hata Temeke.

(a) Mheshimiwa Waziri tatizo hili linatokana kwa kiasi kikubwa na uchakavu wa miundombinu hasa yale mabomba yanayosambaza maji katika majumba. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kukarabati miundombinu ya maji katika Jiji la Dar es Salaam?

(b) Kwa kuwa, majibu ya Mheshimiwa Waziri yamekuwa ya jumla, kwamba mtambo umekamilika, majaribio yameanza, ukarabati unafanyika, Mheshimiwa Waziri anaweza akataja kwa majina mitaa ambayo mradi huu wa maji utafanyika katika kipindi hiki cha haraka?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba msamaha nimetamka Sadi kumbe ni Saed, basi nitafanya marekebisho Mheshimiwa Kubenea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini maswali ya Mheshimiwa Kubenea mawili ni kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Maji inao mpango mkubwa sana wa kumaliza tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa ukarabati na upanuzi wa mfumo wa kusambaza maji safi katika Jiji la Dar es Salaam, unaohusisha maeneo ya Tegeta-Mpiji, Mpiji-Bagamoyo na Mbezi-Kiluvya. Mradi huu unagharimu dola za Marekani milioni 23.927 na ujenzi unatarajiwa kukamilika tarehe 21/4/2017. Mradi huu utakapokamilika maeneo yatakayopatiwa maji ni pamoja na Mji wa Bagamoyo na vitongoji vyake, eneo la uwekezaji la Bagamoyo *EPZ*, Mpiji, Bunju, Mabwepande, Boko, Mbweni, Tegeta, Ununio, Wazo, Salasala, Kizundi, Matosa, Mbezi Juu, Goba, Changanyikeni, Makongo, Kiluvya, Kibamba, Mbezi Msakuzi, Makabe, Marambamawili na Msigani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali kwa kutambua kwamba kuna maeneo mengi ambayo hayatofikiwa kwa haraka na mtandao wa mabomba ya maji, imefanya utaratibu wa kuchimba visima 51, katika hivyo visima 51 visima 24 vimekamilika, na maeneo ambayo tayari yameanza kupata huduma hiyo ni pamoja na Mavurunza A, Kilungule A na B, King'ongo I, King'ongo III, Sandali, Mpogo, Mwemberadu, Mburahati, Kipunguni, FFU, Ukonga, Mongo la Ndege, Segerea, Chanika na Yombo, Saranga na Saranga II. Chang'ombe A, Ununio, Chang'ombe Toroli, Keko Magurumbasi na Keko Mwanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Mheshimiwa Kubenea uwe na uhakika matarajio yetu ni kwamba, ikifika mwaka 2017 maeneo mengi ya Jiji la Dar es Salaam yatakuwa tayari yameshapatiwa maji. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Yahya Omari Masare, Mbunge wa Manyoni Magharibi sasa aulize swali lake.

Na. 69

Taratibu za Usajili katika Biashara ya Mazao ya Misitu

MHE. YAHAYA O. MASSARE aliuliza:-

Ili Mtu au Kampuni iweze kufanya biashara ya Mazao ya Misitu anapaswa kusajiliwa:-

(a) Je, ni kwa nini usajili huu hufanywa kila mwaka?

(b) Je, Serikali haioni kwa kufanya hivyo kunaongezea walipa kodi mzigo?

(c) Je, usajili huu hauwezi kufanywa pale tu mtu au Kampuni inapoanza biashara kwa mara ya kwanza na anapoendelea aweze kuhuisha badala ya kusajiliwa upya kila mwaka.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usajili wa wafanyabiashara wa mazao ya misitu hufanywa kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Sura 323, kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002, Kifungu cha tano (5) na Kifungu cha 108 na Kanuni zake za mwaka 2004, Kanuni ya 54 kwa kuzingatia kiasi cha mazao ya misitu cha kuvuna mwaka hadi mwaka, ambacho hutegemea uwezo na ndicho kigezo cha kutambua idadi ya wafanyabiashara wa mazao ya misitu watakaopewa vibali vya kuvuna ili kuepuka kuwa na idadi kubwa ya wateja kuliko uwezo wa msitu kuvunwa katika mwaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, usajili wa kila mwaka husaidia kutekeleza mipango endelevu ya usimamizi kwa ajili ya kupanga kiwango kinachotakiwa kuvunwa kwa mwaka. Aidha, utaratibu huu hutoa fursa kwa wafanyabiashara wapya kuingia kwenye soko hivyo kuweka mipango mizuri zaidi ya kutambua mahitaji yao kulinganisha na uwezo wa misitu iliyopo. Vile vile kutoa fursa kwa wananchi wengi zaidi kushiriki na kunufaika na uvunaji wa rasilimali za Taifa, mazao ya misitu ikiwa ni sehemu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa zoezi la usajili huambatana na ada mahsusi, wafanyabiashara waone kuwa hii ni fursa kwao kuchangia pato la Taifa kupitia biashara wanazozifanya, utaratibu ambao unafanana na masharti ya biashara nyingine zinazofanyika hapa nchini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Massare swali la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Misitu Namba 14 ya mwaka 2002, ilizuia usafirishaji wa mazao ya misitu ambayo hayajachakatwa ikiwemo asali, mbao na hata wanyamapori. Naomba kuuliza swali langu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya zuio hilo Serikali imeruhusu kusafirisha mbao ya sentimita 15 tu unene na wakati huo wadau na masoko yanahitaji zaidi ya sentimita 15. Je, Serikali iko tayari sasa kuwaruhusu wafanyabiashara ambao wanafanya *export* ya mbao hizi, wakiwemo wafanyabiashara wa mitiki, *pine* na mbao za miche ya asili angalau wafikie katika sentimita 20 ili nao wapate tija na kushindana na wafanyabiashara wenzao katika masoko?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika Jimbo langu la Manyoni Magharibi na Wilaya nzima ya Manyoni, imezuia uvunaji wa mbao na mazao ya misitu kwa ujumla, Je, Serikali sasa ipo tayari kushirikiana na Halmashauri yangu mpya ya Itigi uvunaji uendelee, badala ya watu sasa kuiba ili walipe kodi za Serikali na maduhuli na pia kusaidia pato la Halmashauri wakati misitu ipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ambayo ameitaja Sheria Namba 14 ya mwaka 2002, Serikali iliweka utaratibu kwa uvunaji wa mazao mbalimbali ya misitu kama alivyoyataja na kwa uchache ni pamoja na miti ya mitiki, pamoja na ya *pine,* napenda kusisitiza kwamba pale ambapo Sheria ipo na ilikwishawekwa na Serikali, ni wajibu wetu kufuata masharti ya Sheria hiyo katika kipindi chote ambacho Sheria hiyo bado imesimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo kuna mawazo mengine mapya ambayo ni mazuri, ya kujenga kwa maslahi ya Taifa, basi ni budi kufuata utaratibu wa kawaida wa kisheria kuweza kurekebisha sheria ili kuweza kunufaika na mawazo mapya kama yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, uvunaji wa mazao ya misitu katika Jimbo la Manyoni Magharibi na Wilaya Manyoni kwa ujumla ulizuiliwa kwa sababu za msingi za uhifadhi. Pale unapoendelea kuvuna unatakiwa uvune ukizingatia sharti la uvunaji endelevu, kama utaendelea kuvuna bila kuzingatia masharti ya uvunaji endelevu, ukakiuka masharti *sustainability* maana yake ni kwamba utakosa kila kitu kwa sababu misitu hiyo inaweza kupotea kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunapokea maoni yake na kwamba sasa tutakwenda kufanya utafiti wa kisayansi kwenda kuangalia kama zuio hilo sasa limepitwa na wakati, inawezekana msitu huo sasa umeweza kupata hadhi ambayo inawezekana kabisa tukaendelea kuvuna badala ya kusimamisha kama tulivyosimamisha hapo awali. Tutaongozwa na utafiti wa kisayansi ili tuweze kuona kwamba, sasa tunaweza kuendelea kuvuna.

Na. 70

Kushindikana kwa Utekelezaji wa Tangazo la Serikali la Mwaka 2008

MEH. RISALA S. KABONGO aliuliza:-

Utekelezaji wa Tangazo rasmi la Serikali la Mwaka 2008 juu ya mpaka mpya wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika Bonde la Usangu umeshindikana, hivyo kufanya upanuzi holela wa maeneo ya kilimo, uvamizi wa mifugo mingi na matumizi holela ya maji katika kilimo, jambo ambalo limesababisha uharibifu wa mazingira, Mto Ruaha Mkuu kuendelea kukauka kila mwaka na kuathiri uzalishaji umeme katika Bwawa la Mtera na Kidatu na shughuli zingine na matumizi ya maji ya Mto Ruaha Mkuu:-

(a) Sababu zipi za msingi zilizosababisha utekelezaji wa Tangazo hilo kushindwa kwa takribani miaka nane sasa?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka ili kunusuru na kusitisha uharibifu mkubwa wa mazingira unaoendelea katika Bonde la Usangu?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Risala Said Kabogo, Mbunge wa Viti Maalumu, lenye Sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inampongeza Mheshimiwa Risala Kabongo kwa kutambua na kuthamini jitihada za Serikali na kuona umuhimu wa uhifadhi katika Taifa, hususan uhifadhi katika eneo la Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika Bonde la Usangu, ambako shughuli za kilimo, uingizaji, uchungaji na ulishaji mifugo na matumizi ya maji yasiyo endelevu katika kilimo zimesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira, unaosababisha pamoja na athari nyingine kukauka kila mwaka kwa Mto Ruaha Mkuu na hatimaye kuathirika shughuli za uzalishaji umeme kutokana na kukosekana kwa kiasi cha maji kinachohitajika katika mabwawa ya Mtera na Kidatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu nilioainisha hapo juu Serikali ilikamilisha taratibu zote husika na kutoa Tangazo la Serikali Namba 28 la mwaka 2008, ambalo msingi wake ni Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282, hususan Kifungu cha tatu (3) na cha nne (4) cha sheria hiyo ili eneo la Bonde la Usangu lijumuishwe ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Tangazo la Serikali Namba 28 la mwaka 2008 haujashindikana na badala yake matakwa ya Tangazo hilo yameanza kwa kuhakiki mipaka na kuweka alama za kudumu *beacons* kwa baadhi ya maeneo yaliyoongezwa. Kutoa elimu na kuhamasisha wananchi waliotakiwa kuhama ili kupisha hifadhi, kufanya tathmini na kulipa fidia ya ardhi na mali zisizohamishika kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 na Na. 5 za mwaka 1999. Aidha, Serikali inaendelea na utekelezaji wa matakwa ya Tangazo la Serikali Namba 28 la mwaka 2008, ambapo baada ya changamoto zilizojitokeza kutatuliwa, wananchi walioko katika eneo husika pamoja na mali zao zinazohamishika wataondoka kupisha shughuli za uhifadhi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu yangu ya swali Namba 53 lililouliza na Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed, Mbunge wa Jimbo la Mbarali, katika Kikao cha Sita cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Moja kilichofanyika tarehe 27/4/2016, nilisisitiza kuhusu umuhimu wa kuhifadhi eneo la Bonde la Usangu kwa maslahi mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu hayo nilieleza kuhusu kuwepo kwa timu ya Wataalam iliyopitia changamoto za utekelezaji wa Tangazo la Serikali, ikiwa ni pamoja na kutafsiri mpaka, kuweka alama na kukamilisha malipo ya fidia kwa mujibu wa sheria katika kipindi cha mwezi mmoja, hatua ambayo itawezesha Serikali kuendelea na hatua muhimu na za haraka ili kudhibiti uharibifu wa mazingira katika Bonde la Usangu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kabongo swali la nyongeza.

MHE. RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza, naitwa Risala Said Kabongo siyo Kabogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kukauka kwa Mto Ruaha Mkuu mwaka hadi mwaka kunasababisha athari za kimazingira na athari za kukua kwa utalii katika hifadhi hiyo, pamoja na athari kwa wananchi wanaoishi kando kando ya hifadhi hiyo.

Swali la kwanza, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Mto Ruaha Mkuu ambao ndiyo kiini cha hifadhi ya Ruaha unatiririsha maji yake mwaka mzima?

Swali langu la pili, je, Serikali itawasaidiaje wananchi wanaoishi kandokando ya bwawa la Mtera ambao uchumi wao unategemea uvuvi na kilimo kupitia mto huu wa Ruaha. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimwombe radhi kwa kutamka jina lake ndivyo sivyo, nimepokea masahihisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mkakati, Serikali inao mkakati siyo kuhusu tu eneo la Bonde la Usangu na Mto Ruaha Mkuu, Serikali inao mradi mkubwa kabisa ambao unakusudia kuboresha shughuli za utalii kwenye eneo la Kusini, mradi ambao unatamkwa kwa kifupi re-*grow* yaani *the Resilient Natural Resources Management for Growth*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi huo eneo la Bonde la Usangu ambalo linajumuisha Mto wa Ruaha ni sehemu ya mradi huu. Tunakwenda kuboresha mambo yote yanayohusiana na uhifadhi katika eneo hilo ili kuhakikisha kwamba eneo hilo lote sasa linakuwa na sifa endelevu ya kuwa na kila kitu kilichomo ndani yake katika hali ya uhifadhi unaotambulika Kimataifa na unaokubalika katika kuwezesha shughuli za utalii ziendelee kubaki kuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, mradi huu ambao unatekelezwa chini ya Benki ya Dunia sasa hivi upo katika hatua za awali katika siku zijazo za usoni tutautolewa taarifa kuhusiana na jinsi ambavyo tutakuwa tunaendelea kuboresha eneo ambalo nimelitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wananchi wa Mtera inafanana na jibu nililojibu kwa ujumla kwamba mradi huo ninaoutaja ambao upo chini ya Benki ya Dunia unajumuisha mambo yote, yakiwemo kuhifadhi mito iliyomo ndani yake, kuhifadhi misitu iliyopo ndani yake, pia kuangalia maisha ya binadamu na shughuli zao katika eneo linalohusika kama wafugaji, wakulima na wengine wanaofanya shughuli nyingine zote watajumuishwa katika malengo makuu ya mradi huu na kwa hiyo maslahi yao yatazingatiwa Kitaifa katika mradi huo.

Na. 71

Eneo la Sayaka Salama Bugatu Kufanywa
Hifadhi ya Misitu

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA aliuliza:-

Serikali ilitenga eneo la Sayaka Salama Bugatu kuwa hifadhi ya msitu, lakini msitu wenyewe haukui huku wananchi, wafugaji na wakulima wakikosa maeneo ya mifugo yao na kilimo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwarudishia wananchi maeneo hayo ili waweze kuyatumia kwa kilimo na mifugo.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniventura Desdery Kiswaga, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, msitu na hifadhi Sayaka ulitangazwa rasmi kuwa Msitu wa Hifadhi chini ya Serikali Kuu kwa Tangazo la Serikali namba 90 la tarehe 19 Juni 1996. Katika siku za nyuma Halmashauri ya Wilaya ya Magu iliomba kubadilishwa kwa matumizi ya msitu huu wenye ukubwa wa hekta 5421, lakini kwa kuzingatia sababu za msingi za kiuhifadhi, Wizara kupitia barua kumbukumbu namba JA/66/298/02/33 ya tarehe 19 Desemba, 2001 ilikataa ombi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya msitu wa Sayaka ni sehemu muhimu sana inayochuja na kudhibiti taka nyingi kutoka mto Duma unaopita katika hifadhi hii. Uwezo huu wa kudhibiti na kuchuja taka ambazo ni pamoja na tope na viuatilifu vinavyotoka mashambani unatokana na uoto wa asili uliopo ambao unahitaji kuboreshwa zaidi ili uendelee kupunguza athari za tope na viuatilifu katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, hatua ya kubadilisha msitu huu na kuwa mashamba eneo la kuchungia mifugo au shughuli nyingine za kibinadamu zisizo za uhifadhi itasababisha kupotea kwa uoto wa asili na kusababisha mmomonyoko mkubwa wa udongo ndani ya hifadhi na hivyo kuruhusu taka nyingi kuingia ziwani jambo ambalo litapunguza uhifadhi wa mazingira ya Ziwa Victoria ambalo ni muhimu kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu mkubwa wa msitu wa Sayaka, Serikali haina mpango wa kubadilisha matumizi yake kinyume na malengo ya kuanzishwa kwake, kwani hatua hiyo itasababisha athari kubwa na nyingi za kimazingira na kiuchumi. Aidha, wananchi wanaoishi vijiji vinavyozunguka Msitu wa Hifadhi ya Sayaka ndiyo watakaokuwa waathirika wa kwanza kwa upepo mkali, upungufu wa mvua utakaoathiri mifugo na kilimo na athari nyinginezo kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuanzishwa kwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania mnamo mwaka 2011, usimamizi na ulinzi wa misitu huu umeimarishwa na kufanya uoto wa asili kurejea kwa kufanya marejeo ya soroveya, kuimarisha mipaka na kuweka vigingi 65 katika mipaka. Aidha, Kamati za Maliasili za Vijiji Kumi ndani ya Halmashauri ya Magu zimeanzishwa kwa ajili ya kushirikiana na wataalam katika ulinzi wa msitu huu.

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza msitu unaozungumzwa haupo, hata athari zinazozungumzwa kwamba vijiji vinavyozunguka watapata athari ya upepo siyo kweli, kwa sababu hata wewe ukisimama mle mita mia tatu unaonekana huo ni msitu?

(a) Je, Serikali kwa sababu inasema ni chujio haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kulipunguza eneo hilo ikawapa wananchi upande mwingine, na upande mwingine ili wakaendelea na shughuli za kijamii na eneo linalobaki wakaliboresha kwa kupanda wenyewe misitu endelevu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu majibu haya ni ya kudanganywa, je, Naibu Waziri yupo tayari kuambatana nami kwenda kuliona eneo ambalo linasemwa ni hifadhi?*(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza, nataka hapa kwa ufupi kabisa tuelewane kwamba, dhana hii ni kwa Watanzania wote kwa nchi nzima. Dhana ya kwamba changamoto za mahitaji ya ardhi kwa ajili ya matumizi mengine ya kibinadamu zitamalizwa kwa kuendelea kumega au kwa kuchukua maeneo yaliyohifadhiwa ni dhana ambayo siyo ya maslahi kwa Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiendelea kufikiria kwamba ardhi iliyohifadhiwa ambayo ipo hivyo ilivyo leo kwa sababu imehifadhiwa kwa muda wote ambao imehifadhiwa, dhana hiyo itatufikisha mahali ambapo uhifadhi huo utapotea na ukipotea athari zake ni pana na kubwa na zinatugusa wote nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli inawezekana ukifika katika msitu huo huoni miti juu, lakini msitu unahifadhiwa kwa ajili ya tafsiri ya misitu ya miti unayoiona ipo juu, lakini pia ni kwa sifa za ardhi pale chini, ndiyo maana tumesema chujio, unaweza usione miti lakini, viumbe vilivyopo pale chini kwenye udongo sifa za ardhi ile iliyopo pale na yenyewe pia ni sehemu ya uhifadhi na ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya pili ya swali lake, kwanza siyo kweli kwamba majibu ni ya kudanganywa, lakini hakuna mwisho wa kufanya vizuri, kila unapodhani umefanya vizuri bado kuna kufanya vizuri zaidi. Nipo tayari kuambatana naye kwenda kuboresha uelewa nilionao tayari, kwenda kupata majibu ya pamoja mimi naye wakati tutakapoweza kupanga wote kwa pamoja, ili tuweze kupata hayo majibu sahihi na kuweza kutatua matatizo haya kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naona kuna wageni.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika kuhusu Mwongozo,

NAIBU SPIKA: Naomba ukae Mheshimiwa Juliana Shonza, nikiwa nimekaa ndipo unaweza kuomba Mwongozo ikiwa hakuna mtu mwingine yeyote aliyesimama. Nitakapoletewa matangazo ya wageni nitayatangaza, hata hivyo kuna matangazo machache hapa.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la kwanza ni la Mheshimiwa Abdallah Ulega, Mwenyekiti wa Waheshimiwa Wabunge Waislam, anawatangazia kwamba waumini wa dini ya Kiislam wakahudhurie ibada ya Ijumaa katika Msikiti Mkuu wa Gaddafi na baada ya hapo kutakuwa na mkutano muhimu kwenye madrasa ghorofa ya kwanza, nadhani ni ndani ya jengo hilo la Msikiti Mkuu wa Gaddafi.

Tangazo la pili linatoka kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama *Chief Whip* wa Chama cha Mapinduzi, anawatangazia Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi kuwa kutakuwa na kikao cha Wabunge *caucus,* kitakachofanyika saa tisa kamili katika Ukumbi wa Pius Msekwa, badala ya saa saba ni saa tisa kamili.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine ni kikao cha Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ambacho watakutana leo tarehe 29 mwezi Aprili, 2016, watakutana saa saba mchana baada ya kuahirisha Bunge, katika jengo la Utawala chumba Namba 229, Mwenyekiti anaomba mhudhurie.

Tangazo lingine ni kikao cha Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti anaomba Wajumbe wa Kamati hii wakutane saa 7.30 mchana katika Kumbi zilizopo Hazina. Mnaombwa kuhudhuria bila kukosa leo.

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa orodha ya wageni; wageni tulionao leo wapo jukwaa la wageni, kundi la kwanza ni wageni 20 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri wa Wizara ya Kazi, Vijana na Ajira ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini, wanaosoma shahada ya Mipango ya Maendeleo ya Mikoa mwaka wa pili. *(Makofi)*

Kundi lingine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Hadija S. Ally, Mbunge wa Viti Maalum, ambao ni Ndugu Rehema A. Mohamed, Ndugu Ghanima Sultani na Ndugu Lilian Ibrahim. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ni wageni wa Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar ambao ni Ndugu Silvia Shekilango, Ndugu Happy Mwinyipembe na Charity Mugabi.

Pia kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Esther Matiko ambao ni Ndugu Geofrey John Chacha mwanafunzi kutoka *UDOM* na Ndugu Dorton Kasmil.

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni 30 wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza ambao ni wanafunzi wa *UDOM* na wanachama wa KAUSA, hawa wanaongozwa na Ndugu Gaudin Gabriel.

Pia kuna mgeni wa Mheshimiwa Japhary Michael ambaye ni Ndugu Mbonea Charles Mshana, Diwani Manispaa ya Moshi.

Kundi lingine ni wageni watano wa Mheshimiwa Willy Qambalo ambao ni wanafunzi pia kutoka *UDOM* wanaosomea Ualimu wa Sayansi mwaka wa pili. Kundi lingine ni Wanafunzi 82 na Walimu watano kutoka shule ya sekondari Saint Marx, Dodoma, Wengine ni wanafunzi 136 wa Kitivo cha Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana wageni wote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la kikao cha Kamati ya Utendaji ya *CPA,* Tawi la Tanzania. Wajumbe wa Kamati hii wanaombwa wakutane leo tarehe 29 Aprili, saa nane mchana katika Ukumbi Na. 227 jengo la utawala ghorofa ya pili, wajumbe wote wa mkutano huo mnaombwa kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu!

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JOHN W. HECHE: Mwongozo wa Spika!

NAIBU SPIKA: Mwongozo Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7), wakati Naibu Waziri Mheshimiwa Jafo anajibu majibu yake hapa kuhusu swali la Wenyeviti wa Vijiji kulipwa mshahara au posho ametoa majibu ya jumla sana kwamba wanapelekewa asilimia ishirini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunajua Halmashauri hizi mapato yake yanatofautiana sana, kuna Halmashauri mapato yake ya ndani ni chini ya shilingi milioni mia nne na unakuta ina vijiji zaidi ya mia mbili au mia. Sasa ukichukua asilimia ishirini ile ukapeleka kwenye kijiji, haziwezi ku-*sustain* kulipa Wenyeviti wa Vijiji kwa mwaka mzima. Sisi tulichokuwa tunataka ni *commitment* ya Serikali kwa sababu hawa watu wanafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe umeonekana kuburuza tu na maswali ya msingi ambayo tulitakiwa tuulize ya nyongeza hukutoa nafasi hiyo, sasa naomba Mwongozo wako…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Heche naomba uombe Mwongozo wako, kwa sababu ukianza sasa kutoa maelezo marefu kama unachangia ni sawa na ungepewa fursa ya kuchangia, omba Mwongozo wako ni kitu gani unachokitaka.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo huwezi kuni-*interrupt* Kanuni inasema hivyo, ninachosema ni kwamba...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Heche usitunge Kanuni saa hizi, Kanuni ni hizi hapa, naomba uendelee kuomba mwongozo, naomba uombe Mwongozo ulionyoosha kwa ajili yake. *(Makofi)*

MHE. JOHN W. HECHE: Ambayo pia na mimi nimeisoma na nanukuu, naomba sasa Mwongozo wako kwamba inakuwaje Waziri anashindwa kutoa majibu ambayo yanatoa mwangaza kwa watu hawa ambao wanafanya kazi, lakini inaonekana analeta bla bla! ambazo hazina msingi humu ndani.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Juliana Shonza Mwongozo,

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru, nimesimama kwa Kanuni 149(1), (2), na (3) ambayo inatoa maelezo kuhusu mavazi rasmi ya Mbunge ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Upendo Peneza amevaa mavazi ambayo siyo rasmi ndani ya Bunge lako Tukufu, nilikuwa naomba kupata Mwongozo wako. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwanza Mwongozo wa Mheshimiwa Heche nitautoa baadaye. Mheshimiwa Juliana Shonza ameomba mwongozo kwa Kanuni ya 149, Waheshimiwa Wabunge Kanuni ndogo ya (7) na ya (8), Spika atakaporidhika kuwa Mbunge aliyetolewa taarifa kwa mujibu wa fasili ya (7) ya Kanuni hii hajavaa mavazi rasmi ataamuru Mbunge huyo atoke nje ya Ukumbi wa Bunge. Sasa Waheshimiwa Wabunge sijamuona Mheshimiwa Peneza kwamba amevaa vipi.

MBUNGE FULANI: Asimame!

(Hapa Waheshimiwa Wabunge walipiga Kelele)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane, Mheshimiwa Mbunge ameomba mwongozo kuhusu vazi la Mheshimiwa Upendo Peneza.

MBUNGE FULANI: Wivu wa kike, mlisema getini wana-*determine* nani amevaa vazi sawa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtu ambaye maana hapo juzi nilitoa uamuzi kuhusu Kanuni ya 139(2)(b) inasema wageni wakiwa ndani ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge watalazimika kufuata na kuzingatia masharti yafuatayo:-

(b) wanapaswa wawe wamevaa mavazi ya heshima na Kanuni inaishia hapo, lakini Kanuni ya 149 imetoa maelezo marefu kuhusu Mbunge na ya 3(a) inasema, Wabunge wanawake:

(I) Vazi lolote la heshima ambalo siyo la kubana mwili, lisiloonesha maungo, ambayo kwa mila na desturi za Kitanzania hayapaswi kuoneshwa na ni refu kuvuka magotini.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Pendo amekaa, kwa hiyo nitakapomuona amesimama nitatoa uamuzi. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Naibu Spika, safi sana.

NAIBU SPIKA: Katibu!

NDG. NEEMA H. MSANGI: Hoja za Serikali, hoja ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI Utumishi na Utawala Bora. Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadilio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 - Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Mbilinyi utulivu tafadhali. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wachangiaji Mheshimiwa Dua William Nkurua ambaye atachangia kwa dakika 10, karibu.

MHE. DUA W. NKURUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Nanyumbu kwa kunifanya kuwa kiongozi wao kama Mbunge na kuwa msemaji wao katika eneo hili, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa John Pombe Magufuli, kwa kazi kubwa anazofanya ambazo kila mtu mwenye dhamira ya kweli katika nchi yetu ni lazima amuunge mkono, kwa sababu analengo la kuwafanya Watanzania waishi maisha mazuri na Tanzania iwe sehemu salama ya kuishi watu. Nampongeza sana Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nianze kuchangia katika suala la elimu.

NAIBU SPIKA: Samahani kidogo Mheshimiwa Nkurua, upande wa Kambi Rasmi ya Upinzani naomba utulivu, kama ni kuongea muongee taratibu tafadhali. Mheshimiwa Nkurua endelea.

MHE. DUA W. NKURUA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Katika suala la elimu ni dhahiri kwamba, mkakati ambao umekuja na TAMISEMI unaonesha una dhamira ya kweli ya kupambana na hali halisi tuliyonayo sasa hasa ya mfumuko kwa watoto ambao wamezalishwa kutokana na tamko na Sera ya CCM inayotamkwa kwamba, sasa elimu itakuwa bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali kama hii ni lazima Serikali ijipange vizuri kuhakikisha kwamba yale mambo ya ziada ambayo lazima yaongezeke Serikali ianze kuweka mkakati. Kwa sababu tuna ongezeko kubwa la watoto tutahitaji Walimu wengi, tutahitaji nyumba nyingi za Walimu, tutahitaji madarasa ya kutosha kwa ajili ya kuweza kukabiliana na hawa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hii tusiziachie Halmashauri peke yake kujenga nyumba za Walimu na kuongeza madarasa, kwa sababu mapato ya Halmashauri nyingi nchini ni madogo sana. Kwa hiyo lazima Serikali ije na mpango utakaozisaidia Halmashauri kujenga nyumba za Walimu, madarasa na vifaa vingine. Waziri atakapokuja aje na mkakati utakaotuonyesha kwamba tumejiandaa kukabiliana na ongezeko kubwa la watoto katika mashule yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili, ni kuhusu suala la maji, maji ni tatizo katika nchi yetu hasa katika Jimbo langu la Nanyumbu. Kutokana na hali halisi ya mazingira na uoto tuliokuwa nao maji ni tatizo kubwa sana. Nashukuru bajeti hii imejitahidi kuonesha mikakati mbalimbali katika nchi nzima ya kupambana na shida ya maji, lakini naiomba Serikali iweke mkakati maalum na

wa kipekee, kuliondoa tatizo la maji katika Mji wa Mangaka ambapo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya na Nanyumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mtwara kwa ujumla una shida kubwa sana ya maji, naomba Serikali ijipange kama ambavyo imeshatoa maelezo na nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba, wananchi wa Tanzania wanapata maji ya kutosha ili waweze kufanya shughuli zingine za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maslahi ya Madiwani na Wenyeviti wa Halmashauri za Vijiji. Waheshimiwa Madiwani wanafanya kazi kubwa sana katika maeneo yao ya kazi, kila tatizo linalotokea katika maeneo yetu, watu ambao wananchi wanakwenda kuwafuata moja kwa moja ni Madiwani. Kwa hiyo, Madiwani ni lazima tuwatengenezee mkakati utakaowapa maslahi yatakayoweza kusaidia kukabiliana na kazi ambazo zinawakabili kwa sasa. Naomba maslahi ya Madiwani yaangaliwe na Wenyeviti wa Vijiji walipwe mshahara. Mkakati huu lazima uanzie huku Serikali Kuu, Halmashauri hazina uwezo huu ambao tunauzungumza leo.

Naomba Serikali iwalipe Wenyeviti wa Vijiji nao ni watu wanaofanya kazi kubwa sana katika nchi yetu, tusipowaangalia hawa tutakuwa hatutendi haki. Naomba suala hili tulipe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie asilimia 10 ambayo inapaswa iende kwa Vijana na akinamama, ni kweli Halmashauri nyingi nchini hazitengi pesa hii, hata kama zinapata mapato haya lakini hazipeleki asilimia 10 ya mapato yao. Naomba tutengeneze mpango ambao utakuwa endelevu na mpango ambao utazifanya Halmashauri ziweze kutimiza hiki kigezo, kwa sasa kuna mambo yanawashinda kufanya hii kazi ambayo tumewapa waifanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kwamba, asilimia 60 ya mapato ya ndani ya Halmashauri yanatakiwa yaende kwenye miradi ya maendeleo, asilimia 20 ya mapato ya Halmashauri ya ndani yanatakiwa yaende kwenye vijiji, asilimia 10 iende kwa wanawake na vijana. Asilimia 10 peke yake maana 90 tayari tumeshazigawa, kumi peke yake ndiyo ifanye kazi zingine ikiwa ni pamoja na posho za Madiwani, kuendesha vikao na kadhalika. Kwa sababu OC ambayo ingekwenda kule kusimamia posho za Madiwani na vikao haziendi kwa wakati. Kwa hiyo, inalazimu Halmashauri zitumie pesa ambazo zingeweza kwenda kwa akinamama na vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunataka kweli wanawake na vijana wapate pesa ni lazima Halmashauri zetu tuziongezee pesa, hii asilimia 10 tuliyowapa ni ndogo, tukumbuke kwamba Halmashauri zinalipa mchango wa *ALAT* - Taifa, Halmashauri zinalipa mchango wa *ALAT* - Mkoa, Halmashauri

zinalipa *loans board,* asilimia 10 ile ndiyo inafanya hiyo kazi, katika hali hii unatekeleza vipi hili agizo, ni vigumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakwenda kuwalaumu Waheshimiwa Wabunge hapa, Madiwani kule, tutawalaumu Wenyeviti wa Halmashauri, tutawalaumu Wakurugenzi lakini uhalisia haitekelezeki. Hao Madiwani ndiyo wanaosimamia hizi pesa ambazo tunazipeleka kwao, kikao hakifanyiki kwa sababu hawana pesa watasimamia vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, asilimia 10 iliyobaki haiwezi kumudu kuyafanya haya ambayo tunataka yafanyike, mazingira ni magumu sana tumewatengenezea hao watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tuheshimu bajeti, hapa tunajadili bajeti na hatimaye itapita. Naomba sana mambo yatakayopitishwa hapa yafanyike hayo hayo yasiongezeke njiani wala yasipungue njiani. Tuna uzoefu wa kutosha kwamba, mara baada ya bajeti yanatokea maagizo mengine ambayo Halmashauri sasa yanawachanganya. Ni kweli maagizo yanakuwa na lengo zuri kwa mfano, tutengeneze madawati kwa watoto wetu ni jambo jema, lakini halipo kwenye bajeti! Tunawaambia tujenge maabara ni jambo jema, lakini haikuwa kwenye bajeti. Kwa hiyo, kwa sababu haipo kwenye bajeti kinachotokea hao Waheshimiwa Madiwani na Wakurugenzi wanakwenda kuharibu mipango mingine ambayo ilipangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwaambia kwamba, wao watenge asilimia 10 ya mikopo ya akinamama na vijana maana tunalalamika sana Waheshimiwa Wabunge, mikopo, mikopo, Wakurugenzi hawatengi, watatengaje wakati wameambiwa wapeleke madawati na wamepewa *deadline* watafanya lini! Wameambiwa maabara tarehe fulani iishe, pale kinachoendelea mipango mingine baadaye, kipaumbele ni madawati na mabaara.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kama tunaruhusu watu waendelee kupewa maagizo nje ya bajeti, tukubaliane kwamba na asilimia 10 inaharibika tusilaumu, tunyamaze, haiwezekani! *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Sana.

MHE. DUA W. NKURUA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, kama tumekubaliana na hii bajeti twendeni tuiheshimu. Kule Nanyumbu tunao Viongozi wa Jadi tunaita Mamwenye, wengine mnaita Machifu, wengine mnawaita Watemi. Mamwenye kwa mila yetu anaposimikwa na kufanyiwa sherehe, mtu wa kwanza kwenda kumuamkia ni Baba Mzazi na Mama Mzazi wa yule Kiongozi. Hii ni *massage* kwa watu wengine kwamba, huyu anapaswa kuheshimiwa kuanzia leo. Sasa, kama kweli tunataka bajeti iheshimiwe mtu wa

kwanza kuheshimu bajeti ni Serikali. Naomba sana Serikali tuheshimu tutakayoyapitisha hapa ili ikatekelezwe kule kwa ufanisi ambao tumeutaka na hapo tutakuwa tumetenda jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nitataja baadhi ya majina ambayo watapata nafasi ya kuchangia, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mheshimiwa Azza Hillal Hamad na Mheshimiwa Edwin Sannda, Wabunge wengine watakuwa ni Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage.

Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu!

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Pia namshukuru Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Pwani kwa kunipigia kura na kunifanya kuwa Mbunge katika Bunge lako. Niungane na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Tano kwa kuanza kazi vizuri, nina kila sababu ya kumpongeza kwa matukio yafuatayo machache:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa usimamizi mzuri wa makusanyo ya mapato ambayo naamini yatatekeleza mpango wa maendeleo unaokuja na bajeti hizi ambazo zinaendelea. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uwekaji wa jiwe la msingi wa ujenzi wa *fly over* na naipongeza Serikali ya Japan ilikuwepo, napongeza kwa uzinduzi wa mradi wa Kinyerezi I pamoja na uwekaji wa jiwe la msingi kinyerezi II. Pia nampongeza sana Rais Museven kwa kukubali bomba la mafuta kupitia Bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayapongeza haya nikiamini kabisa viongozi wa Mataifa mbalimbali ya nje yana imani na Mheshimiwa Rais wetu, hawana tatizo na kuona kwamba mpaka sasa *instruments* hazijatoka, kwa sababu wanaamini wao ni kazi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo pia napongeza fursa ambayo Serikali ya China imeonesha kutaka kutu-*support* katika ujenzi wa reli ya *standard gauge*. Naipongeza kwa sababu China wanataka kutoa hela nyingi

lakini hawajapata kuuliza *instrument* ya Waziri wa Mawasiliano wala ya Waziri wa Ujenzi, naamini wao wanaamini hapa kazi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na pongezi hizo, naomba nijielekeze kwenye bajeti. Nampongeza Waziri wa TAMISEMI, pamoja na Waziri wa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora na Naibu Waziri wameanza kazi vizuri, wanashughulikia masuala ya mishahara hewa vizuri na wanapambana. Nikipitia hotuba ya Waziri wa TAMISEMI pamoja na mikakati ya mafanikio mbalimbali yaliyopatikana, naomba nijielekeze zaidi kwenye sekta ya afya. Katika kujielekeza sekta ya afya nimeona kupitia bajeti hii mkakati wa Serikali wa ujenzi wa vituo vipya vya afya, ujenzi wa zahanati, ukarabati wa hospitali za wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali iangalie sera, Wizara ya Afya nadhani ingekuwa vizuri kama ingepewa jukumu pia la usimamizi wa vituo hivi kwa sababu wao wanasimamia sera. Inapokuwa TAMISEMI na wao wana mambo mengi, lakini changamoto kubwa zipo kwenye maeneo ya vituo vya afya, ziko kwenye maeneo ya hospitali za wilaya na ziko kwenye zahanati. Kwa kuwa TAMISEMI wanaendelea kusimamia, lakini kwa kuwa haihusiani na masuala ya sera, usimamizi kidogo unakuwa hafifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijielekeza zaidi katika ujenzi huo wa zahanati na ukarabati nimeona bajeti ya mwaka 2014/2015 takribani bilioni 263 zilitumika, lakini mwaka 2016/2017 zimetengwa bilioni 27. Naona hiki kiwango ni kidogo nikiangalia changamoto ambazo zinatukabili na nazielekezea changamoto hizo kwenye hospitali yetu ya Wilaya ya Mkuranga ambayo haina *X-Ray;* kituo chetu cha afya cha Kibiti katika Wilaya mpya hakifanyiwa upanuzi wa jengo la wazazi; kwenye kituo chetu cha afya Mkoani Kibaha changamoto kubwa ni jengo la upasuaji, pia hata kituo cha afya Maneromango, vifaa vya upasuaji vipo, lakini jengo halipo. Nashauri katika kifungu hiki angalau kingeongezwa zaidi ili tuweze kupata huduma nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona wakati nikipitia hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani katika ukurasa wa tatu, nanukuu:

"Kambi Rasmi ya Upinzani inawataka Wabunge wa CCM waache kufanya ushabiki Bungeni".

Pia katika ukurasa huo huo nanukuu kwamba:

"Vyombo vya Habari vya Umma na Binafsi virushe moja kwa moja mijadala ili wananchi wajue fedha zao zinavyogawanywa katika Halmashauri zao na wajue ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali" mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977, Ibara ya 89 imeipa Bunge wajibu wa kutunga Kanuni za Uendeshaji wa Bunge hili, Kanuni za Kudumu za Bunge, Kifungu 116 zimempa mamlaka Spika kuunda Kamati, pia zimeipa mamlaka Kamati zenyewe kuchagua Wenyeviti wao wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Usimamizi wa pesa za Halmashauri *(LAAC)* na Kamati ya Hesabu ya Serikali *(PAC),* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge ambazo zinatokana na Katiba zinatakiwa ziongozwe na Wapinzani. Leo wanapoituhumu Serikali kuvunja Katiba, kuvunja taratibu mbalimbali, wao hawajitazami mpaka leo Wenyeviti wa Kamati hizo hawajachaguliwa, leo wanaposema Bunge lioneshwe *live* lakini wao hawajatimiza wajibu wao zaidi ya miezi minne, Kamati hazijapata Viongozi kutoka Kambi ya Upinzani na mamlaka hiyo ni ya Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekeni Kiongozi unajipangia utaratibu kuteua Wajumbe wa Kamati hukupewa mamlaka hiyo! Ni mamlaka ya Spika kuwapanga Wabunge kwenye Kamati zao kwa vigezo vyao na Kanuni tumetunga wenyewe za Bunge hili. Nilidhani wangetoa ushauri kwamba Kamati zinazoongozwa zipewe mamlaka zenyewe. *(Makofi)*

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Taarifa!

MHE. SUBIRA K. MGALU: Sasa tulia niendelee *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mgalu naomba ukae, Taarifa.

T A A R I F A

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa mzungumzaji anayeongea kwamba, hata Chama cha Mapinduzi, kabla ya kuleta Wenyeviti wa Kamati walikaa katika *Party Caucus* wakachagua majina, wakaleta kupitisha kama *procedure*. Kwa hiyo, napenda kumpa taarifa kwamba tulichofanya ni sahihi kwa sababu na Chama chake kimefanya hivyo. Nashukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mgalu taarifa hiyo unaipokea?

MBUNGE FULANI: Sema kanuni, sema kanuni.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa siipokei, kwa kuwa hakujielekeza kwenye Kanuni yoyote na mimi nimesema kama ana ushahidi wa *Party Caucus* kukutana ili kuchagua viongozi, walichaguliwa ndani

ya Kamati husika, hiyo taarifa yake siyo sahihi naomba watimize wajibu wao kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG (Controller and Accounting General)* amewasilisha ripoti yake, lakini najua kwa nini hawajachagua mpaka sasa hivi, wamepima maji wameona yana kina kirefu. Mheshimiwa Aeshi endelea na kazi, chapa kazi *PAC*, umegundua mambo, *LAAC* nayo endeleeni, chagueni Makamu Mwenyekiti aendelee na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze pia kwenye ukurasa wa mwisho wa hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, wanaelezea masuala ya vifungu vya Sheria ya Bajeti, kwa kuwa kitabu hiki kinatumika na Wabunge wote na ni upotoshaji, sasa nataka nijielekeze kwenye *Public Finance Act* hiyo, Kifungu 19 naomba wanavyo-*quote* Sheria za Fedha wamalizie wasi-*quote* nusunusu. Kifungu cha 19 kinasema; "*If at the close of account for any financial year it is found that moneys have been expended:-*

(a) on any expenditure vote in excess of the amount appropriated for it by an Appropriation Act;

(b) for a purpose for which no moneys have been voted and approaprated.

(c) the amount of excess expended or not appropriated as the case may be shall be included in a statement of expenditure.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mwaka wa fedha wa Serikali haujakwisha msiwahishe shughuli, mnapo-*quote* Sheria mbalimbali za Fedha mmalizie, mme-*quote Public Finance Act* 18 (a) na 14, kwa nini hamku-*quote* 19 ambayo ndiyo imetoa mamlaka mwisho wa mwaka wa fedha kama kuna pesa zimetumika za ziada ambazo hazikutengwa ziwasilishwe ndani ya Bunge katika taarifa maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha haujakwisha lakini kama pia pesa zilitumika zaidi na naomba kwenye masuala ya barabara, nimeona kwenye kitabu cha TAMISEMI mpango wa ujenzi wa barabara, namwomba tu Waziri wa Fedha mwaka wa fedha wa Serikali ukiisha awasilishe *statement*, tuipitishe kwa sababu yamefanyika mambo ya heri na mamlaka hiyo anayo, kwa hiyo hakuna uvunjaji wowote wa Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba niwazungumzie Wabunge Wanawake namna ambavyo hawashiriki vikao vya Kamati vya Fedha Halmashauri za Wilaya. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri, Ibara ya 66, imetaja aina za Wabunge wakiwemo Wabunge Wanawake. Wabunge wote wana haki

sawa, inashangaza kwamba Wizara ya TAMISEMI Katibu Mkuu anatoa mwongozo wa kuwatoa Wabunge Wanawake ambao wanasimamia maslahi ya wanawake, maslahi mapana na changamoto mbalimbali katika Kamati za Fedha, kama leo wanapoleta milioni hizo hamsini, asilimia 10 ya Vijana na Wanawake, mambo ya sekta ya afya, mambo ya kilimo, Mbunge Mwanamke na yeye ana mchango mkubwa kwenye Kamati ya Fedha ambayo inakutana kila mwezi, Wabunge wana uwezo wa kuchangia hoja na kujenga hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ya TAMISEMI tumelisemea kila siku, huu ni mwongozo tu, mtoe mwongozo kuwa Wabunge Wanawake na Madiwani Wanawake, tusibaguliwe na wala tusinyanyaswe, kwa sababu pia Katiba imekataza sheria yoyote inayoonesha ubaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Bajeti na naunga mkono kwamba hakuna uvunjaji wowote wa Kanuni wala wa Katiba, wanaposhutumu na wao wajitazame, wajisahihishe, kidole kimoja kinawatazama. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Venance Mwamoto atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kilolo ambao kwa kweli wamenirudisha baada ya miaka 10 kukaa *bench*, nawashukuru sana. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Mawaziri, kwa mwanzo mzuri wa kazi nzuri ambazo tumeshuhudia Mawaziri wetu wakifanya na kufuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia kuhusu *TASAF*, kwanza naishukuru Serikali kwa mradi mzima huu wa *TASAF*, tulianza na *TASAF* I na II ambazo zenyewe zilijikita kwenye ujenzi wa barabara, ujenzi wa shule, ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na kadhalika. Kazi ilifanyika vizuri na ilikuwa inafanyika kwa ushirikishi kati ya wananchi wa maeneo pamoja na mchango wa *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachosikitisha ni kwamba. baadhi ya maeneo na baadhi ya miradi ambayo ya awamu ya kwanza na ya pili mpaka leo haijamalizwa. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI naomba nikushauri, jaribu kufuatilia ile miradi ya *TASAF* ambayo haikumalizwa kwenye awamu ya kwanza na ya pili ili iweze kumaliziwa, kwa sababu inavunja moyo sana kuona miradi ile bado ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TASAF* III, napongeza uongozi mzima wa *TASAF* kutoka Makao Makuu mpaka Waziri husika. *TASAF* III ni *TASAF* ambayo imelenga kuondoa au kupunguza umaskini kwa wananchi, wamefanya kazi kubwa sana. Tumetembea baadhi ya maeneo tumeona jinsi ambavyo wananchi wameanza kubadilika. Kuna matatizo madogo madogo ambayo kama Serikali inabidi iangalie.

Moja ni kwamba wale wanaosimamia *TASAF* wakiwemo Wenyeviti wa Vijiji, wao wanasimamia kuwapa fedha wale watu maskini lakini wao hawalipwi, hawana posho Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji anasimamiaje mtu kugawa nyama, wakati yeye mwenyewe hali, haiwezekani! Matokeo yake watu ambao wanaingizwa kwenye *TASAF III* wengine siyo wahusika, wanaingia baadhi ya ndugu wa viongozi, baadhi ya watu ambao wana nguvu zao, baadhi ya watoto wadogo, maana ya *TASAF* inaharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Mheshimiwa umesikia, muangalie na mfikirie jinsi gani ambavyo Wenyeviti wa Vijiji, iwepo sheria kabisa ya kutamka kwamba walipwe shilingi fulani, badala ya kusema Halmashauri zichangie asilimia hii itakuwa haiwezekani, kwa sababu kama Serikali wenyewe tumeshindwa kupeleka fedha kwa wakati, Halmashauri ambazo nazo zinategemea mapato ya ndani zitumie katika zile fedha ambazo Serikali ilikuwa ilete, kweli Mwenyekiti atapata hiyo fedha? Kwa hiyo tuiangalie, tuitungie sheria ili Wenyeviti walipwe, inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna jambo lingine naomba Waziri wa TAMISEMI uje utoe ufafanuzi, kwa sababu *TASAF* wanapeleka fedha kwa watu maskini ili kupunguza umaskini na yule mtu maskini ile fedha anaitumia kwa ajili ya kupika vitumbua, maandazi, anauza nyanya au mama lishe ili apunguze umaskini, lakini cha ajabu Halmashauri zetu zinakwenda kuwalazimisha kulipa ushuru wale watu maskini. Zinamwaga bidhaa zao, wanawekwa ndani kitu ambacho sasa hatujui tunawafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TASAF* inapeleka fedha kupunguza umaskini, Halmashauri inaongeza umaskini kwa kuwatoza kodi na kuwanyanyasa. Naomba Mheshimiwa Waziri utoe tamko kwamba hizi kodi ndogondogo za hawa watu, ambao ni watu wa chini, maskini, ambao kwa kweli anatafuta fedha kwa ajili ya kununua unga ili aweze kupika ugali ale na familia yake, siyo biashara. Halmashauri zijikite kutafuta biashara zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha nyingi za Mfuko wa *TASAF* tunategemea kutoka nje, Serikali nafikiri imekuwa ikipanga fedha mara nyingi, lakini zile fedha hazijaenda kule. Nafikiri safari hii kwa kuwa tumeamua sasa kubadilika, kufanya kazi na kudhibiti mapato, basi Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha na kuunga mkono kwenye Mfuko wa *TASAF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kuhusu ukubwa wa Wilaya ya Kilolo. Wilaya ya Kilolo lilishaletwa ombi awamu iliyopita, ikakubalika kwamba igawanywe, eneo ni kubwa lina takribani ukubwa ambao ni sawa na Mkoa wa Kilimanjaro , lakini mpaka sasa hivi siyo rahisi kwa mwananchi wa Kilolo kuona ile *impact* ya fedha ambayo inapelekwa kwenye ile Wilaya na kugawanya kwenye Kata zote. Kwa kuwa tayari mmegawa Halmashauri, tumepata Halmashauri ndogo ya Ilula, Serikali iamue ile iwe Halmashauri ndogo, hii iwe Halmashauri kamili ili baadaye muangalie uwezekano wa kugawa Jimbo hilo na kupata Jimbo lingine kwenye Wilaya zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite katika sehemu ya miundombinu. Wilaya ya Kilolo ni Wilaya ambayo ndiyo inayotegemewa kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali, tatizo lake kubwa ni miundombinu. Miundombinu ambayo ipo ni ile ile ya miaka 10 iliyopita. Hivyo, nafikiri kwamba, barabara zetu ambazo tumeziomba zipandishwe hadhi, ikiwepo barabara ya kutoka Idete kwenda Itonya, Muhanga kwenda kutokea Morogoro, ipandishwe hadhi iwe barabara ya mkoa, ili iwe rahisi zaidi kufungua maendeleo kwa wananchi wa Wilaya ya Kilolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni suala la Wazee. Wazee pamoja na kuwa tumetamka kwamba wanatakiwa wapewe huduma bure pamoja na matibabu, lakini bado hatujawawekea utaratibu mzuri. Nashauri kwamba katika zahanati, *dispensary* na hospitali zetu litengwe eneo maalum kwa ajili ya huduma za Wazee, ili Mzee akifika pale hana sababu ya kukaa foleni kwa sababu sisi sote ni wazee watarajiwa, yale ambayo tunayafanya leo yatakuja kuturudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nina muda bado kidogo, zingumzie habari ya Wakuu wa Wilaya. Na-*declare interest* nilikuwa Mkuu wa Wilaya. Kazi ya Mkuu wa Wilaya ni kubwa, kwa sababu kinapotokea kipindupindu anayeulizwa ni Mkuu wa Wilaya, wanapotokea wafanyakazi hewa anayebanwa ni Mkuu wa Wilaya, unapotokea ujenzi wa maabara anayebanwa ni Mkuu wa Wilaya, yanapotakiwa madawati anayeulizwa ni Mkuu wa Wilaya, zinapoongezeka mimba mashuleni anayeulizwa ni Mkuu wa Wilaya, lakini uwezeshwaji wa Mkuu wa Wilaya bado haujakaa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *OC* ambazo wanapelekewa Wakuu wa Wilaya zinapita mikono mingi, nashauri kwamba isipunguzwe ile hela ya maendeleo ambayo imepangwa kwa ajili ya Mkuu wa Wilaya zipelekwe moja kwa moja kwake, kwa sababu haifurahishi kuona kwamba, Wakuu wa Wilaya wanakuwa ombaomba. Mtu ambaye anasimamia maendeleo na haki anatakiwa aombe hata mafuta, haipendezi!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo basi, kama kifungu kipo kiende moja kwa moja bila kuguswa na *RAS (Regional Administrative Secretary)* au Mkuu wa Mkoa, kiende kwa Wakuu wa Wilaya moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Kwanza niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Bunda na kwa bahati nzuri nina Kata saba, kwa hiyo, niwashukuru wapiga kura wa Nyamang'uta, Nyamswa, Salama, Mihingo, Mgeta na Hunyali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Wabunge wote nikiwemo mimi mwenyewe, hatua ya kufika hapa ni ndefu sana. Kwa kweli, Mwenyezi Mungu ametusaidia tumefika hapa wote, jambo la kwanza naomba tupendane, hii habari ya kushabikia vyama na kunyoosheana vidole itakuwepo, lakini iwe kwa wastani, kwa sababu wote tunaishi kama binadamu na tukifa au tukifiwa tunaenda kupeana pole, kwa hiyo tunapokuwa humu ndani naomba tupendane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi naomba Wabunge wa CCM wajue kwamba, nchi hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumekabidhiwa sisi, hawa jamaa zetu wapo tu kwa kupinga na kupiga kelele. Kwa hiyo, tunatakiwa tufanye kila la maana kuwatendea haki Watanzania ili tunapofika 2020 hawa watakwenda kuuliza, tuliwaambia CCM hamuwezi sasa mnaona mmefanya nini? Kwa hiyo, tufanye kila la maana ili nchi yetu iweze kupata maendeleo ikifika 2020 tuwaoneshe kwamba tumefanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais, sijui huwa najiuliza mara mbili mbili hivi kuna nini? Kwa sababu kabla ya mambo yote tunasema nchi inaliwa, nchi mbovu, hali mbaya, tunalia kila mahali, leo tumepata jembe, tingatinga anapiga kila upande bado watu wananung'unika nini? Hivi nchi hii tusipopata Rais nje ya Magufuli tunapata Rais wa aina gani? Kilichobaki ni kusahihishana tu pale na hapa mambo yanakwenda sawa, lakini Rais anafanya kazi nzuri sana.nn*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze kwenye utawala bora. Katika utawala bora naangalia mafunzo ya Halmashauri za Vijiji, Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata. Tumekuwa na tabia ya kuchagua viongozi halafu hatuwapi mafunzo, hata humu ndani Wabunge tumo tu, hatukupata mafunzo bora, juzi nilikuwa namuuliza mwenzangu hapa, hivi maana ya mshahara wa Waziri ni

nini? Ananiambia na mimi sijui! Unashika mshahara wa Waziri, mshahara uko benki wewe unaushikaje? Anasema sijui. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitakiwa kuelezwa kwamba hivi vitu vinakwendaje, kuna *Vote*, kuna *sub-vote*, kuna *program* tulitakiwa tupewe mafunzo. Mafunzo kwa Watendaji wa Vijiji ni jambo la msingi sana, lakini imezungumzwa hapa habari ya Wenyeviti wa Vijiji kulipwa mshahara au kupewa posho. Serikali za Halmashauri au Halmashauri za Wilaya haziwezi kutoa posho, hilo tukubaliane!

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wote tumetokea maeneo hayo, tumetoka kwenye vijiji, tumetoka kwenye Kata tunakuwaje hatuwatetei watu hawa wapate posho nzuri? Tunapaswa kufanya kila namna Watendaji wa Halmashauri za Vijiji, Wenyeviti wa Vijiji wapate posho nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo nizungumzie habari ya migogoro ya mipaka. Kuna migogoro ya mipaka ya Wilaya na Wilaya, kuna migogoro ya mipaka kati ya Kata na Kata, kuna migogoro ya mipaka kati ya Vijiji na Vijiji na ni mingi sana, kwenye Jimbo langu ipo katika kila eneo. Tunaomba Wizara zinazohusika na maeneo hayo, TAMISEMI na Ardhi washirikiane kumaliza migogoro hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Shule za Msingi, jambo ambalo Bunge la Kumi na Moja tutafanya na tutapata heshima ni kupata madawati ya watoto, madawati ya wananfunzi katika shule za msingi. Ukienda shule ya msingi ukiingia darasani watoto wanaamka wanakusalimia shikamoo mzazi, unasema marahaba, halafu unawaambia kaeni chini au unafanyaje? Wanakaa kwenye vumbi! Huwa najiuliza, naomba Waziri Mkuu afanye kazi mmoja, tufanye kazi moja au kazi mbili tu na nitoe njia. Kwanza, tukubaliane kwamba Bunge hili Bajeti yoyote kutoka Wizara mbalimbali ikatwe tupate bilioni 150 za kuweka madawati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepiga hesabu hapa yamepungua madawati 1,500,000 kama milioni nne, kwa hiyo, tukipata bilioni 160 au 170 maana yake madawati nchi nzima yanakuwepo. Waheshimiwa Wabunge tukitoka hapa tutakwenda kupambana na tatizo la madawati hamtakwepa, saa hizi kuna meseji zinazotoka kwa *DED* ooh! Mheshimiwa Mbunge hela yako ya Mfuko natengenezea madawati, nani kakutuma utengeneze madawati mimi sijafika huko?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tukubaliane kwamba madawati ni jambo la kwanza katika Bunge hili. Tutoke humu tujue kwamba tunakwenda kupata madawati nchi nzima, tukisema hii ya Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa tumetofautiana kipato katika Mikoa. Dar es salaam watatengeneza,

Arusha watatengeneza, Bunda je, ambayo ni Wilaya ya maskini? hawawezi kutengeneza madawati! Kwa hiyo, nafikiri kwamba jambo la msingi sana kufanya mambo kama haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kama hatuwezi kuweka bajeti bilioni 160 kutoka Wizara mbalimbali, tukubaliane na Waziri Mkuu aunde Kamati ihusishe Kambi zote, Kamati itafanya kazi moja ya kujua idadi ya madawati nchi nzima, lakini kujua mashirika mbalimbali. Kwa mfano, tukasema hivi ukiweka shilingi tano katika Makampuni ya Simu, ukiweka shilingi tano kwa Makampuni ya Mafuta, ukiweka taasisi mbalimbali tulizonazo, hatuwezi kupata bilioni 160? Inawezekana! Waziri Mkuu aunde Kamati ili tuweze kupata watu, wafanye tathmini, watuletee hapa, wote tuchange.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Bunge letu limechanga, tumechanga bilioni sita au uwongo jamani?

MBUNGE FULANI: Kweli!

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, tumechanga bilioni sita kutokea Bungeni humu ndani, tunataka Mashirika mengine yote na Taasisi zingine zichange.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yangu kwa leo yalikuwa hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Josephine Genzabuke atafuatiwa na Mheshimiwa Azza Hilal Hamad, halafu Mheshimiwa Edwin Sannda ajiandae.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri George Simbachawene na Mheshimiwa Angellah Kairuki, Naibu Waziri, Mheshimiwa Jafo pamoja na Viongozi wote walioko kwenye Wizara zao. Nawapongeza kwa hotuba zao nzuri**.** *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu suala la afya, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa kutembelea hospitali ya Muhimbili, baada ya yeye kutembelea Muhimbili huduma zimeboreka, hakukuwa na kipimo cha *MRI*, *MSD* imeanzisha duka pale Muhimbili, wananchi wanapata huduma ya kupata dawa kwa bei rahisi. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie Mkoa wetu wa Kigoma. Serikali kwa kushirikiana na wananchi walijenga vituo vya afya, wakajenga zahanati, hii ni katika nchi nzima, lakini zahanati pamoja na vituo vya afya

vilivyojengwa havina watumishi. Watumishi limekuwa ni tatizo, dawa limekuwa ni tatizo, vifaa tiba limekuwa ni tatizo. Kwa mfano, katika Mkoa wetu wa Kigoma, Mkoa wa Kigoma una Wilaya saba, Mkoa wa Kigoma umekumbwa na wimbi kubwa la Wakimbizi. Wakimbizi wanatibiwa kambini lakini wakati mwingine wanaletwa kwenye hospitali za wilaya. Mkoa wa Kigoma hauna Daktari Bingwa, Hospitali ya Maweni Daktari Bingwa ni mmoja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu fikiria, wananchi wa Wilaya zote saba wanapewa rufaa, wanapelekwa kwenye hospitali ya Maweni ambayo ndiyo hospitali ya Mkoa, lakini Daktari Bingwa ni mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuletewe Madaktari katika Mkoa wa Kigoma. Najua Muhimbili wapo Madaktari wa kutosha lakini huku Mikoa ya pembezoni Madaktari hawatoshi. Kwa kuuangalia Mkoa wa Kigoma naomba upewe kipaumbele kutokana na wimbi kubwa la Wakimbizi kutoka DRC na Burundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kasulu lipo vile vile tatizo la upungufu wa Watumishi, hatuna *ultra sound*, wanawake wanateseka, wanapata shida wanapokwenda kuambiwa wapimwe, wanakuta *ultra sound* hamna, hawawezi kujua mtoto amelalaje tumboni, kwa hiyo wanalazimika kwenda katika hospitali za kulipia. Naomba tuletewe *ultra sound* kuwaondolea adha wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Wauguzi ni wachache, utamkuta Muuguzi mmoja pengine yupo kwenye wodi ya akinamama, akinamama wanaotaka kujifungua wako nane ama kumi, Wauguzi wapo wawili, wanawake wanaohitaji kujifungua wako kumi, hebu angalia tofauti iliyopo, watu wawili kuhudumia watu kumi! Matokeo yake wanawake wanapoteza maisha na wakati mwingine watoto wanazaliwa wakiwa wamekufa? Naomba tuongezewe Waganga pamoja na Wahudumu wa Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia suala la maji. Nimewahi kusema Tanzania tumejaliwa kuwa na vyanzo vingi vya maji; maziwa, mito mikubwa na midogo lakini maji yamekuwa ni tatizo kubwa linalowakumba wanawake. Naomba Serikali itenge pesa kwa ajili ya kufikisha maji vijijini ili kuwaondolea adha wanawake ambao wamekuwa wakiteseka kwa muda mrefu. Utamkuta mwanamke muda mwingi anatumia kwenda kutafuta maji, anashindwa kufanya shughuli za uzalishaji mali. Kwa hiyo, naomba Serikali itenge pesa, ipeleke pesa ili maji yaweze kufikishwa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mji wa Kasulu lipo tatizo la mabomba kutoa maji machafu, Serikali imekuwa ikitenga pesa kupeleka Kasulu kwa ajili ya kuanzisha miradi iliyokwishaanzishwa katika Wilaya ya Kasulu. Naomba kupitia

bajeti hii mtupelekee pesa ili miradi iliyoanzishwa iweze kukamilika. Mtupelekee pesa kwa ajili ya Mji wa Kasulu ambao maji yanatoka machafu bombani ili maji yaweze kutibiwa, kwa sababu maji yakiwa siyo salama ni hatari kwa maisha ya binadamu. Ipo miradi ya Kasangezi, Ahsante Nyerere, Heluwishingo na Nyarugusu pamoja na Nyumbigwa naomba pesa zipelekwe ili miradi hiyo iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Walimu walipwe stahiki zao kwa sababu ni kilio cha muda mrefu. Walimu wanateseka sana wakati mwingine Mwalimu anahamishwa kutoka kituo hiki kupelekwa kituo kingine lakini halipwi pesa ya uhamisho. Siyo hivyo tu Walimu wanapata shida, hela za matibabu hawapewi, sisi tunapata pesa ya matibabu lakini Mwalimu hapewi pesa ya matibabu, hivi kwa nini Mwalimu anatengwa? Wakati mwingine anaweza kwenda akapewa hata sh. 20,000 au sh. 40,000. Hivi kweli mtu unampa sh. 20,000 au sh. 40,000, shika hizi kwanza zikusaidie halafu nyingine utadai! Naomba watendewe haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wastaafu nao; naomba wanapostaafu pesa zao ziwafikie mara moja, wengine wamekuwa wakistaafu wakiwa wamerekebishiwa mishahara, lakini Serikali inashindwa kurekebisha mishahara yao kulingana na jinsi walivyopanda madaraja, matokeo yake wanastaafu wakiwa na mishahara ile ambayo walikuwa nayo huko nyuma. Ile ambayo wamepandishwa madaraja na wamekiri kupanda daraja inachelewa kufanyiwa marekebisho, matokeo yake wanapata pensheni ambayo hailingani na mishahara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuja na wazo la kukarabati shule za sekondari ambazo ni kongwe, kwa mfano, Tabora *Boys*, Tabora *Girls*, Pugu na kadhalika. Naomba Serikali itenge pesa na Kigoma Sekondari nayo iweze kukarabatiwa, hii ni shule kongwe, naomba Serikali iweze kuikumbuka Sekondari ya Kigoma ambayo ndiyo amesoma Mheshimiwa Zitto, amesoma Kigwangallah, na wengine wengi. Naomba shule hiyo ikumbukwe, ni shule kongwe nayo ipelekewe pesa kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo kuhusu milioni 50. Naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutenga shilingi milioni 50. Imekuwepo mikakati mingi kwa muda mrefu ya kutenga pesa kwa ajili ya kuwapelekea vijana na wanawake, lakini mipango hiyo imekuwa haitekelezeki, zilipelekwa pesa kidogo kidogo kupitia *SIDO,* kupitia *SELF*…..

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Sannda na Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, ajiandae.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote. Amenipa afya njema na hatimaye kusimama katika Bunge lako Tukufu. Kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika bajeti hii, natumia fursa hii kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Shinyanga kwa kuniamini kwa mara nyingine kuweza kuwatumikia. Nawaahidi sitowaangusha kama kawaida yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Magufuli. Mheshimiwa Rais hongera sana pamoja na Baraza lako la Mawaziri, chapeni kazi, tuko bega kwa bega na ninyi mpaka kieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze katika hotuba ya Waziri wa TAMISEMI. Ukurasa wa 65 anasema ujenzi wa miundombinu ya Mikoa na Wilaya mpya. Baada ya kusoma hotuba ya Waziri wa TAMISEMI nimesikitika sana kwa sababu maeneo ambayo yanatazamwa ni maeneo mapya ya utawala, wakati kuna maeneo yaliyopo ya zamani hayana miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mfano wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ni Halmashauri mama kwa Mkoa wa Shinyanga, ni Halmashauri ambayo imezaa Wilaya zote na Halmashauri zote za Mkoa wa Shinyanga. Hivi sasa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga iko ndani ya Manispaa ya Shinyanga, majengo yake yako ndani ya Manispaa ya Shinyanga. Halmashauri za Wilaya ya Shinyanga ina Tarafa tatu, Kata 26, Vijiji 126, ina watu laki 355,930.

Mheshimiwa Naibu Spika, lilitoka agizo kwa Mkuu wa Mkoa kwamba tunapaswa kuhamia kwenye maeneo yetu ya utawala, tusifanyie vikao Manispaa ya Shinyanga. Kinachonishangaza unapotuambia tuhamie kwenye maeneo yetu ya utawala hatuna chumba hata kimoja cha ofisi, vikao vyote vya Baraza la Madiwani kwa sasa hivi vimehamia eneo moja la Iselamagazi ambapo ndiyo tulitenga kuwa Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafanyia wapi vikao vyetu? Tunafanyia kwenye majengo ambayo ni ujenzi wa hospitali ya Wilaya. Inasikitisha na inakatisha tamaa, kama tunasema tunataka kupunguza matumizi, unapunguzaje matumizi kwa kuondoa gari za Halmashauri zaidi ya sita kutoka Manispaa ya Shinyanga halafu zikafanye vikao zaidi ya kilometa 80, hayo matumizi unayapunguzia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa TAMISEMI aliangalie hilo. Hoja siyo kuangalia maeneo mapya, angalieni na maeneo ambayo ni ya muda mrefu ambayo yanahitaji miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kulisema hilo, naomba sasa nijielekeze upande wa afya. Nimepitia bajeti yote ya TAMISEMI katika vitabu vyote lakini sijaona, Mkoa wa Shinyanga tuna ujenzi wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga, sijaona tumepangiwa kiasi gani cha fedha. Siku zote nimekuwa nikisimama humu ndani nasema hospitali ya Mkoa wa Shinyanga ina msongamano mkubwa wa wagonjwa, ukizingatia Wilaya zetu zote hazina hospitali za Wilaya isipokuwa Wilaya ya Kahama. Nilitegemea basi katika bajeti hii nitaona bajeti ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga, lakini sijaona! Kama ipo naomba Waziri uniambie iko wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini gharama yake ni zaidi ya bilioni 10. Toka ujenzi huu umeanzishwa kwa nguvu za wananchi, Serikali imechangia milioni 270 tu mpaka hivi tunavyoongea, bado mnatuambia turudi kwenye maeneo yetu ya kazi, tunarudi kwenda kufanya kazi gani wakati hata miundombinu haituruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea nini iwapo hospitali hizi hatujazikamilisha, bado naendelea kusema hospitali ya Mkoa wa Shinyanga itakuwa na mrundikano wa wagonjwa kwa sababu hatuzitazami Wilaya zetu, miundombinu yake ikoje na wale ambao wameanzisha ujenzi wa hospitali hizi hamjatutengea fedha hata kidogo. Inasikitisha, naomba mtutazame Mkoa wa Shinyanga na mtazame Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, imeanzisha ujenzi wa hospitali ya Wilaya. Kwa sasa hivi taratibu imeanza kufanya kazi lakini kuna baadhi ya majengo hayajakamilika na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu imeomba ombi maalum la shilingi milioni 600 angalau kujaribu kusogeza tu zile huduma, sijui ombi hilo mpaka sasa hivi limefikia wapi? Hiyo yote ni kujaribu kuondoa msongamano mkubwa uliopo katika hospitali ya Mkoa wa Shinyanga. Naiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri namwomba sana atutazame kwa jicho la huruma Mkoa wa Shinyanga kwa sababu hatuwatendei haki wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi yanayotakiwa katika hospitali ya Wilaya ya Kishapu ni bilioni tatu, lakini tumeomba milioni 600, sijui imefikia wapi, nitaomba majibu Waziri utakapokuwa umesimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuishauri Serikali, huu utaratibu wa kila mwaka kuanzisha majengo mapya kama Wilaya imeanza mpya, Halmashauri mpya, mnaanzisha majengo, hebu tuusitishe, tumalize kwanza miradi iliyopo. Hakuna sababu ya kila siku kuanzisha miradi wakati tuna magofu mengi hayajakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila ninaposimama humu ndani huwa nasema, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga tuna zaidi ya zahanati 28 ambazo tumeanza kujenga ambazo hazijakamilika. Tuna zaidi ya vituo vya afya nane ambavyo havijakamilika, sijaona kwenye bajeti hii tunafanya nini. Niombe tusianzishe miradi mipya, tukamilishe kwanza ile iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa watumishi katika Wizara ya Afya. Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, mahitaji yake katika watumishi wa afya ni 726, watumishi waliopo ni 227, upungufu ni 499. Tunategemea watu hawa wanafanya kazi kwa kiasi gani? Nawaomba sana tuangalieni muweze kutuongezea watumishi ambapo tuna upungufu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielekee upande wa maji. Nasikitika sana Bunge lililopita la mwezi wa Pili Mheshimiwa Naibu Waziri Suleiman Jafo alijibu swali langu la Mradi wa Maji wa Mji Mdogo wa Tinde, alisema ndani ya Bunge kufikia mwezi wa Nne Mradi wa Maji wa Mji Mdogo wa Tinde utakuwa umekwishaanza kufanya kazi, lakini mpaka hivi ninavyoongea hapa mradi haujakamilika na SHIWASA hawajapewa fedha ambayo ilikuwa imebaki. Nawaomba sana mtakaposimama kujibu, Waziri wa Fedha aniambie ni kitu gani ambacho kimesababisha mradi huu ulikuwa ukamilike kutoka 2014 na mpaka leo ni milioni 100 tu inayosumbua ili mradi ukamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, nijielekeze katika mradi wa *TASAF*. Mradi wa *TASAF* wa awamu ya tatu ni mradi mzuri sana, kinachosikitisha Kamati zilizowekwa pamoja na baadhi ya watendaji wanautumia mradi huu kwa kudanganya, kuweka watu ambao hawastahili kupata ruzuku hii. Niombe ukafanyike uhakiki wa kila kaya kwa wale ambao wamechukua ruzuku hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, niwashauri Serikali, Mheshimiwa dada yangu Kairuki, kwa sababu *TASAF* imeazimia kuwasaidia watu hawa upande wa afya, isiwe ombi, iwe ni sheria kwa watu wote wanaopewa ruzuku kutoka *TASAF* wakatiwe bima ya afya moja kwa moja na wasipewe zile pesa wapewe huduma ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Mheshimiwa Subira upande wa Wabunge wa Viti Maalum. Imekuwa ni mazoea Wabunge wa Viti Maalum hawaruhusiwi kuingia kwenye Kamati za Fedha. Ukienda Halmashauri zingine wanaingia. Namwomba sana Waziri Mkuu atuangalie Wabunge wa Viti Maalum, mnatuogopa nini kuingia kwenye Kamati za Fedha? Kila unapokwenda Wabunge wa Viti Maalum hawaruhusiwi kuingia kwenye Kamati za Fedha, naomba sana Wabunge wa Viti Maalum turuhusiwe kuingia kwenye Kamati za Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwaomba Wenyeviti wa Vijiji waweze kulipwa posho ukizingatia asilimia 20 haifiki.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Azza, muda wako tayari.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Edwin Sannda, Mheshimiwa ConchestaRwamlaza ajiandae atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa niweze kuchangia kwenye hotuba ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nawapongeza Mawaziri wote wawili kwa hotuba zao nzuri sana, zimesheheni mambo mengi, hata hivyo, pamoja na hotuba nzuri napenda kutoa maboresho kwenye maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni suala zima la utawala bora na uwajibikaji. Taarifa na hotuba inaeleza vizuri baadhi ya watumishi ambao wamekuwa wakifanya makosa na wakivuruga wanawajibishwa kwa kufuata taratibu za kinidhamu na hatimaye pia za kijinai. Wapo ambao pia wamepelekwa Mahakamani, wapo ambao wamefukuzwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa hii inaonesha tuko vizuri sana katika utaratibu huu, lakini kiuhalisia nikitoa mfano wa Halmashauri kama ya kwangu ya Kondoa Mjini wamekuwepo watu wengi sana ambao wamekuwa wakivuruga hasa Maafisa Ardhi, hata Mkurugenzi aliyekuwepo. Kinachotokea badala ya kuwajibishwa kutokana na makosa yaliyofanyika, wanahamishwa. Sasa unapomhamisha huyu mtu unahamisha tatizo siyo? Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Mawaziri, badala ya kufanya suala la kuwa-*reshuffle* hawa watumishi wanaovurunda, taratibu za kuwawajibisha kinidhamu na hatimaye kijinai zifanyike kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na Maafisa Ardhi wengi sana wamekuwa wakituvuruga, anatoka Kondoa anapelekwa Rombo, anatoka Rombo anapelekwa sijui eneo lingine, wanaenda kuhamisha matatizo tu hayo. Pia wapo ambao kesi zimepelekwa Mahakamani, lakini wanatoka pale wanakwenda Makao Makuu TAMISEMI, wanasema sijui wamekaa benchi au vipi, sasa utaratibu huu haujengi nidhamu ya kuwafanya hawa watumishi wengine wawe waadilifu na wafanye kazi zao kadri ya miongozo na taratibu zinavyowataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri huu utaratibu wa kutumbua majipu, huku kwenye Halmashauri zetu uende vizuri kabisa, watu kweli watumbuliwe maeneo yote, siyo mtu anavuruga halafu anahamishwa, hii haitatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, ipo hali ya baadhi ya watumishi kutokuwajibika, mfano, sasa hivi Halmashauri yangu ni zao la Halmashauri iliyokuwepo, wale wote ambao walionekana kwamba *they are non-performance*, wanahamishwa wanapelekwa kwenye Halmashauri mpya, kweli hakuna utaratibu tunaoweza kujiwekea kupima *performance* ili hawa ambao mwisho wa siku hawa-*perform* wawajibishwe? Nafikiri hilo ni suala muhimu sana la kuliangalia Waheshimiwa Mawaziri, ili watumishi wetu wanaokuwa Serikalini na kwenye hizi Halmashauri waweze kuwa wawajibikaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala zima la elimu, kwenye elimu naongelea suala la Walimu, nikianza na upungufu wa Walimu. Upungufu wa Walimu ni tatizo kubwa, najua utaratibu unafanywa ili Walimu wengine watoke vyuoni waweze kuingia kwenye mashule kufundisha, lakini wanapotoka upungufu ni mkubwa sana hapa katikati, shule zinateseka, wanafunzi wanaumia, wanashindwa kupata masomo yao kadri inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kwangu kwenye elimu ya Sekondari tuna upungufu wa Walimu zaidi ya 80. Jibu dogo tu la Kondoa Mjini upungufu zaidi ya Walimu 80, kwenye shule ya msingi kuna upungufu wa Walimu zaidi ya 60. Mpaka waje kutimia na mahitaji najua ni ya nchi nzima, utakuwa mtihani mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nishauri kitu kimoja, wapo wale Walimu ambao *in the interim* kama mpango wa muda mfupi tu wakati tunasubiri uzalishaji wa wale Walimu wengine wapya. Wapo Walimu ambao walistaafu, haiwezekani tukawapa mikataba ya muda mfupi, wa- *fill* hii *gap in the interim* wakati tunasubiri hao wengine wanakuja, itusaidie kidogo kupunguza makali ya upungufu wa Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niliweke hilo kama changamoto na mapendekezo ya kuboresha hawa Walimu ambao tunazungumzia wanadai

mafao, wanadai malimbikizo ya mishahara, hebu tuwatumie wale wanaweza wakatusaidia kwa muda mfupi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa hapo, katika suala la Walimu, najua hili litamgusa zaidi Waziri wa Elimu Profesa Ndalichako, pia nataka niliweke hapa kwenu, Walimu na nilizungumza kwamba mkazo wangu upo sana kwenye elimu. Walimu watokane na *best performance*, siyo Walimu watokane na yale madaraja ya mwisho ndiyo wanaenda kuwa Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kufanya ni kuboresha maslahi yao pia kuwa-*remunerate* vizuri, kuwa- *compensate* vizuri na kwa kuwa ajira yao itakuwa inaonekana ina uhakika zaidi na iko vizuri wanafunzi wengi watataka kwenda kufanya hii kazi ya Ualimu. Tutakuwa tumewa-*motivate*, tumewa-*inspire*, matokeo yake kazi ya Ualimu itaonekana ni kazi yenye heshima, siyo kazi tu ya wale wanaofeli. Wanalipwa vizuri, wanatengenezewa mazingira mazuri ya kazi, matokeo yake inawa-*motivate* na kuwa-*inspire* watoto wetu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Profesa Ndalichako katika marekebisho yetu tunayoyafanya, moja ya vitu vya kuhakikisha vinarekebishwa ni kuona kwamba Walimu wanatokana na *best performance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa hapo elimu, naomba sana hili najua linaenda zaidi kwa Profesa Ndalichako Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi tena, tubadilishe huu utaratibu wa madaraja, tunasema ufaulu ni asilimia kubwa, tunaamini kwamba mpaka *division* IV ni ufaulu!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tusijidanganye, tunajipa picha kwamba watu wetu wanafaulu, kumbe tunakwenda kupeleka katika soko la ajira watu ambao hawako *competent*. Turudishe ufaulu *division one* mpaka *three,* ndiyo iwe *maximum* ya ufaulu na watu watajitahidi, watu watapambana, na Walimu watapambana kuhakikisha kwamba vijana wetu wanafaulu katika madaraja hayo.

Mheshimiwa Nabu Spika, tunajiridhisha tu kwamba ufaulu mwaka huu asilimia 69 kumbe kuna *division four* kule ndani, *division four* ni ufaulu? Haiwezekani tunataka tutoe Taifa la watu ambao wanajiweza. Taifa la watu ambao wako *competent,* tukitoka hapa tunashindanishwa na watu wa Mataifa mengine, tuweze ku-*survive*. Naomba sana hilo tulizingatie na kama inawezekana , tuanze kulibadilisha sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu nataka kuliongelea kidogo ni maji. Katika Jimbo langu la Kondoa kuna upungufu mkubwa sana na tatizo kubwa sana la maji Mjini pamoja na Vijijini. Pamoja na upungufu wa maji huu

na miradi inayokwenda michache, bado usimamiaji wa miradi ambayo ilikwenda kule mwanzo siyo mzuri kiasi kwamba miradi inakufa, visima vinashindwa kuendeshwa vizuri, wale watu hawapati elimu ya kutosha, Kamati za Maji hazijielewi, matokeo yake hata ile miradi michache iliyokwenda inakufa na tatizo linazidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba Waziri wa TAMISEMI suala hili tuliangalie, tuhakikishe maelekezo mazuri yanakwenda kwenye Halmashauri zetu, watu wasimamiwe wapate maelekezo mazuri, Kamati ziundwe, ziwe zinakuwa *monitored*, matokeo yake miradi iweze ku-*survive*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua bajeti yenyewe ni ndogo, hiyo miradi michache itakayokwenda kule lazima tuilee na iwe endelevu, bila usimamizi mzuri, tunawaelewa watu wetu vijijini, itakuwa changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimependa nizungumze hayo matatu tu katika hotuba hizi mbili. Nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Grace Kiwelu ajiandae, atafuatiwa na Mheshimiwa Savelina Mwijage.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kidogo katika hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze na Mfuko wa Barabara. Halmashauri zetu zinapokea fedha kidogo kwa ajili ya matengenezo ya barabara, kwa sababu fedha hizo ni kidogo, hawawezi kutengeneza barabara ambazo zina viwango kama zile zinazotengenezwa na *TANROAD*. Uwiano wa utoaji wa pesa za Mfuko wa Barabara kwa kila shilingi laki moja inayotoka kwa ajili ya Mfuko wa Barabara, Halmashauri inapewa sh. 30,000 *which is* 30 *percent,* kwa hiyo unaweza kuona Halmashauri wakipewa fedha, ni zile fedha ambazo zinaweza kufanya *grading* peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawawezi kutengeneza mitaro, hawawezi kuweka karavati, kwa hiyo mwaka hadi mwaka tutabaki kulaumu hizo Halmashauri. Serikali imekuwa ngumu kubadili sheria hii ili kusudi Halmashauri ziweze kupata fedha angalau hata asilimia 40 waweze kutengeneza barabara ambazo zinawiana, kwa kuangalia jinsi walivyotueleza ukisoma katika hotuba ya Waziri, anasema kuna zaidi ya barabara mtandao wa kilomita laki moja na kitu na nafikiri inawezekana ni zaidi ya hizo, maana yake sina uhakika wamefanya lini *research*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya kuongeza maeneo mapya ya utawala, hizi barabara za Halmashauri zina mitandao mikubwa ambayo kwa

kweli Serikali inapaswa ifikirie namna ya kuwapa Halmashauri fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napitia hili jedwali ambalo tumepewa na Waziri, nitoe mfano tu wa Mkoa wa Kagera peke yake. Mwaka 2014/2015, Mkoa wa Kagera ulikuwa umetengewa bilioni 9.1, lakini ulipewa bilioni 3.9, mwaka 2015/2016, Mkoa wetu tulitengewa bilioni 6.9 lakini tulipewa milioni 366, kwa hiyo ukichukua pesa zote hizo tulizopewa katika miaka hii miwili, tumepewa 4.2 bilioni. Unaweza ukaona ni jinsi gani, pesa zinavyokwenda katika Halmashauri na katika Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ifikirie namna ya kupeleka pesa ili tuweze kusaidia hizi Halmashauri, ziweze kutengeneza barabara kwa kuzingatia kwamba watu wote wako kule katika Halmashauri na huduma zinahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili naomba niongelee, ni kuhusu elimu. Ukurasa wa 24 wa kitabu cha Waziri, ameongelea kuhusu mambo ya elimu, mipango ni mizuri, lakini naomba nijielekeze katika hizi shule maalum ambazo zinafundisha watoto wenye matatizo, walemavu wa ngozi, walemavu wa viungo, pamoja na wale wasioona. Naomba nitoe mfano wa shule ambayo iko katika Mkoa wa Kagera inaitwa Ngeza Mseto.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 8 Machi ilikuwa ni Siku ya Wanawake Duniani, Chama chetu cha CHADEMA kilisherehekea sherehe hiyo kwa kwenda kutoa huduma katika sehemu mbalimbali ikiwemo shule hiyo. Tulichokikuta pale kuna watoto walemavu wa ngozi, kuna wale walemavu wa viungo, lakini pia kuna watoto wasioona. Tulichokikuta pale, wale wamama walioenda pale, walikuta vitanda vimejaa vinyesi, watoto hawaoni wale, wanalalia vinyesi, yaani mizinga ya vinyesi imejaa kwenye vitanda vyao, Walimu wapo, Matroni yupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *worse still*, nakumbuka mwaka 2000 nilikuwa Diwani, wakati ule Mheshimiwa Mizengo Pinda alikuwa Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI, alifika kwenye shule hii na kwa kweli aliomba Hazina, Hazina wakawa wanatoa fedha *extra money* milioni 60 kila mwaka, yaani milioni 15 kila baada ya kota moja. Je, naomba niulize TAMISEMI na nimuulize Waziri wa Elimu, pesa hizo bado zinakwenda na kama zinakwenda zinafanya nini?*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchungu mkubwa kabisa wale watoto wanavaa mpaka lisani zinatazama huko hawana mtu wa kuwaambia au kuwavisha, mabweni yao yote yamezungukwa na vinyesi, uchafu, wale watoto wanaishi kama wanyama. Ninyi mmetamka katika kitabu hiki kwamba

mtahakikisha kwamba watoto wenye mahitaji maalum watapewa elimu na wataangaliwa afya zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli shule ya Ngeza Mseto iko Manispaa ya Bukoba, tunaomba Waziri wa TAMISEMI na Naibu Waziri nendeni mkaiangalie hiyo shule, mhakikishe kwamba inapewa pesa. Siyo hiyo tu, hata vile vituo vingine ambavyo vina watoto ambao wana matatizo ya namna hiyo Serikali iweke mkono wake. Halmashauri peke yake ya Manispaa ya Bukoba haiwezi kabisa ku-*manage* shule hii, kwa sababu shule inabeba watoto wa Mkoa mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu taarifa ya Mdhibiti, mimi niko kwenye Kamati ya *LAAC* na hapa wameongelea kuhusu asilimia 20 ya fedha za Serikali ambazo zinazotoka kama ruzuku ambazo zinapaswa kwenda katika Vijiji, zingeweza kulipa mishahara ya Wenyeviti wa Vijiji au posho zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tulichogundua Kamati yetu imepitia Halmashauri 30, Halmashauri zote 30 zimeshindwa kupeleka hiyo asilimia 10, hizo Halmashauri zina jeuri! Zile pesa siyo mapato ya ndani ya Halmashauri, zile fedha zinatokana na ruzuku ya Serikali ambayo ni fidia ya vile vyanzo vya mapato, lakini Halmashauri hazipeleki hizo fedha na zikipeleka zinapeleka kwa asilimia kidogo. Mheshimiwa Simbachawene anajua na nafikiri Mheshimiwa Jafo anaelewa, waliona maoni yetu ni kwamba hizi fedha haziendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihakikishe na kusimamia pesa hizi ziwe zinakwenda na ninachotaka kuwaambia hata Vijiji vyenyewe havijui, havina taarifa kuhusu fedha hizo, inawezekana hata zikipelekwa zinaweza kulambwa na Wenyeviti wa Vijiji pale au na Watendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kusema juu ya utawala bora. Nisimalize bila kuongelea kuhusu haya mambo mnayosema hapa kuhusu *TBC* na nashangaa sana, wenzangu CCM msije mkafikiri kurudi ndani ya Bunge hili, mjitazame ninyi huko nyote kuna watu hawakurudi *almost* 60 *percent* kwani matangazo hayakuwepo? Kurudi au kutorudi haina maana kwamba wasiangalie matangazo yao *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii inaendeshwa kwa demokrasia ya uwakilishi, ndiyo maana kuna vyombo kama Bunge, Bunge siyo mali ya Serikali, Bunge ni mali ya watu, ni chombo cha watu na ukitazama dunia nzima huwa kunakuwa na mvutano mkubwa kati ya Serikali na Bunge. Serikali hailipendi Bunge, kwa sababu Wabunge mnaisema Serikali, mnaisahihisha, mnafichua, kwa hiyo itafanya kila mbinu kuhakikisha kwamba hili Bunge linadhoofika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi hii, viongozi wote nawaambia, Naibu Spika upo hapo na Spika, hebu igeni hayo Mabunge ya nyuma yalikuwa yanafanya kazi gani, igeni hata nyuma, mnakumbuka Wabunge mliokuwepo, ilikuwa ni kazi kubwa sana kuanzisha Kamati ya Bajeti ndani ya Bunge hili, tunamshukuru *Madam* Spika pamoja na kwamba tulikuwa tunamkoa makwenzi humu, lakini yule Mama alisimama imara kuhakikisha Kamati ya Bajeti inaanzishwa. Serikali ilikuwa haitaki Kamati ya Bajeti lakini Bunge lilisimama imara,na Spika alisimama imara na Naibu wake. Kwa hiyo na ninyi msikubali Serikali kutuyumbisha, tutashindwa kusimamia watu.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Watakuwa hawana *legacy*!

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, mtashindwa kuwa na *legacy* kwa sababu mkimaliza miaka yenu mitano au kumi watu watawakumbuka kwa sababu ipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana haya mambo ya watu kusikia taarifa ni namna ya kuwaelimisha Watanzania. Katika kitabu hiki, wametuambia kwamba kuna watoto zaidi ya laki mbili na sitini na kitu, hawakuweza kufanya mtihani wa darasa la saba, tunawa-*damp* huko ndani na inawezekana hawawezi kujiendeleza tena. Watu wanapaswa kupata elimu kupitia majarida, ndivyo wanavyoweza kujua namna Serikali yao inavyoendeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnawaambia watoe kodi, watajuaje maana ya kodi, watajuaje zinasimamiwaje hizo kodi, mnawarudisha Watanzania katika ujima. Hatuwezi nchi hii kwenda hivyo, mngefanya miaka ya 60, sasa hivi Watanzania ni waelewa, wanataka kusikiliza Bunge lao, wanataka kujifunza na tuwasaidie kujifunza, tusiwadumaze Watanzania kwa kuwarudisha katika kuvaa ngozi, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni hayo, lakini nakuomba tena ninyi ni wasomi… *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Grace Kiwelu

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala Bora ni pamoja na watu kupata habari na kujua wawakilishi wao waliowachagua wanawawakilisha vipi ndani ya Bunge, lakini Bunge letu leo limekuwa ni Bunge la kujifungia ndani, tumefunga milango, tumefunga madirisha, hatutaki wananchi ambao tuliwaomba kura kwa unyenyekevu mkubwa, wengine walipiga magoti, wengine walipiga

pushapu, ili mradi tupate kura, lakini leo hamtaki kuwapa nafasi wananchi wasikie mnachokisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana, Bunge letu liendelee na ule utaratibu wa zamani. Huko nje wananchi wanalalamika kwa sababu bajeti tunayoipitisha hapa ni kodi zao, lakini leo tunajifungia hatutaki wasikie, ni aibu!

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo kuhusu mwenge. Kama kuna kitu kinachonikera ni suala la kukimbiza mwenge mchana. Wabunge wa Upinzani tulishasema, kuhusu sherehe zinazoadhimishwa na Serikali, lakini mlitucheka, leo zipo baadhi zimesitishwa. Namwomba Mheshimiwa Rais kama alivyoacha kusherehekea hizo sherehe nyingine ambazo ni za muhimu kama Uhuru na Muungano, tuachane na biashara ya kukimbiza mwenge mchana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zinatengwa bajeti kwenye Halmashauri zetu, leo kila Mbunge analalamika mafuriko kwenye maeneo yake watu wanakimbiza mwenge, watu wetu wanakufa hawana maji safi na salama, hawana dawa, madaraja yamebebwa na maji, hakuna barabara, tunakimbizana na mwenge, hii ni aibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana kama ni kazi ya mwenge naamini imetosha, maana yake siamini kama hata hao mafisadi, hauna tija kwa sasa pamoja na kumulikwa kila mwaka, lakini ufisadi bado upo pale pale. Naomba sana hizi fedha zinazotengwa kwa ajili ya kukimbiza mwenge tuzipeleke kwenye shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la upotevu wa pesa katika Halmashauri zetu. Katika Manispaa ya Moshi Mjini kulitokea ubadhirifu wa shilingi milioni 90 kutoka kwenye *Basket Fund* na suala hili TAKUKURU walililiingilia, wakachunguza na wakagundua baadhi ya watumishi waliziiba fedha hizi na wakawashauri wale watumishi warudishe fedha hizi na mpaka sasa inasemekana zimesharudishwa shilingi milioni 70.

Swali langu ni kwa nini TAKUKURU pamoja na nia njema waliyoonyesha na kazi nzuri waliyofanya, maana wamewaomba warudishe fedha na zimerudi, ni kwa nini sasa TAKUKURU hailipeleki suala hili mahakamani ili wale wote walioshiriki kwenye suala hili wakachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu zetu za nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiliacha hivi TAKUKURU wakiendelea kumalizana ofisini fedha za walipa kodi zitaendelea kupotea na tukizingatia zaidi ya 70% ya fedha tunazopitisha hapa zinakwenda kwenye Halmashauri. Fedha hizo zingekuwa zinafanya kazi inayotakiwa leo wananchi wetu vilio walivyonavyo vingepungua. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa

Simbachawene, Waziri wa TAMISEMI, suala hili mlifuatilie na wale watumishi mhakikishe wanafikishwa mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine niungane na Mheshimiwa Waziri (TAMISEMI) kuhusu uongezaji wa mapato katika Halmashauri zetu. Halmashauri zetu hasa mapato ya ndani yamekuwa ni kidogo sana na hii inatokana na wale wazabuni tunaowapa *tender* hawawi wa kweli, wanaziibia Halmashauri zetu. Wengi wamekuwa wakitumia vitabu viwili na kuleta yale mapato madogo katika Halmashauri zetu na kusababishia Halmashauri zetu kushindwa kujiendesha na kukosa yale mapato ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitolee mfano Halmashauri yetu ya Siha, yupo mzabuni mmoja, niiseme hii kwa sababu watumishi wamekuwa wakianzisha kampuni zao na wamekuwa wakijipa *tender* wenyewe na suala hili linasababisha sana Halmashauri zetu kushindwa kuendelea. Halmashauri yetu ya Siha yupo mzabuni mmoja amepewa zaidi ya zabuni tano na mpaka sasa anadaiwa zaidi ya shilingi milioni 56 hajaweza kuzileta katika Halmashauri yetu. Nimeona kwenye magazeti juzi wanasema Halmashauri ya Siha tusipoweza kukusanya itafutwa, lakini wanaoturudisha nyuma ni wazabuni kama hawa. Niombe Mheshimiwa Waziri tufuatilie na wale watumishi wote watakaogundulika kwamba wana kampuni ambazo wamejipa bila kufuata taratibu waweze kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la elimu. Mzungumzaji aliyemaliza kuongea alisema siku ya wanawake duniani tulitembelea maeneo mbalimbali kwenda kusherehekea sikukuu ya wanawake duniani. Mimi nilibahatika kwenda katika shule ya watoto wenye ulemavu iliyopo Njia Panda, Jimbo la Vunjo. Shule ile ina wanafunzi 69 wasiosikia, wana matatizo makubwa sana, ina walimu 11 lakini ina watumishi watatu, matroni na mlinzi hawa bado hawajaajiriwa. Ukizingatia kauli ya elimu bure, awali wazazi walikuwa wanachangia kwa kuwaandikia lakini leo mwalimu mkuu wa shule ile hawezi kuandika kwa sababu anaogopa kufukuzwa kazi. Matroni na mlinzi hawajalipwa mshahara huu ni mwezi wa nne. Hata kutoa huduma ndogo ndogo kama matengenezo ya vitasa, kununua vitabu, toka Januari mpaka sasa wamepata *capitation* shilingi 25,000 tu, hii ni aibu. Mheshimiwa Waziri umeonesha hapa shule tulizonazo, nilitegemea ungetuonesha tuna shule ngapi za watoto wenye ulemavu kwa sababu tunahitaji watoto wetu wapate elimu na najua shule za watoto wenye ulemavu zina mahitaji zaidi ya hawa watoto wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shule ile inahitaji mambo mengi mfano na pia ukarabati haina uzio. Pia walikuwa na kilio kwamba wanahitaji kupata shule ya sekondari kwa sababu watoto wanaotoka pale wakifaulu, wakipelekwa kwenye shule hizi nyingine kuendelea na masomo hawapati walimu wenye

lugha ya alama. Kwa hiyo, uelewa wao unakuwa ni mdogo wakifika *form two* wanarudi nyumbani. Wanasema wanalo eneo kubwa pale, wanaomba sana ile shule iendelezwe mpaka sekondari ili watoto wetu pamoja na ulemavu lakini akili wanazo, wanao uwezo wa kusoma, tukiwapa mahitaji yao na tukatekeleza mahitaji yao, naamini watakwenda kuwa viongozi wazuri katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine nizungumzie suala la posho za Madiwani, Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji. Leo tuko Bungeni tunayo maafa kwenye maeneo tunayotoka lakini wanaowajibika ni hawa Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa. Tunaiomba sana Serikali hii ya Hapa Kazi Tu basi watazameni hawa, wanafanya kazi ngumu. Likitokea janga wa kwanza kugongewa ni Diwani. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Savelina Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete halafu Mheshimiwa Hussein Bashe ajiandae.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu na napenda kumpongeza Katibu wangu Mkuu Maalim Seif kwa kuwa na msimamo wa kukataa kuburuzwa kwenye uchaguzi wa marudio wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi napenda nichangie kwenye bajeti hii. Mkoa wa Kagera naona una tatizo kwenye Serikali kwa sababu kila wakipanga bajeti unaangalia huo Mkoa unatupwa pembeni. Bajeti yake ni ndogo sana na matumizi yao ni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitaanzia kwenye usafiri wa majini, Ziwa Victoria, kila Rais anayeingia kwenye madaraka anaahidi meli mpya, meli tatu mpya, meli mbili mpya mpaka anamaliza uongozi wake anaingia Rais mwingine. Tumekuwa watu wa kujaribiwa kila miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliahidiwa meli na meli tuliyonayo ya Victoria wamepanga bajeti ya kufanya ukarabati. Meli hiyo ni ya miaka, imeshazeeka, hata wakifanya ukarabati siku mbili, tatu lazima yatokee maafa. Kuliko kukarabati, hizo pesa kwa nini wasikusanye wakawaletea meli mpya ya kuweza kuwasaidia ili isiwe mitego ya kuwa watu wanadumbukia kwenye maji mara kwa mara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye kilimo. Mkoa wa Kagera kilimo chetu hasa ni ndizi na kahawa na ndizi ni zao la chakula na la uchumi, sasa hivi zao hili limekuwa na matatizo. Halmashauri nyingi ziliandika barua na kuomba Serikali kuwasaidia kuwaletea wataalam wa kutibu ugonjwa ambao umeleta madhara, kwa kweli miaka miwili inayokuja mbele watu watakufa na njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kahawa ni zao kuu ambalo sisi toka tumezaliwa tumekuta ni zao kuu la kiuchumi. Ukiangalia Uganda hilo zao lina bei kubwa lakini Mkoa wa Kagera zao hili limerudi chini. Inafika mahali watu wanakata miti ya kahawa na kuifanya kuni kwa sababu hawana faida nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye barabara. Fedha ya barabara inayotengwa ni ndogo kweli lakini ukiangalia ni barabara ambazo zina fursa ya kuingiza uchumi katika Mkoa wetu, imepakana na Uganda, Rwanda na Burundi. Ukiangalia barabara ya kutoka Kayanga kwenda mpaka Kyerwa, Karagwe ni barabara ya vumbi miaka nenda miaka rudi, hawakumbuki hata kuwatengenezea barabara lakini tukija humu ndani tunauingiza ushabiki wa vyama bila kuwafikiria watu wetu wanapata shida. Ukiangalia barabara ya kutoka Kanazi kwenda mpaka Katoro, kuzunguka kwenda mpaka Kyaka, ni barabara nzuri ambayo ina fursa nzuri ya kuzalisha uchumi katika mkoa wetu lakini mpaka sasa hivi Serikali haijagusa hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Bukoba Vijijini wana tatizo la kivuko na nimepiga kelele hapa kuanzia mwaka 2006. Mara kwa mara kivuko kilichopo kinakwama katikati ya maji na watu wanapata shida. Niliiomba Serikali angalau wawaletee kivuko hata kama kimetumika lakini kiwe na uimara siyo mara kwa mara kuwa kinatengenezwa, watu wanapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye maji. Mkoa wa Kagera umezungukwa na mito mingi lakini akina mama wanapata shida ya maji. Unashangaa ukienda sehemu za Katoro, Karagwe, wanakunywa maji ambayo rangi yake utafikiri wameweka maziwa, lakini tukija hapa tunashabikia kuzomeana hatukumbuki watu wetu tuliowaacha nyuma wana matatizo makubwa. Akina mama wanapata shida, wanatembea zaidi ya kilometa 20, zaidi ya kilometa 50 wanatafuta maji. Ukienda pale mgeni wakikuletea maji utafikiri wamekuwekea maziwa kumbe ni maji ya kunywa lakini tukija hapa kazi ni kelele ya upinzani-upinzani, tunasema kitu ambacho kinatusaidia na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye usafiri. Sisi Mkoa wa Kagera usafiri ni wa matatizo, mabasi yakishaharibika huku ndiyo wanatuletea kule kama nilivyosema kwenye meli. Sasa ni lini Serikali itaona umuhimu angalau wa kututengenezea bandari mbili, Bandari ya Kemondo na Bukoba Mjini kwa

sababu bandari iliyopo ya Bukoba Mjini ilikuwa inaingiza meli kutoka Bukoba inabeba mizigo inapeleka Uganda, inatoka Uganda inapeleka Mwanza inakwenda Musoma, leo hii hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inafanya mpaka mkoa wetu ushuke kiuchumi, Serikali ituangalie. Mara kwa mara watu tunakuja hapa tunapiga kelele, mimi nawaeleza Wabunge wa Mkoa wa Kagera, tukae pamoja tuangalie fursa za kuweza kutusaidia katika Mkoa wetu, vyama tuweke pembeni tuangalie fursa za mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri kuna wizi ambao hata pesa hizi zilizopangwa shilingi milioni 50 hazitafanya chochote bila kuwa na mikakati. Mfanyakazi wa Halmashauri anaiba pesa wanambadilisha hapo hapo wanamweka Wizara nyingine lakini anapokwenda kule anaendelea kufanya mambo kama hayo, kwa nini asifukuzwe? Mtu anakaa Halmashauri mpaka miaka 10 bado yuko Halmashauri. Anafanya kazi kwa mazoea, anafanya kazi kwa kujua hakuna mtu wa kufanya kitu chochote kwa sababu analindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Muleba kuna mkandarasi ambaye alisimamishwa kazi na Mheshimiwa Mwanri, aliyekuwa Naibu Waziri wa TAMISEMI lakini mpaka sasa hivi huyo huyo ndiyo amepewa kazi kwa sababu ana ushirika na mtu wa Chama cha Mapinduzi, anamkingia kifua aendelee kupewa kazi. Hatutakwenda kwa sababu pesa zinatengwa hapa kwenda kufanya kazi lakini tunaendelea kuweka mtu ambaye ana makosa na alishasimamishwa asiendelee kufanya kazi. Tunaomba haya tunayoyaongea na kushauri sisi wapinzani muwe mnayaangalia, siyo yote yanakuwa mabaya. Tunaishauri Serikali ili ikafanye kazi vizuri siyo tusimame hapa tuanze kuimba ngonjera ya vyama, kitu kilichotuleta hapa ni kuwatetea wananchi ambao ni maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu hawana uwezo wa kununua dawa. Anakwenda hospitali anaandikiwa dawa anaambiwa akanunue, pesa atatoa wapi? Kuna wazee ambao hawana uwezo, wanasema wazee watatibiwa bure, mimi sijawahi kuona wazee wanaotibiwa bure, anapanga foleni kama mimi, mzee anafia pale pale barazani hata kidonge hajapata. Naiomba Serikali kama wazee wanatibiwa bure wapewe bima za afya na watengewe dirisha lao ili wawe wanapata matibabu stahiki kwa sababu hawana pesa ya kununua dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwa wagonjwa walioathirika na UKIMWI. Tunaomba Serikali, kwa sababu inaonesha inawapa hata chakula, ni masikitiko makubwa, nilikuwa nashauri hata kwenye Kamati yangu, mtu anakwenda pale ameathirika badala ya kumweleza mapema kabla

hajapimwa, anapimwa akirudi wanaanza kumwambia ukijua umeathirika utafanya nini, ukijua unaumwa utafanya nini? Mtu anaweza akafia palepale hajafika hata kuchukua dawa wala hajajua kama ameathirika ama hakuathirika. Naomba wale ambao wanawa-*treat* wale watu wawaeleze mapema kabla hawajaanza kuwaeleza kama wameathirika au hawajaathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kamati tuliomba kwamba pale wanapopewa dawa wawe wanapewa na watu wengine kwa sababu ukiwaweka pale kwenye dirisha peke yao mtu mwingine anaogopa kuchukua dawa abaona aibu! Kwa nini umewatenga na hiyo ni kuwanyanyapaa. Naomba watibiwe na sisi lakini dawa zao zinakuwa zimeandikwa zinajulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye elimu. Watoto wa kike wanapata shida na elimu. Nashauri mtoto wa kike akipata mimba aliyempa mimba na yule aliyempa mimba apewe adhabu. Siyo msichana peke yake anapata mimba anarudi nyumbani anakaa chini kijana anaendelea na masomo, huo siyo unyanyapaa? Huyo kijana na yeye apewe adhabu ili kama wanapewa adhabu wapewe adhabu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo lakini haya niliyoyaongea hapa naomba ushauri wangu ufanyiwe kazi na Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Bashe na Mheshimiwa John Peter Kadutu ajiandae.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo pia nianze kwa kuwapa pole wananchi wangu wa Jimbo la Chalinze na Halmashauri ya Chalinze kwa mafuriko makubwa yaliyowapata. Wajue tu kwamba Mbunge wao niko nao pamoja sana. Nitakwenda *weekend* hii ili kushirikiana nao pale panapoonekana Mbunge natakiwa nifanye kazi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ni nzuri na imejikita katika mambo mazuri. Mimi sina wasiwasi sana na Waheshimiwa hawa wawili katika utekelezaji wa majukumu yao. Hata hivyo, yapo maeneo ambayo yanahitaji tuzungumze ili kuweka nguvu lakini pia kuendelea kukumbushana katika mambo ya msingi ambayo nafikiri kwamba wangeweza kuyasimamia basi mambo ya Chalinze na Tanzania yangekwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na jambo la usimamizi wa maendeleo ya miji na halmashauri zetu. Pamoja na mambo mazuri ambayo yameainishwa lakini jambo la kupanga miji ili iweze kufanana na sura ambayo kila mtu angeitaraji iwepo ni jambo la msingi sana. Kwa mfano, nimeona katika maelezo ya mipango ya kibajeti kwamba ziko Halmashauri ambazo zimeshapanga maendeleo yao na Serikali imepanga kupeleka fedha. Nataka nikumbushe kwamba katika bajeti iliyopita Halmashauri ya Chalinze ilikuwa imetengewa fedha kwa ajili ya kupanga mji wake. Kwa bahati mbaya zile fedha zilipokuja zilitumika katika kipande kidogo sana cha kufanya tathmini ya maeneo ya watu lakini pia uanzishaji wa uchoraji wa ramani ya Mji wa Chalinze. Mpaka leo fedha zile zimeshindwa kukamilika hivyo Mji wa Chalinze bado unahitaji fedha ili tuweze kuupanga vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo pia nataka niikumbushe Ofisi ya Mheshimiwa Waziri, TAMISEMI kwamba Halmashauri ya Chalinze ni mpya, imeanza mwaka jana. Tunawashukuru kwa mambo mazuri waliyokwishatufanyia na ofisi nzuri tulinayo lakini ipo ahadi ya Serikali ya kujenga Ofisi za Halmashauri ya Chalinze katika Makao Makuu ya Halmashauri hiyo ambayo ni Mji wa Chalinze. Mpaka leo navyozungumza fedha zile zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya matumizi hayo ili tuweze kujenga makao makuu yetu bado hazijapatikana. Kwa hiyo, ningemuomba Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa kufanya majumuisho au kutoa majibu au tafsiri ya mambo ambayo wameeleza Wabunge hawa basi hili jambo la Chalinze nalo liwe ni moja ya jambo ambalo akiliweka vizuri tutamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwamba upo Mfuko wa Barabara Vijiji. Chalinze kwa sura yake ilivyo ina Mamlaka ya Mji ambayo ni Chalinze na Ubena lakini pia mahitaji yetu makubwa sana au eneo kubwa sana la Halmashauri ya Chalinze bado ni vijiji. Kwa hiyo, napoona katika mpango huu ambao umepangwa kutekelezeka katika bajeti ya mwaka huu zimewekwa shilingi milioni tisa tu kwa ajili ya Mfuko wa Barabara, Wilaya ya Chalinze, binafsi naona fedha hizi ni ndogo sana haziwezi kufanya ile kazi ambayo Serikali hii inataka kuisimamia. Kubwa zaidi lazima wajue kwamba Mbunge mimi ni Mbunge nayependa kutembea, napenda sana kwenda vijijini na huko ili paweze kufikika barabara lazima zikae vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia limezungumzwa jambo la afya, niwashukuru sana kwa mipango yao mizuri ambayo wamekwishaionesha lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa fungu kubwa sana la afya maana tunajua kwamba pasipokuwa na afya mambo hayaendi. Pamoja na hayo liko tatizo kubwa limeibuka Chalinze nafikiri la wiki hii, jambo hili nafikiri nilitolee taarifa kwamba kumetokea tatizo kubwa sana la upungufu wa chanjo ya surua. Wananchi wangu wa Jimbo la Chalinze wamekwenda kwenye vituo vya afya, wamekwenda kwenye maeneo mbalimbali kwenda kutafuta chanjo hizo lakini

walipokwenda hapakuwepo na chanjo hiyo. Kwa hiyo, ni vyema Wizara kama Wizara mama TAMISEMI au Wizara ya Afya ikalitolea taarifa jambo hili ili wananchi wa Chalinze wajue kwamba Serikali yao inaendelea kujali na mambo ya afya ni moja ya vipaumbele vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nishukuru sana Serikali ya CCM kwa kutupatia Hospitali ya Wilaya ya Chalinze. Hospitali hii zamani ilikuwa ni kituo cha afya pale Msoga na sasa ndiyo Hospitali yetu ya Wilaya. Kila panapokuja mazuri basi makubwa nayo hujitokeza. Hospitali ile inahitaji mabadiliko makubwa katika miundombinu ile ya kituo kile cha afya. Kwa hiyo, fedha kwa ajili ya upanuzi wa hospitali yetu ya Msoga nayo ni moja ya kitu cha msingi sana kutiliwa maanani. Ninaposimama hapa ningeomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kuzungumza basi atuambie katika lile fungu aliloweka katika afya, je, fedha hizo zilizowekwa ni pamoja na upanuzi wa hospitali hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipekee kabisa nimshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na dada yangu Mheshimiwa Ummy kwa kazi nzuri waliyoifanya pale Tumbi maana ilikuwa ni kilio kikubwa kwa watu wanaosafiri na barabara ile. Likitokea tatizo hata mtu kwa mfano akifariki *mortuary* hakuna Tumbi, akina mama wakipata matatizo ni shida na ndiyo hospitali tulikuwa tuinategemea kwa ajili ya rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii napozungumza hapa kazi nzuri imekwishafanyika, *mortuary* ile iko vizuri na wodi nzuri imekwishakamilika. Kwa hiyo, ni mambo mazuri yamefanyika na tunaendelea kuwashukuru sana viongozi wetu hawa tuliowachagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hilo katika hotuba ya Wizara imezungumzia juu ya mradi wa maji vijijini na fedha ambazo zimekwishatengwa. Napenda tu nitoe taarifa kwamba mradi wa maji wa Chalinze umekuwa ni mradi ambao kila siku hauishi kuharibika katika miundombinu yake. Pia mahitaji ya kufikisha maji katika vijiji vyetu nalo limekuwa ni jambo moja la msingi ambalo siku zote mimi kama Mbunge wa Chama cha Mapinduzi nimekuwa nalisimamia. Naomba sana tunapotenga fedha kwa ajili ya miradi ya maji vijijini basi Mheshimiwa Waziri ni vyema ukaliangalia hili nalo ili tuweze kuona watu wa Chalinze wanaendelea kupata mambo mazuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona katika randama yenu ya bajeti kwamba mmepanga kutumia shilingi milioni 10 kwa ajili ya miradi ya maji ya vijiji vya Chalinze, fedha hizi ni ndogo sana. Chalinze ni moja ya Majimbo makubwa sana katika Tanzania yetu na vijiji vingi sana vinahitaji maji hayo. Kwa hiyo, unapotenga fedha shilingi milioni 10 kwangu mimi hizi naziona ni fedha ambazo zitatosha kwa ajili ya uendeshaji tu na siyo mradi mzima tunaoutarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo Serikali imeendelea kusaidia kuweka fedha katika miradi kama ya *TASAF* na MKURABITA, ni jambo la msingi sana. Hata hivyo, niendelee kuwasisitiza kuendelea kukagua na kutathmini kaya zenye uhitaji wa fedha za *TASAF* lakini pia kupeleka fedha nyingi kwenye mradi wa MKURABITA ili vijiji vyangu sasa viweze kupimwa na hati zile za kimila ziweze kupatikana ili kuondoa migogoro isiyo ya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maendeleo ya jamii, wananchi wa Chalinze wameendelea kulilia soko lao. Katika hotuba ya bajeti iliyopita ya Wizara ya Kazi ilizungumzwa hapa kwamba patajengwa soko la kisasa ndani ya Chalinze. Cha ajabu zaidi mpaka leo hii wananchi wangu wanasubiri hawaelewi nini hatima yake. Nakumbuka ilipangwa mipango mizuri hapa pamoja na kushirikiana na mashirika mbalimbali ya kiserikali kwamba wangeliangalia jambo hili lakini mpaka leo hii bado tunaendelea kusisitiza mahitaji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Chalinze wanapounguliwa nyumba zao gari la kuzima moto halipo. Ile ni Mamlaka ya Mji na imani yangu ni kwamba mkiliangalia hili kwa vizuri basi tunaweza kuepusha vifo visivyo vya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono asilimia mia moja hoja za Ofisi zote mbili, lakini msisitizo mkubwa ukiwepo kwamba watupe jicho la karibu sana watu wa Chalinze kwa sababu Halmashauri ni mpya na mahitaji bado yako pale pale. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hussein Bashe, Mheshimiwa John Peter Kadutu ajiandae.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia. Nianze kwa kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutufanya tuweze kuwa salama na tuweze kushiriki kikao hiki cha siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kuwapongeza Mawaziri na nawapongeza kwa jambo moja la msingi. Zamani kabla sijaingia Bungeni nilikuwa nasikia kwamba kumfikia Waziri ni kazi ngumu kweli, lakini Mawaziri wa Serikali ya Awamu ya Tano naona ni Mawaziri *reachable*, ni rahisi kuwafikia. Binafsi niwashukuru kwa dhati kabisa Waziri Mheshimiwa Simbachawene na Naibu wake Mheshimiwa Jafo kwa sababu yanayohusu Halmashauri yangu ya Mji wa Nzega wamekuwa wakitoa ushirikiano hata yale ambayo hajakamilika lakini angalau unakuwa una moyo kwamba kesho litakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na jambo la kwanza. Halmashauri ya Mji wa Nzega ni mpya, lakini kwa muda mrefu kwa lugha ambayo nimeisikia

Serikalini inalelewa na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega. Kwa maana kwamba bajeti *ceiling* zake zinakuwa zikipitia Halmashauri ya Wilaya ya Nzega. Mheshimiwa Waziri anafahamu matatizo yanayoikabili Halmashauri ya Mji wa Nzega, fedha za *OC* mnazopeleka Halmashauri ya Mji wa Nzega zinazopitia *Nzega DC* hazifiki katika Halmashauri ya Mji wa Nzega. Inakuwa ni *unfair* kwa watendaji walioko pale, Serikali Kuu ina *disburse* fedha kwenda kwenye Halmashauri ya Mji wa Nzega kupita Halmashauri ya *Nzega DC* kwa sababu tu *ceiling* na *vote* ya Halmashauri ya Mji wa Nzega ilikuwa chini ya Halmshauri ya Wilaya ya Nzega. Mpaka leo fedha mlizotuma kwenda Halmashauri ya Mji wa Nzega *56 million shillings* ambazo ni za *OC* zimetumika katika Halmashauri ya Wilaya na Halmashauri ya Mji haijapata zile fedha, ni tatizo kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Halmashauri ya Mji wa Nzega ipewe *vote* yake, ijitegemee, ina wafanya kazi wake, ina vyanzo vyake vya mapato, ina kila kitu, *for how long* Halmashauri ya Mji huu itakuwa chini ya Halmshauri ya Wilaya ya Nzega, ni mateso. Leo hii fedha za Mfuko wa Jimbo la Nzega Mjini tunashindwa kuzipata na hili siyo suala la Wabunge ni la watendaji walioko pale hawako *flexible* kutumia taratibu zilizowekwa ili fedha zile ziwe *disbursed* kwenda kwenye Halmshauri ya Mji wa Nzega, hili ni ni tatizo. Nakuomba Mheshimiwa Simbachawene, Halmashauri ya Mji wa Nzega muiondoe kwenye kwapa la Halmashauri ya Wilaya ya Nzega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo vyanzo vya mapato vya Halmashauri ya Mji wa Nzega vinakusanywa na Halmashauri ya Wilaya kwa hoja kwamba fedha hizi zitahamishiwa katika Halmashauri ya Mji lakini hawahamishi. Kwa hiyo, ningeomba hili jambo litatuliwe kabisa katika Mji wa Nzega. Hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nimeona hapa katika jedwali lililoambatanishwa, Halmashauri ya Mji wa Nzega imetegewa shilingi milioni saba kwa ajili ya kilimo, Halmashauri ya Mji wa Nzega ina kata 10, kata nane zote ni za wakulima na ndiyo zinalisha ule mji lakini tume-*allocate only seven million shillings.* Bajeti iliyokuwa *proposed* na Halmashauri ya Mji ambayo tuliomba *for development* ni *176 million shillings* lakini tunapata shilingi milioni saba. Kwa hiyo, naomba mnapo-*allocate* fedha hizi mnazoweka kwenye majiji makubwa kama Mwanza, Arusha na kwingine kwamba ni ya kilimo hawalimi, hizi fedha pelekeni kwenye maeneo yenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano katika Mji wa Nzega tuna eneo kubwa la kilimo katika Kata ya Mwanzori, kumekuwepo na *irrigation scheme* toka miaka ya 1970. Kwa sababu tu hakuna *allocation* ya *resources*, sasa hivi ile *irrigation scheme* katika Kijiji cha Idudumo inakufa. Namuomba Mheshimiwa Waziri waliangalie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiitazama *allocation* ya *funds* kwenye kilimo kwa Wilaya zote za Mkoa wa Tabora imetengwa *198 million shillings*. Mkoa wa Tabora unalima tumbaku na kwa mwaka jana tumbaku ime-*contribute over three hundred million US dollars* kwenye pato la Taifa, tunawapelekea shilingi milioni 180. Ukiangalia fedha zilizokuwa *allocated* kwenye Wizara ya Kilimo na zenyewe ni masikitiko. Najua kasungura kadogo wekeni *priority* sehemu ya kuzi-*allocate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alipofika katika Mji wa Nzega wakati anaomba kura tarehe 14 Oktoba, 2015 aliahidi mambo makubwa mawili. Jambo la kwanza katika Mji wa Nzega tuna tatizo sugu la maji, tukamuomba Mheshimiwa Rais kwamba kutatua tatizo la maji katika Mji wa Nzega wakati tunasubiri mradi wa maji wa Ziwa Victoria, kwanza nimwambie Mheshimiwa Waziri wa Maji akija hapa atuambie ni lini mradi wa Ziwa Victoria utaanza kwa ajili ya Mkoa wa Tabora. Wasiposema *specifically* ni tarehe ngapi mkandarasi anaingia pale mimi nitakuwa mmoja kati ya Mbunge wa Chama cha Mapinduzi ambaye hataunga mkono bajeti ya Serikali kwa sababu mradi huu umejadiliwa mwaka 2013, 2014 na 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, wakati anajadili suala la maji alitupa *shorten solution*, katika Mji wa Nzega tunahitaji pampu na matenki matano, ukitazama *allocation* ya maji iliyowekwa ni shilingi milioni nane. Nikiangalia fedha zilizokuwa *allocated* Wizara ya Maji hazitatui kabisa tatizo la maji la muda mfupi Nzega. Leo tunatarajia maji kutoka Bwawa la Kilimi, chujio liko Bwawa la Uchama, kwa hiyo vijiji vyote vinavyotoka Kilimi mpaka Uchama ambako tunaenda kusafishia maji hawapati maji. Naiomba Serikali kwa heshima kabisa tunapo-*allocate* hivi vitu kidogo kidogo hatutatui tatizo. Ni lazima tulitatue tatizo kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba ahadi ya Rais ya kufunga pampu ya maji katika Bwawa la Kilimi na kujenga matenki matano katika Mji wa Nzega ili kutatua tatizo la maji wakati tunasubiri utekelezaji wa mradi wa maji wa Ziwa Victoria itekelezwe na tuone *commitment* ya Serikali katika jambo hili. *For good news,* nimwambie Waziri wa Maji yupo hapa kwamba kwa kuwa Rais alisema mkandarasi atakaa pale Nzega kwa sababu ni njia panda kupeleka maji Singida na Tabora, sisi Halmashauri ya Mji wa Nzega tumetenga eneo ambalo Serikali haitataka fidia yoyote hata shilingi kwa ajili ya kuja kumkaribisha huyo mkandarasi ili aweze kukaa pale na kufanya huu mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimsikia Mbunge mwenzangu mmoja hapa anaongea simkumbuki nadhani ni Mheshimiwa Sannda, namuomba Mheshimiwa Naibu Waziri Jafo na Waziri Mheshimiwa Simbachawene, leo tunaenda kuwaambia wananchi wachangie madawati, wachangie ujenzi wa

maabara, Nzega zimeliwa 2.2 *billion shillings* zilizotolewa na Mgodi wa *Resolute* ambazo zilikuwa *allocated* kwa ajili ya ujenzi wa maabara.

Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla aliandamana, alipigwa mabomu, aliwekwa jela ndiyo akapata hako kasungura ka shilingi bilioni 2.2 kalivyoenda Halmashauri waliopiga *deal* mwingine mme-*promote* ndiyo kawa Injinia wa Manispaa ya Kagera. Huyu mtu aliharibu Ilala, akahamishiwa Nzega *and Nzega is a dumping place* kwenye *local government,* zikaja 2.2 *billion shillings* akapiga yeye na wenzake maabara zilizokuwa *allocated 68 million shillings* hazijafika hata kwenye lenta, akahamishiwa kuwa Injinia wa Manispaa ya Kagera, yupo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Nzega, tena Mheshimiwa Waziri Mkuu nisikilize, aliyekuwa Mweka Hazina wa Halmashauri ya Sumbawanga ana kesi ya uhujumu uchumi akapelekwa Magu, akapata kesi ya uhujumu uchumi, leo kahamishiwa Nzega. Leo tumemkamata yeye na *network* yake wakiiba fedha za *parking*, wenzake wamewekwa ndani yeye anazunguka pale, *this is unfair*. Halafu tunaenda kwa wananchi kuwaambia watuchangie fedha za maabara, mimi nimewaambia wananchi wangu wa Mji wa Nzega hakuna kuchanga fedha ya maabara mpaka wezi wapelekwe mahakamani tutafunika maabara zilizobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kwa masikitiko kabisa, dhamira ya Rais kumpatia kila mtoto wa nchi hii elimu bora ni dhamira njema, tuione kwenye *commitment* ya Serikali katika *allocational of resources,* tumefanya *mass expansion* ya elimu. Hata ukisoma Mpango wa Miaka Mitano, Waziri Mpango anakiri kwenye *document* yake kwamba *quality* ya elimu yetu ni tatizo. Niiombe Wizara ya TAMISEMI, kwa sababu kwa sasa hivi dhamana ya ku-*expand infrastructure* iko mikononi mwenu, jamani tengeni fedha ya kujenga *infrastructure* ya elimu, tukiuacha huu mzigo kwa wananchi peke yao hawawezi, tuiombe *central government*. Nishukuru nimepokea madawati 250 nadhani ni chenji ya rada, nashukuru kabisa na nimeyapokea yako pale. Nitumie fursa hii kushukuru *institution* ambazo zimetusaidia katika Mji wa Nzega, tumepata madawati 600 kutoka *TEA*…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa John Peter Kadutu atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga.

MHE. JOHN P. KIDUTU: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kukushukuru wewe mwenyewe kunipa nafasi hii kuchangia mchana huu hoja mbili zilizopo ya TAMISEMI pamoja na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijachangia nichukue fursa hii kuipongeza timu yetu ya Bunge kwa ziara nzuri kule Zanzibar, ni katika kuuimarisha Muungano wetu. Nitoe wito kwa niaba ya uongozi wa timu ya Bunge, Wabunge pamoja na Mawaziri tuungane kufanya mazoezi kila asubuhi pale uwanja wa Jamhuri. Mfano mzuri ni wewe Mheshimiwa Naibu Spika umekuwa unatutia moyo kuwepo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niwapongeze Mawaziri wawili hawa, Ndugu yangu Mheshimiwa Simbachawene pamoja na dada yangu Mheshimiwa Angellah.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAMISEMI ni dude kubwa, ukishakabidhiwa Wizara ya TAMISEMI lazima utambue ni dude kubwa na bahati nzuri Mheshimiwa Simbachawene unalijua hilo kwamba TAMISEMI ni dude.

Kwa hiyo, niwapongeze sana kwa hotuba zenu nzuri. Pia nichukue fursa hii kuwapongeza wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kwa kazi nzuri iliyofanyika mpaka tumepata hati nzuri ndani ya miaka miwili na hasa kwa sababu mimi ndiye nilikuwa naongoza Halmashauri ile kama Mwenyekiti wa Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa Waziri wangu Mheshimiwa Simbachawene pamoja na Waziri Mkuu wanisikilize kwa makini, iko hoja nilianza kuizungumza wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, bahati mbaya muda haukuwa rafiki, nayo inahusu waraka aliokuwa ametoa Katibu Mkuu, TAMISEMI wa wakati ule akikataza Mabaraza ya Madiwani kuhoji yale yaliyokuwa yamefanyika wakati Mabaraza yakiwa yamevunjwa. Tarehe 10 Novemba alitoa waraka wa kukataza jambo hilo wakati akielezea taratibu za kuitisha mikutano ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nisome kipengele (g) cha waraka aliokuwa ametoa Katibu Mkuu, TAMISEMI na bahati nzuri mimi niseme ni bahati nzuri kumuondoa pale kunatusaidia kwenye TAMISEMI kukaa vizuri maana makatazo mengine haya hayafai.

Anasema, moja ya kazi za mkutano ule wa kwanza, kipengele (g) anasema; "Kupokea taarifa ya Mkurugenzi wa Halmashauri kuhusu kumbukumbu ya maamuzi ya utekelezaji wa shughuli za Halmashauri zilizofanyika katika kipindi ambacho Baraza la Madiwani lilivunjwa." Akaweka msisitizo kwenye maandishi; "Wajumbe wa Baraza watapokea taarifa hiyo ya

utekelezaji na kuijadili bila kubatilisha maamuzi yaliyofikiwa." Maneno haya siyo mazuri kwa kazi nzuri inayofanywa na Halmashauri. Tukiwa na watendaji ambayo si wazuri maneno haya wanaweza kuyatumia kufanya wanalotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa nini Baraza la Madiwani lizuiwe kuhoji yale yaliyofanyika? Tunao ushahidi kesho yake Madiwani wanarudi yamefanyika jana yake. Sasa kama umewakataza wasijadili maana yake unawakataza haki yao. Kwani kuna ubaya gani Bunge hili likajadili kazi ya Bunge iliyofanyika huko nyuma? Kwa hiyo, kazi kubwa lazima ifanyike hapa. Niombe Mheshimiwa Waziri toa tu tamko ili kufuta Waraka huu nadhani watu wengine huwa wanalewa madaraka, hilo lilikuwa la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuna ahadi ya Rais Mstaafu, Mheshimiwa Jakaya Kikwete wakati wa kampeni za mwaka 2010, eneo letu lilikumbwa na mtafaruku katika kulizimazima jambo lile, Mheshimiwa Kikwete akaahidi Ulyankulu kuwapatia Wilaya pamoja na Halmashauri. Bahati mbaya mtani wangu huyu Mkwere kaondoka hatujapata Halmashauri kule na wala Wilaya haijapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati Mheshimiwa Rais anapita kwenye kampeni za uchaguzi uliopita na yeye akasisitiza jambo hili kuwapatia wananchi wa Ulyankulu Wilaya pamoja na Halmashauri. Kwa kweli wananchi wana imani hiyo kwamba upo utaratibu wa kuhakikisha jambo hili linakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe basi Serikali ije na majibu wakati wa kujibu suala hili limefikia wapi ikizingatiwa kwamba ahadi zimetolewa toka mwaka 2010. Wapo watu hapa wanasema tuzuie kuanzisha maeneo mapya ya utawala. Zinaweza zikawepo sababu kule unapotoka wewe kuna kaeneo kadogo, ukitembea saa tatu umemaliza jimbo lako lakini kutembea Jimbo la Ulyakulu Mheshimiwa Waziri Mkuu unajua ni kati ya majimbo makubwa na lenye watu wengi. Kwa hiyo, tunahitaji jambo hili likamilike ili wananchi wawe na imani, tupate wilaya na Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi kwa Madiwani. Jamani zile pesa Wabunge mnazopata mwishoni Madiwani wanapata shilingi milioni 11, ni kiasi kidogo mno, hebu tuwasaidie. Kama hatuwapi hizi stahili zao za kila siku, zile za mwisho basi wapate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la magari, yapo magari yamekwishakuwa *allocated,* tulizungumza nina imani utakuja na majibu hapa. Watu wanashindwa kukagua miradi kwa sababu magari hakuna lakini magari yameshakuwa *allocated* muda mrefu yapo *yard* kwa nini yasiende *site* yakafanye kazi? Bila shaka jambo hili litakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni juu ya fedha za Serikali Kuu kwenda kwenye Wilaya, *speed* ya pesa kwa maana ya bajeti ni ndogo sana. Kufikia Machi Halmashauri ya Kaliua ilikuwa imepelekewa asilimia 62 tu lakini kwa mwaka jana pesa zilizoletwa kwa ajili ya maendeleo ziliishia asilimia 30 asilimia 70 hazikuletwa. Kwa hiyo, jambo hili linafanya miradi mingine iende kwa kusuasua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala lingine la hizi Sekretarieti za Mikoa kuingilia kazi za Halmashauri. Ni sehemu yao ya kazi lakini mara nyingine wanaingilia shughuli za Halmashauri katika hali ambayo inafanya hata ikosekane maana ya kuwepo Madiwani. Baraza linaamua hivi lakini Sekretarieti za Mikoa zinaingilia kati na maamuzi mengine yanakuwa ya hasara kwa Halmashauri. Kwa hiyo, niombe basi Mheshimiwa Waziri utupe mwelekeo mzuri lakini hizi Sekretarieti za Mkoa ziweze kuzuiwa na ziache mambo mengine ambayo yanaamuliwa na Halmashauri kwa maana ya Madiwani na Baraza lao waweze kutekeleza mambo yao yaende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo kwa shule za msingi na sekondari. Nimekuwa nikisema yupo mzee wetu mmoja nadhani alilewa au uzee au vipi alikataza michezo kwenye mashule. Nishukuru Serikali sasa michezo inachezwa, lakini iko haja ya kuongeza nguvu kwa maana ya bajeti ya ile michezo ya shule za msingi pamoja na sekondari kwa maana ya UMISETA. Pesa inayopelekwa kwa ajili ya michezo hii ni ndogo mno kiasi kwamba michezo haina tija yaani mafanikio ya michezo hii yanakuwa madogo kuliko kawaida. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri ulitolee ufafanuzi jambo hili ili mambo yaende vizuri.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. JOHN P. KADUTU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii, niseme tu naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Sasa tutamsikia Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko halafu Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ajiandae.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu huyu aliyenijalia afya na nguvu kuweza kusimama katika jengo lako hili Tukufu. Pia niwashukuru wananchi wangu wa Lushoto kwa kuniamini ili nije niwawakilishe katika jengo lako hili tukufu. Niendelee kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na timu yake ya Mawaziri, aendelee kutumbua majipu na sisi Wabunge tutaendelea kuyapaka *spirit* ili yakauke haraka siku ya siku

tuyapeleke mahakamani majibu haya ili wakome kuita nchi hii ni shamba la bibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwashukuru Mawaziri wangu wawili Mheshimiwa Angellah Kairuki na Mheshimiwa George Simbachawene. Pia niendelee kuwapongeza ndugu zangu wapinzani maana leo naona wameanza kuchangia hoja, wamebakisha tu kusema naunga mkono hoja, lakini kwa uwezo wa Mungu naamini itafikia hatua hiyo sasa naona roho mtakatifu amewashukia leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mchangiaji mmoja dada yangu Mheshimiwa Grace Kiwelu alisema kwamba tufute mbio za mwenge. Kufuta mbio za mwenge ni sawasawa na kufuta historia ya nchi, hiyo haitawezekana. Kama isivyowezekana kwa CHADEMA kufuta historia ya Edwin Mtei ndani ya CHADEMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuchangia hoja sasa. Niishauri Serikali iendelee kuanzisha vijiji, kata, Halmashauri, wilaya hadi mikoa kwani hii inapelekea kupeleka huduma karibu na wananchi. Historia ya Jimbo la Lushoto au Wilaya ya Lushoto kwa kweli ni kubwa sana na Rais wetu Mstaafu wa Awamu ya Nne alivyotembelea Lushoto alituahidi Halmashauri ya Mji wa Lushoto na Mlalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapoongea juu juu hivi mtu huwezi ukaamini kwamba Wilaya ya Lushoto ni kubwa sana. Nataka niseme ili ujue uhondo wa ngoma uingie ucheze, namuomba Mheshimiwa Waziri wangu Simbachawene atembelee Lushoto ili tunapoongea maneno haya tuwe tunamaanisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Lushoto inapakana na Kenya. Kuna watu wanatoka kwa miguu kufuata huduma Wilayani Lushoto inashindikana wanatumia siku mbili. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu sasa ituangalie kwa jicho la huruma ili kwenye bajeti hii ya 2016/2017 iweze kutupatia Halmashauri ya Mji na iweze kutupatia Halmashauri ya Mlalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye afya. Suala la vituo vya afya ni tatizo la nchi nzima na naamini Serikali yangu sikivu imejiandaa vyema kuweza kujenga vituo hivi vya afya. Pamoja na hayo kwenye mpango huo naomba sasa Waziri, Mheshimiwa Simbachawene tuangalie Lushoto kwa sababu Jimbo la Lushoto lina kituo cha afya kimoja na zahanati nane. Kwa hiyo, huduma hii ya watu wa Lushoto kwa kweli imekuwa na hali ngumu kiasi kwamba kwa kweli inatia masikitiko. Kituo hiki kiko sehemu moja inaitwa Mlola, kutoka sehemu moja wanaita Makanya kwenda Mlola kwanza hata miundombinu ya barabara hakuna, wananchi wa kule wanapata taabu sana.

Hawa wananchi ni wapiga kura wetu tunawategemea, hawa hawayumbi wala hawayumbishwi, hawajui CHADEMA wanajua tu CCM. Kwa hiyo, nikuombe Waziri wangu katika bajeti ya mwaka 2016/2017 hebu liangalie hilo tuweze kuongeza vituo vya afya. *(Makofi)*

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Pamoja na vituo vya afya vilivyopo sambamba…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shekilindi naomba ukae, Taarifa.

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji anayeendelea kuongea …

MBUNGE FULANI: Kanuni gani?

MHE. JAMES K. MILLYA: Kanuni 68(8).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anajaribu kuishawishi nyumba hii au Bunge hili kwamba kwa sababu watu wa Lushoto ni wa CCM, Serikali iliyoko madarakani kwa wale ambao wamechagua CHADEMA, CUF na vyama vingine…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa mpe taarifa kwamba kile alichosema aidha siyo au wewe unayo taarifa ya kumuongezea kwenye kile anachokisema. Ukianza na wewe kuhutubia inakuwa kama unachangia mpe taarifa.

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mengine siyo kwamba yanakatishwa tu tunajaribu kukushawishi na wewe ili kama ni taarifa tunampa ni ili tumfundishe kwamba Serikali iliyoko madarakani haitoi huduma kutokana na …

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa naomba ukae kidogo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tukumbuke taratibu zetu, Taarifa anapewa anayeongea. Kama unataka kuniambia mimi itakuwa ni Utaratibu au Mwongozo kwa muda muafaka, mpe Taarifa anayezungumza.

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili linatakiwa liwe linapendelea pande zote. Jana Naibu Waziri Mheshimiwa Nape alilihutubia Bunge hili…

MBUNGE FULANI: Kaa chini wewe.

NAIBU SPIKA: Toa taarifa kwa anayezungumza kwa sababu unapoteza wakati sasa. Toa taarifa kwa Mheshimiwa Shekilindi, anaongea habari za Lushoto mpe taarifa uliyonayo wewe.

WABUNGE FULANI: Huyoo.

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni Wakili na ni Mwanasheria *double standard* hazitakiwi. Kwa taarifa hiyo Serikali ya CCM…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 72(1) tunaendelea, Mheshimiwa Shekilindi. *(Makofi)*

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba unilindie muda wangu kwani mtoa taarifa, taarifa hiyo nadhani hajajielewa aipeleke Simanjiro lakini Lushoto ni kijani tupu. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Ulipata asilimia mia?

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Ndiyo ni asilimia mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naongelea suala zima la afya. Kwa kuwa Serikali yetu ina mpango mzuri wa kujenga vituo vya afya katika Jimbo la Lushoto, niiombe sasa isimamie hawa watu wa *MSD* kwani dawa hazifiki kwa wakati. Nimechunguza kweli hawa watu wa *MSD* ni majipu kwani *DMO* anapeleka pesa za kununulia dawa labda shilingi milioni tano lakini akifika anapewa dawa za shilingi milioni mbili. Kwa hiyo, hili ni jipu naomba lifuatiliwe. Sisi tunalalamikia madaktari wetu kumbe kuna kidudu mtu hapa katikati anakwamisha huduma nzima ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye suala la kilimo. Uti wa mgongo wa Taifa hili ni kilimo lakini huachi kuongelea pia na miundombinu. Miundombinu ya barabara ndani ya Jimbo la Lushoto hasa za vijijini ni tatizo. Wananchi walio wengi hususan wakulima wanakwamisha na miundombinu ya barabara. Kwa hiyo, niishauri Serikali yangu tukufu kwamba katika bajeti hii ya 2016/2017 ipeleke pesa za ruzuku za kutosha katika Halmashauri ili barabara hizi ziweze kutengenezwa kiwango cha kupitika ndani ya mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo kuna barabara za vijiji ambazo ni tegemezi hata katika Jiji la Dar es Salaam, barabara hii ni ya Mshizihii

- Boheloi, inatoa mazao mengi sana. Barabara nyingine ni ya Kwemakame - Ntambwe - Mazumbai - Baga kwa Mheshimiwa January.

Kwa hiyo, hizi ni barabara ambazo zinatoa matunda na mazao mengi sana. Pia kuna barabara inatoka Malibwi – Kwekanga - Kilole - Ngwelo ni ya muhimu sana kwani inachangia pato kubwa la Taifa hili.

Barabara nyingine ni ile inayoingilia sehemu moja wanaita Kwaikileti – Dindira – Bandi – Kwaboli – Migambo. Barabara hii inatoa matunda mengi mno kiasi kwamba hata tukielezea uchumi wa matunda ya Lushoto basi chanzo chake kinatoka maeneo hayo niliyotaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuzungumzia suala zima la redio ya Taifa *(TBC)*. Nimuombe Mheshimiwa kaka yangu Mheshimiwa Nape, kule kwetu tunasikiliza redio za Kenya tu. Kwa hiyo, ifikie hatua sasa kwenye bajeti hii ya mwaka 2016/2017 basi watutengee mafungu ili wananchi wale waweze kupata taarifa mbalimbali za Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda wangu umeisha, naunga mkono hoja asilimia mia. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko halafu Mheshimiwa Cosato David Chumi ajiandae.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kunipa nafasi hii na mimi kuwa ni sehemu ya wachangiaji. Niwashukuru Mawaziri ambao wamewasilisha hotuba zao nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwenye suala zima la elimu. Eneo la elimu kwenye Jimbo la Mpanda Vijijini bado kuna changamoto kubwa sana. Zipo shule ambazo zimejengwa toka enzi za ukoloni, zimechakaa kwa kiwango kikubwa sana, tulikuwa tunahitaji katika bajeti hii Serikali iangalie mazingira ya kuziboresha zile shule ambazo zimechakaa kwa kiwango kikubwa sana.

Katika Tarafa ya Mwese kuna shule ya Lugonesi na Mwese, shule hizi zimejengwa toka kipindi cha wakimbizi wa Rwanda. Kwa hiyo, shule hizi zimechakaa, tulikuwa tunaomba Serikali iangalie jinsi ya kuzijenga upya ili ziweze kutoa huduma nzuri kwa wananchi na watoto wetu waweze kupata elimu iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zipo shule ambazo zinahitaji kuboreshwa, shule hizo ni za sekondari. Tunazo shule za sekondari kwenye Jimbo la Mpanda

Vijijini saba, bado zina uhitaji mkubwa sana wa walimu. Sambamba na kwenye shule za msingi ambako kunahitajika idadi ya kutosha ya walimu ili shule hizo zitoe elimu inayofanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo maeneo mengine mapya ya kiutawala, tunalo eneo la Mishamo ambalo raia wapya wamepata uraia. Eneo hili lina changamoto kubwa sana kwani idadi ya watu ni wengi lakini bado tunahitaji huduma za kijamii hasa kwenye suala la elimu. Tunaomba Serikali iangalie kwa kina yale maeneo ambayo yalisahaulika kupata huduma za kimsingi ambazo huko nyuma zilikuwa zinatolewa na *UN* kwa sasa zinategemewa sana kutolewa na Serikali yetu. Naomba Waziri mwenye dhamana aelekeze nguvu, aende akaone mazingira ambayo vijana wanasoma, shule moja inachukua idadi ya wanafunzi karibu 1,800 na darasa moja unakuta lina wanafunzi zaidi ya watoto 100, tunaomba eneo hilo mliangalie sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni maji. Jimbo langu lina tatizo sana la maji kwenye vijiji vingi. Kipo kijiji cha Kamjelam ambacho kiko eneo la Mishamo, hakuna maji. Tunahitaji eneo hili kwa ujumla kwenye Kata za Bulamata, Mishamo, Ilangu na Ipwaga, wajaribu kufufua visima ambavyo vilikuwa vimechimbwa na *UN* kipindi hicho cha nyuma. Serikali ione umuhimu sasa wa kuangalia vile visima ili viweze kutoa maji na wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni barabara za vijijini. Maeneo ya Jimbo la Mpanda Vijijini yana vijiji vingi sana ambavyo havipitiki kwa sababu barabara zake si nzuri. Tulikuwa tunaomba Serikali iweze kuongeza bajeti hasa kwenye Wilaya ya Mpanda ambayo kimsingi ndio imezaa Halmashauri zote ambazo zimezaliwa katika Mkoa wa Katavi.

Kwa hiyo, tunaomba waelekeze nguvu kujenga miundombinu ambako kuna uzalishaji mkubwa sana wa mazao ya mahindi na mpunga, yanayotegemewa kuchukuliwa kutoka vijijini kuyaleta makao makuu ya Wilaya na mkoa na baadaye sehemu ya Mikoa ya Mwanza Shinyanga wanakuja kununua mazao hayo. Sasa ili kuweza kuboresha na wakulima waweze kunufaika, tulikuwa tunaiomba Serikali iboreshe barabara za kijiji cha Kabage kuja barabara kuu inayounganisha kutoka Kagwila - Karema. Iboreshe barabara za kutoka Kalilankurukuru kwenda kijiji cha Kamsanga na iboreshe barabara za kwenda kijiji cha Mnyagala ambako kuna uzalishaji mkubwa wa mazao. Ili wananchi waweze kuzalisha na wapate bei nzuri lazima Serikali iboreshe barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ambazo zinahitaji kufanyiwa urekebishwaji kwa kiwango kikubwa ni maeneo ya vijiji vya Mishamo ambako barabara nyingi zimeharibika. Tunaomba Serikali iweze kusaidia iweze kufanya

kazi nzuri na iweze kutoa huduma nzuri kwa ajili ya kupita ili wananchi waweze kuzalisha mazao yao na yapate nafasi ya kupelekwa kwenye masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutaiachia tu Halmashauri ya Wilaya kwamba ndiyo itaweza kusaidia hizo barabara, itakuwa ni jambo gumu kwa sababu eneo la Wilaya ya Mpanda ni kubwa na ukubwa wa Jimbo umekuwa mkubwa sana tofauti kabisa na maeneo mengine. Jimbo la Mpanda Vijijini ni jimbo ambalo lina uwezo wa kuchukua Mkoa mzima wa Kilimanjaro, ukachukua na sehemu ya Zanzibar, ukiunganisha unapata Jimbo ambalo naliongoza mimi. Lina kilometa za mraba 16,900 kitu ambacho kuwafikia wananchi inakuwa ni taabu. Naomba Serikali iangalie ukubwa wa Jimbo hili ili liweze kugawanywa na wakati mwingine kutoa huduma zinazofanana ili tuweze kuwafikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwenye suala la afya. Eneo la afya Mheshimiwa Anna Lupembe amezungumzia sana na mimi nalitilia mkazo wa aina yake kwa sababu eneo hili ni muhimu sana. Kwanza, hatuna vifaa vya kuwafikia wananchi kwa maana vituo vya afya havina *ambulance*. Halmashauri hii ilipokuwa inatoa mgawanyo kwa Halmashauri zingine, kila Halmashauri iliyokuwa inazaliwa walikuwa wanatoa magari kutoka Halmashauri mama kuyapeleka kwenye maeneo ya Halmashauri zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Halmashauri Mama kwa maana ya Wilaya ya Mpanda bado haina vitendea kazi kwa maana ya magaari. Ukienda kwenye sekta ya elimu hawana magari, sekta ya afya na vituo vya afya havina magari. Naiomba Serikali iangalie umuhimu wa kununua *ambulance* kwa ajili ya Halmashauri ya Mpanda ambayo itasaidia kutoa huduma kwenye vituo vya afya vya Mishamo, Mwese na Karema. Idadi ya wananchi walio wengi hasa akina mama wajawazito wanapoteza maisha yao kwa sababu ya umbali wa kufikia huduma ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho tunaomba Serikali iangalie kwenye sekta ya afya, itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Mkoa wa Katavi. Ni eneo pekee ambalo kiutawala halijakuwa na Hospitali ya Mkoa. Bado wanatumia Hospitali ya Halmashuri ya Wilaya ya Mpanda kama Hospitali ya Wilaya na Mkoa kwa ujumla. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iangalie umuhimu wa kuweka mkakati wa kutoa fedha za kutosha ili kujenga Hospitali ya Mkoa itakayotoa huduma kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Serikali kwa namna nyingine kwa kutupa Wilaya mpya ya Tanganyika. Bado Wilaya hii ya Tanganyika haijapata makao makuu yake. Niiombe Serikali iangalie mazingira ya kuweza kuharakisha mchakato wa kupeleka makao makuu hasa pale yalipokuwa yamelengwa na Waheshimiwa Madiwani walipokuwa wamependekeza. Ni vizuri Serikali

itakapokuwa imepeleka huduma hiyo na mchakato wa Halmashauri kwa ujumla ukafanyika mapema utasaidia kupeleka maendeleo kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa namna ya pekee kabisa, naomba niwape hongera sana Mawaziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Kairuki na Naibu Waziri, bado ni vijana na mna nguvu, tunataraji mtakimbia na kasi hii na mtafika. Pia kwa namna pekee naomba nimshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara yenu ni mtu msikivu sana, Alhaji Iyombe, kila ukienda ofisini kwake ni mtu wa msaada sana. Alhaji Iyombe kama unanisikia hongera sana kwa utulivu wako na utu uzima wako, endelea kulea vijana hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa na machache ya kuzungumzia. La kwanza ni utawala bora. Wakati Mheshimiwa Bashe anachangia alizungumzia habari ya majizi ambayo yanahama kutoka halmashauri moja kwenda nyingine. Mheshimiwa Waziri Mkuu maadam uko hapa nikukumbushe jambo moja kwamba moja ya majizi makubwa nililokuletea lilipelekwa Nzega kutoka Kasulu.

Mheshimiwa Simbachawene liko tatizo kubwa la wizi uliotokea pale Kasulu wa shilingi bilioni 5.9 kati ya mwaka 2013/2015 na haya majizi bado yanatembea tu na mengine yamehamishwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu katika yale majizi yaliyokubuhu, moja ya majizi yale lilitoka Kasulu likaenda Nzega na kule Nzega nimeambiwa amestaafu baada ya kutuibia pesa nyingi sana. Haiwezekani! Huyu mtu lazima atafutwe na afikishwe kwenye mikono ya sheria.

Kwa hiyo, kusema kwamba Nzega ilikuwa ni *dumping ground* nadhani ni kweli maana hata hilo jizi lililokubuhu lilitoka Kasulu likapelekwa Nzega. Mheshimiwa Waziri Mkuu mtusaidie majitu haya yakamatwe yafikishwe kwenye vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo napenda kulizungumzia alilisema Mheshimiwa Makamba siku anachangia bajeti ya Waziri Mkuu, juu ya utawala bora. Mheshimiwa Simbachawene tuna Halmashauri zaidi ya 34 zinaongozwa na wapinzani wetu kwa maana kwamba baada ya matokeo ya uchaguzi walichaguliwa na wanaziongoza. Nawashauri sana, hizi Halmashauri ambazo zinaongozwa na wapinzani na hizi zinazoongozwa na wana CCM zenye wapinzani wengi vilevile, kuna haja kabisa ya kuzipangia mkakati wa

mafunzo maalum vinginevyo hazitatawalika, wataishia kwenye ubishi tu, ndio ni zote, hazitatawalika hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ile Mheshimiwa Makamba alisema jambo la msingi kwamba chama cha siasa kikishinda uchaguzi kinaunda Serikali, ni kweli na ndiyo utamaduni wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Siyo kuunda Serikali tu, kinaanza kutekeleza ilani yake ya uchaguzi na hakiishii hapo lazima kipate *space* ya kutawala na wapinzani wetu lazima watupe nafasi ya kutawala, hilo halina ubishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, *equally the same*, chama tawala nacho lazima kijue kwamba kuna nafasi ya wapinzani katika demokrasia na hiyo *space* lazima iwepo. *Space* hiyo Mheshimiwa Simbachawene haiwezi kutoka mbinguni lazima hawa watu wawe *trained*. Halmashauri 34 zinaongozwa na wapinzani *per se* lakini ziko nyingine kama 14 hivi zina wapinzani wengi kwa maana kwamba unakuta CCM tumezidi mmoja, wawili, watatu au wanne, kwa sababu ya dhana nzima ya utawala bora lazima kuwe na *special program* kupitia TAMISEMI kuwajengea uwezo vyama na Halmashauri zote hizi na hasa hizi ambazo zinaongozwa na CCM kwa wingi na hizi ambazo zinaongozwa na wapinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu wa Kambi ya Upinzani niwakumbushe kitu kimoja, *opposition* maana yake ni kuikumbusha Serikali ya siku isilale usingizi.

MBUNGE FULANI: Kama itakubali kukumbushwa.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Ndiyo utamaduni huo lakini na ninyi kwa sababu mlishindwa uchaguzi mkuu lazima mtoe *space* ya kutawala kwa watu walioshinda na hilo hatubishani. Mimi sikuwepo siku mbili hizi nimeshukuru sana leo kuona wapinzani wanachangia ndiyo demokrasia hiyo. Ile kukimbia hupati kitu unaposema unatusaidia sisi tujue unachosema, unachofikiri lakini mkikaa kimya mlikuwa mnatunyima haki yetu.

MBUNGE FULANI: Eeeeh.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Ndiyo na mlikuwa mnafanya vibaya, lakini sasa nashukuru busara zimeingia, mmewasomesha wameelewa na tutakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo napenda nilizungumzie ni mipango miji. Mheshimiwa Simbachawene unazungumza kwenye hotuba yako upangaji wa miji na kwamba umeisha-*identify* miji 600, hiyo miji yenyewe iliyopo haina Maafisa wa Ardhi, Maafisa Mipango Miji na haina *Valuers*. Sasa niulize, hivi

kuna tatizo gani la kuajiri moja kwa moja toka kwenye vyuo vyetu vya ardhi wataalam hawa wakaenda kwenye Halmashauri zetu ili kuzuia miji holela? Hili ni jambo muhimu sana, Waziri wa Ardhi uko hapa hebu mshirikiane na TAMISEMI muweze kuondoa tatizo hili. Huwezi kuzungumzia kupanga miji kama huwezi kuwa na wataalam ambao kazi yao ni kupanga miji hii. Jambo hili linawezekana na mnaweza mkalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne ni nyumba za walimu. Nadhani walimu wenzangu mtakubaliana na mimi kwamba kama kuna shida kubwa iliyopo kwenye halmashauri zetu ni nyumba za walimu jamani, walimu hawana nyumba za kukaa, kabisa. Unashangaa sasa kila Halmashauri inakuwa na utaratibu wake wa kuweka kwenye bajeti nyumba 5, 10, 12. Nilikuwa naangalia kwenye kitabu hiki cha TAMISEMI kwenye *development*, Mheshimiwa Simbachawene una karibu shilingi trilioni moja kwa ajili ya *development*. Hebu Mheshimiwa Simbachawene hizi fedha za *development* katika eneo la nyumba za walimu kwa nini ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda umeisha.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache hapa, nitaanza na tangazo la Wabunge watakaoanza kuchangia mchana. Ataanza Mheshimiwa Cosato Chumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Kandege, Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambi, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah na Mheshimiwa Aysharose Mattembe.

Waheshimiwa Wabunge, yako matangazo mengine hapa, tangazo moja ni la kuwakumbusha Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwamba kuna *caucus* saa 9.00 mchana ukumbi wa Pius Msekwa.

Tangazo lingine linahusu kikao cha Kamati ya Katiba na Sheria leo tarehe 29/04/2016, chumba namba 229, saa 9.00 mchana. Sasa naona hizi saa tisa mchana zinagongana, nadhani wanaohusika watajaribu kuona ni namna gani wafanye vyote.

Tangazo lingine ni kuhusu kuanza zoezi la kutumia *biometric* katika kusaini mahudhurio. Mnataarifiwa kwamba zoezi la kutumia *biometric* katika kusaini

maudhurio wakati wa kuingia Bungeni litaanza rasmi Jumatatu, tarehe 2/05/2016. Maeneo yatakayotumika ni kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza, ni sehemu ya mapokezi kuingia ukumbi wa Bunge baada ya mashine za upekuzi yaani hapo nje. Sehemu ya pili ni mageti ya kuingilia Ofisi ya Bunge ya *VIP* na Msekwa. Sehemu ya tatu ni pembeni mwa lango kuu la kuingilia Jengo la Utawala na sehemu ya nne ni lango la kuingilia Ukumbi wa Msekwa.

Aidha, Waheshimiwa Wabunge ambao hawajafanya usajili wanaombwa kufanya hivyo kwa kuwa hakutakuwa na kusaini fomu iliyokuwa ikitumika humu ukumbini. Nadhani hilo tangazo tumelielewa, kuanzia Jumatatu hakutakuwa na karatasi za kusaini.

Waheshimiwa Wabunge, pia nalazimika tukumbushane Kanuni kadhaa, moja ni Kanuni ya 66 kuhusu staha ndani ya Bunge. Yapo mazingira ambayo Wabunge wanapita mbele ya mtu anayechangia wakati akiendelea kuongea. Tunakumbushana kwa sababu huu ni mwanzo lakini baadaye tutaanza kutaja majina ili urudi ulikotoka ukatulie mpaka mtu amalize kuchangia. Sasa tusifikie hapo Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni hiyo hiyo ya 66(3)(e) kinaongelea simu za mkononi. Tukumbushane tu kwa sababu kuna mtu ananyanyuka ameishikilia simu anaweka sikioni yaani kwamba kashapokea anaenda kumalizia kupokea nje. Sasa kwa mujibu wa Kanuni zetu huo sio utaratibu mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni nyingine ambayo ni muhimu tuifahamu ni Kanuni ya 60(2) na kifungu kidogo cha (16), kinazungumza kuhusu namna ya kuita Wabunge na Mawaziri humu ndani. Leo asubuhi limetokea jambo la kurekebisha jina mtu anapotajwa kwa jina lake la mwisho, ikiwa mtu ameweka neno Mheshimiwa kabla ya majina mawili ama matatu ya mtu au ameweka neno Mheshimiwa kabla ya jina la mwisho la mtu huyu, yuko sahihi anakuwa hajakosea jina.

Kwa hiyo, naomba wakati tukiwasiliana tuone hivyo. Majina yanayopaswa kurekebishwa ni yale ambayo aidha alivyotamka linaleta maana nyingine ama linakupa wewe jina lingine lakini akitamka jina la mwisho la kwako wewe mwenyewe na akaweka neno Mheshimiwa anakuwa yuko sawasawa hajakosea jina lako.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, nasitisha Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI: Hoja za Serikali. Hoja ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora, kwamba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Majadiliano yanaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2016/2017

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Katika orodha niliyonayo mbele yangu, mchangiaji wetu wa kwanza mchana huu atakuwa ni Mheshimiwa Cosato David Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuipongeza Serikali kwa usikivu wake wa kusikiliza kilio cha wananchi na kutoa agizo la kukubali kuagiza sukari. Huo ni uthibitisho kwamba hii ni Serikali tulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo napenda pia kuwashukuru Mawaziri. Kuna mjumbe mmoja alipokuwa anachangia alisema Mawaziri hawa wako *reachable,* kwa kweli na mimi nawapongeza kwamba ni kama simu ukipiga inakuwa *reachable*. Wakati mwingine hawa hata kama hujapiga wako *reachable*.

Nasema hivi kwa sababu nilifanya ziara katika Jimbo langu na Mheshimiwa Jafo, Naibu Waziri alipoona taarifa ya ziara ile na yeye akaenda kutembelea pale mahali ambapo mimi nilikwenda kutembelea ili kujionea mwenyewe zile changamoto. Kwa hiyo, hii ni uthibitisho wa usikivu pia wa Mawaziri hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo nianze kwanza kwa kusema kwamba tumesema tunapokusudia kujenga uchumi wa viwanda sekta binafsi ni injini ya kujenga uchumi huo. Mimi napenda kuongeza kwamba injini hii bila *oil*, ambapo kwangu mimi *oil* ni utumishi wa umma *(public service)*

maana yake ni kwamba injini hii inaweza ika-*knock*. Kwa sababu hiyo basi, niiombe Serikali kupitia Wizara husika iwatazame watumishi wa umma walau kwa baadhi ya mambo kwa mfano fedha zao za likizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetokea kwenye utumishi wa umma ambapo ikiwa mwaka huu utakwenda likizo basi utalipwa fedha yako ya nauli mwaka unaofuata hulipwi, unalipwa *alternatively*. Sasa naomba wakati Serikali inaendelea na jitihada za kuongeza makusanyo na kubana matumizi basi iwatazame watumishi wa umma katika suala hili. Pia iwatazame katika fedha zao za uhamisho kwa mfano walimu. Hata katika hii nauli unakuta mtu anakwenda likizo halafu anaambiwa fedha yako utakuja kulipwa ukirejea na inaweza kumchukua hata miaka mitatu, mwingine anakata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie nauli kwa watumishi wa umma wanaokaa maeneo ya mijini. Mnafahamu kwa mfano Jiji la Dar es Salaam Serikali ina utaratibu wa kutoa mabasi lakini kuna maeneo mengine ya mikoani ambako watumishi wanatoka umbali mrefu kwenda kwenye maeneo ya kazi. Sasa kama sehemu ya kuwaongezea *morale* na kuwapunguzia ukali wa maisha, nashauri Serikali ilitazame jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kuhusiana na Waraka huu wa Serikali, labda niusome. Kuna Waraka wa TAMISEMI Na.CFB/173/355/0 wa tarehe 06/06/2011 wenye kichwa cha habari kinachosema Majukumu ya Maafisa Biashara na namna bora ya utoaji taarifa. Mojawapo ya majukumu katika waraka huu ni kuhamasisha shughuli zilizo chini ya viwanda, biashara na masoko na uwekezaji pamoja na kutoa elimu ya ujasiriamali ili kuongeza kipato cha wananchi na kuongeza wigo wa kodi katika Serikali za Mitaa na Serikali Kuu.

Sasa ukienda katika halmashauri zetu ofisi za biashara si kitengo wala si idara isipokuwa ziko ndani ya Idara ya Fedha. Naziomba Wizara hizi mbili zijaribu kuangalia muundo wa Maafisa Biashara ili kusudi hata hizi shilingi milioni 50 ambazo tunatarajia zitatoka kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais basi zikawe na tija ili Maafisa Biashara wasibaki tu kuwa watu wa kukagua leseni bali wawe watu ambao wanaweza kusaidia wananchi katika kung'amua fursa mbalimbali za kijasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu nijielekeze katika Sekretarieti ya Ajira. Napenda kuipongeza kwa sababu kweli tuna changamoto kubwa ya ukosefu wa ajira lakini jinsi ambavyo imejitengeneza kimtandao, jinsi ambavyo watu wana-*apply online* na maombi yao yanaendelea kutunzwa *online* ni jambo la kupongeza kwa sababu pia linapunguza malalamiko katika ajira ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo niombe pengine ingeanza kwenda kwenye *zones* ili kuwapunguzia waombaji wa nafasi za kazi gharama zile za nauli na malazi kwa sababu mpaka sasa hivi pamoja na kuwa kuna nyakati inafanya *interview* kwenye maeneo ya nje ya Dar es Salaam lakini asilimia kubwa ni Dar es Salaam. Sasa uwezo utakapoongezeka basi tuanze walau na *zone* kwa ajili ya kuwasaidia watafuta ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, nijikite sasa kwenye Jimbo langu. Namshukuru tena Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea katika shule ya msingi Mchanganyiko Makalala. Shule hii ina watoto wenye mahitaji maalum. Kwa sababu shule hii iko katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga lakini ni kama shule ya kitaifa kwa sababu inachukua watoto kutoka maeneo mbalimbali ya nchi yetu basi Serikali iitazame kwa macho mawili. Nampongeza Naibu Waziri na Wizara kwa ujumla kwa hatua ile ya kutembelea shule ile, naamini changamoto zile alizojionea zitamsaidia katika kuona umuhimu wa kuitazama shule hii kwa macho mawili katika uwiano wa walimu lakini pia miundombinu ambayo kwa kweli siyo rafiki sana kwa watoto wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala la elimu naiomba Wizara, Mheshimiwa Rais alipozungumza na Wazee wa Dar es Salaam tarehe 13/02/2016 aliahidi kwamba ataupa Mkoa wa Dar es Salaam shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kukabiliana na ongezeko la wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza.

Niiombe Serikali hata sisi tunaotoka kwenye Halmashauri za Miji changamoto hii tumekutana nayo. Mafinga pale kuna ongezeko la watoto kwa asilimia 135. Serikali itutazame kwa sababu kwanza ni Halmashauri mpya bado haina makusanyo lakini pia iko mjini. Sasa sisemi kwamba na sisi tupewe shilingi bilioni mbili lakini tutazamwe kwa chochote kitakachoweza kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusiana na suala la pampu. Pale tuna pampu ilipaswa iwe imefungwa toka mwezi wa kumi na moja lakini mpaka wakati huu yule aliyepewa kazi ya ku-*supply* amekuwa anapiga chenga. Kwangu naona hili ni jipu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kwa sababu wao ndiyo walitakiwa wanunue pampu na kutufungia sisi kwenye Halmashauri ya Mji. Ametuletea pampu haina *TBS certification*, haina *manual*, maana hata ukinunua simu Kariakoo ya shilingi 18,000 unapewa *manual,* lakini pampu hii hata *manual* haina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie katika suala la utawala bora. Wenzetu upande wa pili kule wanalialia Rais apunguze kasi ya kutumbua majipu. Mimi nasema tumuunge mkono Mheshimiwa Rais. Kuwa *opposition* sio kupinga kila kitu. Madawati kupinga, ujenzi wa maabara kupinga, hapana, kuna mambo

tumuunge mkono Mheshimiwa Rais. Mimi naamini ninyi huko si majipu kwa hiyo mpunguze kulialia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, nimalizie kuzungumzia wastaafu ambao wanahudumiwa na *LAPF* wanalalamika kwamba wenzao wa *central government* tayari wameongezewa lakini wao bado. Kwa hiyo, niombe pia suala hilo litazamwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, niwahakikishie wana Mafinga kwamba nitaendelea kuwatumikia bila kuangalia rangi wala itikadi zao, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Chumi, tunaendelea na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya TAMISEMI na Utawala Bora na Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kueleza kwamba ni ukweli usiopingika hali za Halmashauri zetu nchini kwa ujumla wake ni mbaya sana. Halmashauri hizi zina hali mbaya kwa sababu nyingi zimekuwa tegemezi na kwa asilimia kubwa zinategemea fedha kutoka Serikali Kuu. Halmashauri zetu hizi pia vyanzo vile muhimu ambavyo vingewezesha mapato ya Halmashauri zetu kuongezeka, kwa kiwango kikubwa vimechukuliwa pia na Serikali Kuu. Kwa hiyo, tumeziacha Serikali zetu za Mitaa katika hali ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine kuna uhaba mkubwa wa watumishi katika Serikali za Mitaa kwa maana ya rasilimali watu. Takwimu zinaonesha tuna uhaba wa watumishi 43,560 katika idara 470 za Halmashauri zetu nchini, huu ni upungufu mkubwa sana. Kama kuna upungufu huu mwisho wa siku hata ufanisi wa fedha zinazopelekwa unakuwa hauonekani au haupo kabisa au ufanisi unakuwa kwa kiwango kidogo sana.

Kwa hiyo, ni muhimu sana Serikali ikaangalia ni namna gani wanakwenda kupunguza uhaba wa watumishi walioko katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine unapoongelea suala la Serikali za Mitaa huwezi kuwaacha Madiwani pembeni. Ni kwa muda mrefu Serikali mmewatelekeza Madiwani si kwenye maslahi, si kwenye kujengewa uwezo, Madiwani maslahi yao yanaboreshwa kwa kiwango kidogo sana. Ukiangalia sisi Wabunge hatuna utofauti sana na Madiwani lakini tunawaacha Madiwani na sisi tukiwa Bungeni muda mrefu wanaotufanyia kazi kwa kiwango

kikubwa na kutusaidia ni Madiwani. Ni muhimu sana Serikali ikaangalia namna gani maslahi ya Madiwani yanaboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si maslahi tu, wakati wa awamu iliyopita walifuta mafunzo *(capacity building)* kwa Madiwani. Hivi unampeleka Diwani akamsimamie Mkurugenzi na watendaji wake ambao wao ni wataalam wa mambo fulani fulani halafu Madiwani wetu wamechaguliwa tu kwa kigezo cha kusoma na kuandika, hana ujuzi wowote, baadhi lakini wako wengine ambao wana ujuzi lakini walio wengi hawana ujuzi huo, hivi kwa nini Serikali isiirudishe ile programu ya kuwajengea uwezo Madiwani kwa kuwapatia mafunzo. Mimi nilikuwa Diwani, nakumbuka kulikuwa kuna programu ya kuboresha Serikali za Mitaa, tulikuwa tunapelekwa mafunzo ya miezi sita lakini inakwenda kwa awamu, ilitusaidia kutujenga na kusimamia zile fedha zinazopelekwa. Kwa hiyo, ni muhimu pia mkalitazama hili muone namna gani Madiwani wanarudishiwa hizo programu za kujengewa uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia kuhusu TAMISEMI ni udhaifu mkubwa ulioko katika usimamiaji wa Bajeti na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa. Kuna udhaifu mkubwa sana, udhaifu huu unaendana na bajeti zilizoidhinishwa kutokufuatwa na hizi bajeti wakati mwingine hazifuatwi kwa sababu ya matamko ya viongozi mlioko ngazi za juu na mlioko katika Serikali Kuu. Mfano, Halmashauri 34 zimetumia kiasi cha shilingi bilioni 33 kwa ajili ya ujenzi wa maabara. Hakuna mtu anayepinga au anakataa umuhimu wa maabara, umuhimu wa maabara unajulikana lakini ujenzi huu na fedha hizi zimetokana na tamko lililotolewa na Rais bila kuangalia wakati huo anatoa tamko kwenye bajeti za Halmashauri za Wilaya fedha hizi zipo? Kwa hiyo, inaonesha kuna shilingi bilioni 33 zimetumika kinyume na bajeti eti kujenga maabara katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine, kuna takriban upotevu wa shilingi bilioni nane kwa ajili ya malipo yaliyofanywa na Serikali za Mitaa bila kuwepo na nyaraka za malipo. Pia kuna Halmashauri 62 zimefanya malipo ya shilingi bilioni 1.4 kinyume na vifungu vilivyopitishwa katika bajeti. Sasa kama Serikali hizi za Mitaa hazifuati bajeti ambayo imejiwekea hakuna sababu ya kupitisha bajeti au kama kuna matamko yanayotolewa bila kuangalia uhalisia wa Serikali zetu za Mitaa hakuna sababu ya kuwa na Serikali za Mitaa kama hatutambui na kuthamini yale ambayo yanayopitishwa katika bajeti zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ripoti ya CAG anasema watekelezaji wa miradi 76 walifanya matumizi nje ya bajeti ya kiasi cha shilingi bilioni 4.6. Yote ni kukiuka bajeti waliyojiwekea, yote ni kukiuka Sheria ya Fedha ambayo ipo. Wanasema matumizi mengine yalifanywa nje ya bajeti na yameongezeka, CAG anasema matumizi nje ya bajeti yameongezeka kwa asilimia 224. Kwa

hiyo, haya ni mambo ya kuyaangalia na kuyasimamia kuona yanaondoka katika Serikali zetu za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie eneo lingine la elimu bure. Mmesema mnatoa elimu bure, lakini nilidhani mngepaswa kujiridhisha na kuangalia hivi ni kweli mnaweza kutoa elimu bure au mlikurupuka tu mkachukua llani yetu na yenyewe mkaweka kwenye llani yenu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo, kuna watu wamefanya tafiti, wanasema ili uweze kutekeleza elimu bure unahitaji takriban shilingi bilioni 715 kwa mwaka mmoja wa fedha. Ili uweze kutekeleza elimu bure maana yake unahitaji mambo makuu manne; jambo la kwanza ni kutoa ile ruzuku ambayo ilikuwa inatolewa ya shilingi 10,000 kwa shule za msingi na shilingi 25,000 kwa shule za sekondari. Kama ile ruzuku mmeamua kuitoa kwa sababu mnasema ni elimu bure maana yake Serikali inahitaji karibia shilingi bilioni 130 kwa shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kama mnaondoa ada ya shilingi 20,000 kwa watoto wa sekondari, Serikali inahitaji kuwa na shilingi bilioni 31.5 ili kufidia ada hiyo. Hivi hizi fedha hizi mnazo? Si huwa mnasema kasungura kadogo? Safari hii kamenenepa? Nadhani mnapaswa kuangalia haya mliyoyasema ya elimu bure hivi mnakwenda kutekeleza? Halafu mmetoa Waraka mwingine Na. 5 wa elimu mnasema kama wanataka wapate kibali kwa Mkuu wa Mkoa, sasa kwa nini hizi *contradiction,* si mmesema elimu bure? Basi acheni bure mbebe huo mzigo, mtafute fedha hizi mwende kutekeleza elimu bure ambayo mnataka kuitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwa haraka ni kuhusu Mfuko wa Vijana na Wanawake. Waheshimiwa Wabunge wengi tunachangia kwamba tuhakikishe Serikali za Mitaa zinatenga ile *10 percent* kwa ajili ya Mfuko wa Vijana na Wanawake lakini lazima kidogo twende mbali ya hapa. Mifuko hii ukiangalia mwongozo wake na mwongozo huu ulipitishwa na Bunge hili mwaka 1991, ni mwongozo wa zamani ambao hauendani na uhalisia wa leo.

Katika Bunge la Kumi niliuliza Swali Na. 379 kuitaka Serikali i-*review* ule mwongozo wa kuanzisha Mifuko ya Vijana na Wanawake, ni mwongozo wa zamani sana kwa sababu unasema kikundi cha watu watano watapewa mkopo wa shilingi 500,000. Hivi unawapa mkopo wa shilingi 500,000 kwa watu watano, shilingi laki moja moja inasaidia nini, haisaidii kitu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ni vizuri mkaangalia tena kwa upya namna gani ya kuu-*review* mfuko huu uendane na hali halisi iliyoko katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye Wizara ya Utumishi na Utawala Bora, kuna Mfuko wa *TASAF*. Mfuko wa *TASAF* ni mkopo kutoka *World*

Bank ambao ni dola za Kimarekani milioni 200 lakini fedha hizi zinakwenda kupewa watu kwenye kaya, wanasema kaya maskini na kwenye kaya maskini wanaangalia vigezo mbalimbali kama kuna wategemezi na vitu kama hivyo na kwenye kila kaya *range* ya fedha hizi ni kati shilingi 20,000 mpaka shilingi 62,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kuwakwamua watu wetu kutoka kwenye hali mbaya ya umaskini hivi ni kuwapa fedha mkononi? Kwa sababu ukimpa fedha mkononi itamsaidia nini? Kwa sababu hizo hizo Kaya maskini wakati mwingine hata mlo kwa siku ni taabu, ukimpa shilingi 20,000/= unamwendelezaje aondokane na huo umaskini? Kwa hiyo, ni muhimu mkaangalia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na mifuko mingi ambayo mwisho wa siku hatuoni manufaa yake.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umeisha.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Unajisikiaje baada ya kuchangia, unajisikia vizuri eeh, haya. *(Kicheko)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko atafuatwa na Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuweza kunipa na mimi fursa hii niweze kuchangia kwenye bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia maeneo kadhaa kwa sababu dakika 10 ni chache sana. Nianze na suala zima la utawala bora na utawala bora wenyewe nitaanzia suala la kuwanyima fursa Watanzania kuweza kuona ni nini wawakilishi wao wanafanya Bungeni. Ni dhahiri kwamba tumesikiliza michango mingi sana na mingine kwa kweli inasikitisha, ukimwona Mbunge anasimama, anaunga mkono hoja hii dhalimu ya kupoka haki ya uhuru wa wananchi kuweza kujua wawakilishi wao wanafanya nini *then* unatakiwa ujiulize mara mbili mbili kwamba hata hao wananchi waliomleta huyu mwakilishi huku walifanya makosa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilisikitishwa na Mheshimiwa kijana kabisa Halima Bulembo, anasema tukionekana kwenye *televisioni* ni kwamba tunatafuta umaarufu. Nikasema labda nitembee kwenye hoja yake hiyo hiyo

nimuelimishe kidogo huyu mdogo wangu. Akumbuke kwamba sisi wengine tuliweza kupata *morale* ya kutaka kuingia kwenye siasa baada ya kuwaona wanawake wenzetu akina Mama Abdallah, Anna Kilango, Halima Mdee na wengine na hata ukiwaona watu waliogombea Udiwani na Wenyeviti wa Mitaa wanapata *inspiration* wanapomwona Esther Matiko anachangia nini, fulani anachangia nini, wanaona kwamba hata sisi wanawake kumbe tunaweza tukiingia kwenye uwanda huu wa siasa. Sasa leo mwanamke kabisa anapiga vigelegele hiyo *fifty fifty* mnafika vipi? Yaani mnaungana na wanaume ambao wanaona hii ni njia pekee ya kuwakandamiza ninyi msifikie lengo lenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wengine tuna malengo makubwa, kuna Mheshimiwa mwingine alichangia kaka yangu Chegeni anasema kwamba twende tukafanye kazi Jimboni. Mimi lengo langu siyo kulitumikia Jimbo la Tarime tu kuna siku nataka niwe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, ninachokiwakilisha hapa nataka Tanzania nzima itambue Esther Matiko anafanya nini kwa Taifa lake wala siyo Tarime tu. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Hamia CCM.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Kwa hiyo, kama ninyi mna *short vision* ya Jimbo tu na mnaamua kuwanyima Watanzania haki zao, jitafakarini mara mbili na mkienda pale mnaapa kuitumikia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania halafu mnaikiuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani alisema na Wabunge wengine wamechangia mkubali, msikubali suala hili liko wazi na nitaomba mpitie hii Katiba, tulipokuja tulipewa kibegi kina hivi vitu vyote msiende kuweka ndani ya uvungu pitieni hii Katiba. Mwanasheria Mkuu, Waziri wa Fedha na wengine waliochangia juzi hapa mlikuja mkapotosha lakini ni dhahiri Rais hawezi kuhamisha fungu moja kwenda lingine bila idhini ya Bunge tunaopitisha hapa, Mwenyekiti wewe ni Mwanasheria unajua, ni Mfuko wa Dharura tu. Kasomeni vizuri kuanzia Ibara ya 135 mpaka 140, kama hamna Katiba nitawatolea *copy* niwape ili tuweze kumshauri Rais asivunje Katiba na sheria yetu ya nchi. Inawezekana kabisa Rais ana lengo zuri aje sasa watuletee *statement* ya *reallocation* tuipitishe, mwenye mamlaka hayo ni Waziri au ndiyo hiyo tunasema kwamba hamna *instrument* kwa hiyo Rais inapoka mamlaka ya Waziri wa Fedha na kufanya anachokifanya ninyi mnapiga makofi, haikubaliki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie sasa, TAMISEMI na nachangia kwenye Jimbo langu, nimechangia Kitaifa narudi sasa kwenye Jimbo langu.

MBUNGE FULANI: Sawa sawa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bure ni sawa sawa na mgonjwa yuko *ICU*. Kuna siku nilisema tuseme tumepeleka unafuu kwa wananchi, tusiseme elimu bure. Kwa sababu leo utasema elimu bure lakini Serikali Kuu mnasema Halmashauri ndiyo ijenge maboma, ihangaike kupata madawati lakini hazina uwezo. Kwa mfano kwangu Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI pitia uone, kadri tunavyozidi kwenda mbele Halmshauri ya Mji wa Tarime kwa mwaka huu unaomalizika makusanyo ni shilingi milioni 300. Leo Halmashauri hiyo ijenge maboma ya shule za msingi za Tarime, ipeleke madawati na afanye na mambo mengine kwa fedha zipi? Walau mlitoa Waraka Na.5 wananchi walikuwa wameshaanza kujitolea mara tena Rais Magufuli akasema usichange labda upate kibali, wameacha, watoto wetu wanakosa mahali pa kusomea. Kama mnataka kutoa elimu bure jipangeni tunahitaji madarasa ya kutosha watoto wa Kitanzania wasome. Leo ukienda Tarime watoto zaidi ya 200 kwenye darasa, madarasa yenyewe hayapo. Walimu wanakaa kwenye miti, Tarime Mjini pale ofisi inatazamana na ofisi ya Chama cha Mapinduzi, walimu ofisi zao ni miti. Halafu mnakuja mnasema elimu ni bure. Mheshimiwa Cecilia Paresso hapa kasema *do you have seven hundred billions* kuweza kufanya elimu bure i-*take off*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hamna madawati, hamna madarasa, Sera ya Elimu inasema walau watoto 45 kwa darasa moja wanakaa zaidi ya 200. Walimu wenyewe hawawi-*motivated*, hawana nyumba, umesema umejenga nyumba 183; sijui 188 kwa sekondari, mimi najiuliza mwalimu apange mjini, achukue sijui ni pikipiki au gari aende kufundisha Kenyamanyori hiyo fedha ni ya kwake kwenye kamshahara kale unakompa hana *motivation allowance* yoyote ile halafu mtasema elimu bure inaenda kuwa elimu ambayo haina manufaa yaani bora amefika la saba au la kumi na mbili lakini anarudi kitaa hajapata elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mtu afanye kazi vizuri lazima walau ufanye akili yake itulie yake, mwalimu anayekwenda kumfundisha mwanafunzi ni lazima awe ametuliza akili. Mwalimu hana nyumba na wenye vinyumba vyenyewe wakikaa wananyeshewa nilisema mwaka jana hapa, shule ya sekondari nyumba zao zinavuja wanahamisha vigodoro huku na huku halafu leo useme kwamba watoto wale wa maskini watafundishwa waelewe, hata siku moja. Tuwe na vitabu vya kutosha, tuwe na madawati, tuwe na madarasa ya kuweza kuhakikisha wanafunzi wanakaa walau 45 ili mimi mwalimu ninavyofundisha waweze kunielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye afya. Sera ya Afya inasema walau kila kijiji au mtaa wawe na zahanati, mmeonyesha mna zahanati 4,500 tangu uhuru mpaka sasa hivi bado kuna upungufu wa zahanati 8,043. Vituo vya afya mnavyo 488 upungufu wa 3,506 na mnajua Maazimio ya Abuja walau asilimia 15 ya bajeti ya Serikali iende kwenye afya tumekuwa tukiimba, *you*

don't do that. Leo mnasema mnaboresha afya, kama imewachukua miaka 50 tuna vituo vya afya 484 itatuchukuwa zaidi ya miaka 350 kutimiza hivi vituo vya afya vinavyohitajika, watu wetu wanakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kwa Tarime kuna Zahanati ya Gamasara ambayo iko Kata ya Nyandoto inahudumia wananchi wa Kata ya Nyandoto kama kituo cha afya wakati ni zahanati, inahudumia wananchi wa kijiji cha Kongo na Ketere hiyo ni Wilaya ya Rorya na inahudumia wananchi wa Kewamamba na Nyagisya hiyo ni Halmashauri ya Wilaya ya Tarime (Jimbo la Vijijini). Zamani walau mlikuwa mnapeleka shilingi milioni nne kwenye Halmashauri ya Mji leo mnapeleka shilingi166,000 baada ya miezi mitatu, hawa Watanzania tunawapenda au tunachezea afya zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije tena kwenye Hospitali ya Mji ambayo mliishusha hadhi kutoka Hospitali ya Wilaya mkaifanya Hospitali ya Mji na niliuza swali hapa nikasema ilitakiwa iwe Hospitali ya Rufaa maana inasaidia wananchi wa Rorya, Serengeti na Tarime kwa ujumla siyo mji tu, mnapeleka ruzuku ya shilingi milioni 51 halafu Halmashauri ya Wilaya ya Tarime mnapeleka shilingi milioni 91 wakati mkijua kabisa kwamba ile Hospitali ya Mji iliyoko mjini inahudumia huko kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi milioni 51 iweze kutibu Wilaya nzima maana kiuhalisia haitibu wananchi wa Mji wa Tarime tu. Ndiyo maana nasema hivi mna watendaji na watu wenu wanafanya kazi ku-*check* uhalisia? Halmashauri ya Wilaya ya Tarime haina hospitali, wanakuja kutibiwa kwenye Halmashauri ya Mji wa Tarime, kwa nini mnaweka *allocation* za kitoto namna hii? Mnachezea afya za Watanzania, tunaendelea kushuhudia wananchi wakifa, waoneeni huruma. Nipeni mwanga maana sioni na mniongezee dakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo. Halmahsuri ya Mji wa Tarime tuna *Mogabiri Extension Farm*...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Nitachangia siku nyingine kwenye Wizara zingine, nina nondo nyingi sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah atafuatia Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege na Mheshimiwa Masoud Suleiman Nchambi.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kusimama hapa. Pia

nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Leo nitakuwa na mada mbili tu kuhusu Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na nitaongelea masuala ya ajira pamoja na utawala bora.

Tatizo kubwa la watumishi wetu ni maslahi yao na siyo maslahi yao tu lakini pia ni kujengewa uwezo wa kazi zao. Wafanyakazi wanalipwa mshahara ambao haulingani na maisha ya sasa. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri alisema mwaka 2010 uliongezwa mshahara kwa asilimia 13.2 tatizo siyo kuongeza tu mshahara, je, mshahara unakidhi mahitaji ya lazima ya mfanyakazi, hilo ndilo swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mshahara wanaolipwa, kiwango cha chini ni kuanzia shilingi 300,000 au 400,000 kwa wafanyakazi mbalimbali haufiki hata wiki moja. Wafanyakazi ambao wanautumia muda wao kuanzia saa moja mpaka saa tisa na anafika nyumbani saa kumi na moja afanye nini, hizi wiki tatu atafute wapi fedha za kuweza kuendesha maisha ya lazima, mfanyakazi huyo atatafuta njia ya kuweza kujisaidia. Nasema kwamba mtatumbua majipu mpaka mtatumbuana wenyewe kwa wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia watumishi ambao wanaondoka nchini na kwenda nchi za nje, Mheshimiwa Waziri hakuligusia suala hili katika hotuba yake. Tuna wataalam ambao tunawasomesha kwa fedha za umma ambao wanahitajika katika nchi, lakini baada ya kufundishwa na kupewa utaalam wa kutosha wanaondoka kwenda kujenga Taifa lingine. Ni vizuri Mheshimiwa Waziri uangalie upya suala hili ili uhakikishe watumishi hawa ambao ni wataalam wanajengewa vivutio ili kuwawezesha kuishi na kufanya kazi katika Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni upungufu wa wafanyakazi. Kuna malalamiko kwamba zaidi ya wafanyakazi 16,443 na wale wa wakala 2,552 bado wanahitajika. Huwezi kutoa *service* kama hakuna wafanyakazi. Uchumi unajengwa kwa watu kufanya kazi. Leo nguvu kazi, rasilimali watu zaidi ya 16,000 ukiongeza na 2,500 *almost* 18,000 na zaidi wanahitajika, leo Waziri anasema anakwenda kufanya mchakato. Hapa hakuna haja ya kufanya mchakato, nenda kafanye mchakato katika Wizara yako utuambie ni lini utaajiri watu hawa waweze kufanya kazi katika Wizara na sehemu nyingine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja katika utawala bora. Ninavyofahamu mimi utawala bora ni msingi mkubwa wa kuendesha Taifa. Utawala bora kama utausimamia vizuri hakuna haja ya kuhangaika kutumia nguvu, utawala bora unagusa kila maeneo ya nchi, kila mwananchi, kila kiongozi na kila mfanyakazi. Utawala bora ni kuheshimu Katiba na sheria ya nchi na ni kuheshimu demokrasia. Utawala bora ni kuheshimu utawala wa sheria na utawala bora ni

kusimamia misingi mikuu ya uchumi na kuleta maendeleo ya Taifa. Utawala bora ni kusimamia haki na usawa na uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni kwa nini tunapata kazi kubwa ya kupambana na watu kwa nini tusitumie nyenzo kuu ya utawala bora kujenga misingi mizuri ya kuendesha Taifa hili? Kwa vyovyote vile kama hatutadumisha utawala bora tutazorotesha uchumi na maendeleo ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba ni vizuri tuige kwa wale viongozi waliopita ili tujifunze walifanya nini. Kwa mfano, ukiangalia Waraka wa Programu ya Pamoja *(Joint Program Documents),* Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa William Benjamin Mkapa alichukua suala la utawala bora kama mhimili mkuu wa utawala wake katika Urais wake. Mnamo mwaka 1999 alijenga mazingira ya nidhamu ili kuweza kurekebisha masuala ya uchumi na kuweza kuleta maendeleo ya Taifa. Sera na mabadiliko yalikuwa ndiyo nguzo kuu ya mwelekeo pamoja na kuhakikisha kwamba utawala bora ndiyo dira ya Taifa. Kwa kufanya hivyo, aliweza kubadili mfumo wa dola ya Afrika katika nchi zile za Jangwa la Sahara. Matokeo yake aliweza kualikwa na *World Bank* kuweza kutoa hotuba ni kwa vipi ameweza kubadili masuala ya uchumi na utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kutenda haki na kuleta uchumi wa nchi hii hakuna haja ya kutumbuana majipu kwa nguvu. Silaha yetu tuliyonayo ni utawala bora, kila mtu atawajibika kwa nafasi yake. Rais atawajibika kwa nafasi yake, Waziri atawajibika kwa nafasi yake na Wizara mbalimbali zitawajibika kwa nafasi zao. Tanzania leo kwa kukosa haya niliyosema ni nchi ya 51 ambayo inakosa sifa za utawala bora katika nchi 72 na itaendelea kuwa chini kwa sababu misingi ya utawala bora imekiukwa, wanawekwa Mashehe ndani bila kosa. Watu wa aina hii hawataweza kuleta maslahi yoyote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kimenishangaza tena sana na nitaendelea kushangaa ni Waziri anayehusika na Utawala Bora anasimama mbele ya Bunge kupongeza utawala haramu uliovunja Katiba ya nchi hii, hili ni tatizo kubwa. Zanzibar wamenyang'anywa haki yao, Waziri anakuja hapa mbele ya Bunge kusifu uvunjaji wa Katiba ya nchi, kunyang'anya demokrasia ya Wazanzibari, hili halikubaliki. Nasema Zanzibar itendewe haki yake na kamwe haki haikai chini, itakaa juu na mapambano yanaendelea hatuko kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili limetoa sura mbaya kwa Taifa na sura mbaya kwa Mataifa. Kukandamiza demokrasia ya wananchi ambao wamemchagua Rais wao waliomtaka na kuvunja Katiba na hatimaye kusaidiwa kupelekwa majeshi na zana nzito katika Visiwa vya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanzazibar wameumia sana, lakini dhuluma haidumu, yana mwisho, kila kitu kitaonekana. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu haki itaonekana ilikiukwa wapi. Asilimia 51.8 hawaitambui Serikali ya Shein, Serikali haramu, Serikali batili kabisa, tunasema waziwazi na tuna ushahidi wa kutosha kabisa. *(Makofi)*

KUHUSU UTARATIBU

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu Utaratibu.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana…

MWENYEKITI: Hapana, sema kifungu kwanza.

MBUNGE FULANI: Kifungu cha 63(3).

MWENYEKITI: Soma sasa.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 63 (3)…

WABUNGE FULANI: Kwa sababu ya muda endelea.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, msemaji aliyepita anazungumzia suala ambalo halipo. Anasema watu wa Zanzibar hawaitambui Serikali yao, hili suala ni la uongo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge aliyezungumza aweze kurekebisha kauli yake au hatua nyingine ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tupo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ulisimama vizuri sana kwa saula la utaratibu maana linahusu Kanuni na linachukua kipaumbele kwa shughuli yote ndiyo maana nilitaka utusaidie. Hiyo Kanuni ya 63(3), suala Kuhusu Utaratibu nikikuruhusu kama nilivyofanya ulipaswa sasa utoe maelezo ya kutosha kuonyesha kwamba anachokisema si sahihi. *(Makofi)*

Hata hivyo, mimi kama kiongozi wenu na pia kwa kufahamu masuala ya sharia, nafahamu kabisa Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein ni Rais wa Zanzibar. Yawezekana miongoni mwetu tukaona kwamba hakufika hapo kihalali ni maoni yao, lakini sisi tunaolinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambapo na Katiba ya Zanzibar inatajwa katika Katiba hiyo, lazima tuheshimu mamlaka iliyo kuu. Nisingependa Waheshimiwa Wabunge tuanze malumbano

ambayo hayatakuwa na tija kwa shughuli iliyo mbele yetu. Nawasihi sana twende katika njia kuu iliyonyooka na tutafika vizuri tu. Ahsanteni, tunaendelea. *(Makofi)*

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasihi Waheshimiwa Wabunge wasome Katiba, hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nenda Sura ya Nne ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utaona kwa nini Zanzibar inazungumzwa. Hakuna hata mmoja aliyekuwa hajui, akiwa mtoto, mtu mzima na wanyama wanajua ukweli uko wapi na ukweli utaendelea kujulikana uko wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia niseme kwamba msaidieni Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba *aspect* 22 za utawala bora anazifuata vizuri. *(Makofi)*

Narudia, msaidieni Mheshimiwa Rais aangalie *aspect* 22 za utawala bora anazitekeleza. Hakuna haja ya kutumbua majipu, hakuna haja ya fujo, uongozi si mabavu, mabavu yamepitwa na wakati. Mabavu ya Rais ni kufuata Kanuni na utaratibu wa utawala bora, basi! Utawala bora umejengeka katika Wizara zote hata vijijini, nadhani tukifanya hivyo haki itatendeka. Hakuna amani bila ya haki. Kama mtu unamnyang'anya haki yake na ananyamaza kimya hana imani huyo na imani haipo. Ni kama ilivyo Zanzibar, Zanzibar hakuna amani. Amani siyo kupigana kwa mtutu wa bunduki, amani ni ndani ya roho yako. Ukiwa huna amani ndani ya roho yako ndiyo unaanza kufanya mashambulizi. Kwa hiyo, nasema Zanzibar hakuna amani, tunasema waziwazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Nina tangazo fupi sana kabla sijamuita Mheshimiwa Kandege.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, anaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo kutoka Chama cha Mapinduzi mkutane kwa muda mfupi sana pale Ukumbi wa Msekwa.

Tunaendelea, Mheshimiwa Kandege atafuatiwa na Mheshimiwa Nchambi.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi jioni ya leo hii niwe miongoni mwa wachangiaji wako. Awali ya yote, nalazimika kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama leo nikiwa na nguvu ya kutosha na afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana wananchi wa Kalambo, nuru mpya Kalambo ambayo tumeiahidi tutaitimiza na hasa kwa kasi hii kila mtu ana kila sababu ya kuunga mkono Serikali inayoongozwa na Rais, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. Kubeza ni kama namna tu ambavyo mtu ambaye ameanza safari unamwambia ongeza *speed*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu najielekeza katika suala zima la bajeti ya mikoa. Nashindwa kuelewa kama hili limekuwa likitokea kwa bahati mbaya au ni katika *design* ambayo imewekwa. Ukipitia katika *budget allocation,* ukienda Mkoa wa Katavi, kupitia TAMISEMI wametengewa shilingi bilioni 3.9, unaujumlisha na Mkoa wa Lindi shilingi bilioni 6.1, unakwenda Mtwara na ya Mtwara imeongezeka hivi karibuni na sababu zinaweza zikawa zinapatikana lakini ni shilingi 10.7, ukienda Mkoa wa Rukwa ni shilingi bilioni 6.7, inawezekana pia hawakujua na Shinyanga nayo imetengewa kidogo…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kandege, ni kitabu kipi hicho unachotumia?

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki hapa.

(Hapa Mheshimiwa Josephat S. Kandege
Alionyesha Kitabu anachotumia)

MWENYEKITI: Sawa, ili wote tuwe pamoja.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Ndiyo, maana ndiyo bajeti, hii nyingine ni porojo, sisi tunataka twende kwenye *facts. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shinyanga imetengewa shilingi bilioni 9.2 na Singida ni shilingi bilioni 9 ukijumlisha mikoa yote hiyo na ukija ukilinganisha na hii yote na ukajumlisha Mkoa wa Manyara ambao ulikuwa sehemu ya Mkoa wa Arusha, mikoa hii miwili wametengewa jumla ya shilingi bilioni 38.3. Jumlisha pesa ya mikoa yote hiyo niliyotangulia kuitaja haifikii pesa ambayo imetengwa kwa ajili ya mikoa miwili na mikoa ambayo ilikuwa mkoa mmoja. Hili nimekuwa nikilisema, ifike mahali ambapo sasa Serikali ituelewe, haiwezekani ile mikoa ambayo tunasema iko nyuma kiuchumi ambayo haijaendelea, hiyo ndiyo ambayo iendelee kutengewa bajeti ndogo, hatuwezi kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya hawa ambao wanapata 27, hebu katafute kura, katafute jinsi gani ambavyo wanaitambua Serikali iliyopo madarakani kaangalie wametoa kura kiasi gani? Inawezekana kuna wataalam ambao wametangulia wako huko waka-*design formula* ambayo watahakikisha daima wao ndiyo wanapata pesa nyingi katika mikoa yao. Jambo hili halikubaliki! Tunaomba Serikali ituambie ni utaratibu gani ambao wanautumia katika *budget allocation*. Haiwezekani ambaye yuko nyuma useme ataendelea

kuwa nyuma daima dumu. Hii nchi ya kwetu sote, keki kama ndogo tugawane kwa usawa. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Ndiyo, haiwezekani.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi imekuwa ikisikika kwa wale ambao imegawanywa mikoa na Wilaya, Wilaya zingine zinafanana na kata zangu mbili, ukiwaambia kwamba na sisi tunaomba tuongezewe mgao wanasema hapana, huu ni ulaji lakini ni kwa sababu tayari wao ukubwa wa Wilaya ni sawasawa na kata zangu mbili. Mtu kama huyu ukimwambia kwamba Serikali iendelee kugatua madaraka kupeleka huko chini hawezi kuelewa kwa sababu tayari yeye alishatosheka. Naomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, nimetoa *sample* tu ya hiyo mikoa na iko kwenye kitabu hiki. Wakati unakuja kuhitimisha ni vizuri ukatuambia *formula* gani ambayo inatumika katika kugawanya keki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niseme jambo ambalo limekuwa likinitia simanzi. Katika mikoa yote Tanzania, ukiachia hii ambayo ndiyo imeanza hivi juzi, Mkoa wa Rukwa ndiyo mkoa pekee kwa taarifa nilizonazo ambao hauna Chuo cha Ufundi kwa maana ya *VETA*. Kwa hiyo, naomba Serikali hii ili sisi tusilazimike kukimbilia huko ambako kuna vyuo, kupitia Wizara zote kwa namna mtakavyoweza kujikusanya ujenzi wa *VETA* Rukwa iwe miongoni mwa vipaumbele. Kwa sisi Kalambo tayari tulishatenga eneo na tunafuata ramani ili tuanze ujenzi tukiamini kwamba Serikali nayo itatuunga mkono hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi na kwa bajeti finyu kama hii ambayo umeiona kupitia TAMISEMI hali kadhalika hatuna Hospitali ya Wilaya. Niiombe Serikali, huko ambako mlishapeleka vinatosha, sasa hivi tuelekeze nguvu maeneo ambayo tunaita *peripherals* ili wananchi wakienda sehemu zote za Tanzania wasijione ukiwa kwamba ukifika maeneo fulani inakuwa kama vile haupo Tanzania. Niiombe Serikali, bado hatujachelewa, naona Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko pale ana-*take note*, Mikoa yote ambayo ni *under privileged* ipewe kipaumbele tuhakikishe kwamba inapata *allocation* ya fedha ya kutosha na wananchi wako tayari kuiunga Serikali yao mkono si tena kwa hila bali kwa upendo wa dhati kutoka moyoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niyaseme machache ili yachukuliwe kwa uzito niliotaka ufike, kimsingi naunga mkono bajeti. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Zungu kama yupo.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na pia namshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono bajeti hii ya Wizara ya TAMISEMI kwa asilimia mia moja. Nina hakika kwa Mawaziri hawa na usimamizi mzuri utakaofanywa wataweza kufanikiwa kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kupongeza Serikali kwa kuweza kuingia mkataba na Serikali ya China kujenga reli ya kati nchini mwetu. Hili jambo sio la mchezo. Kwanza tumeweka pesa zetu, wadau wa nje wakashawishika na wao kuleta pesa zao kwa asilimia zaidi ya mia moja. Napongeza sana jitihada zilizofanywa na Mheshimiwa Magufuli pamoja na Serikali yote na Waziri Mkuu kwa namna reli hii itakavyojengwa. Reli hii ita-*capture* biashara katika nchi nyingi sana ambazo zinatuzunguka. Uwezo wa reli hii kubeba mizigo ni zaidi ya tani milioni kumi kwa mwaka. Reli hii katika kipindi cha miaka saba mpaka kumi gharama zote za deni zitalipwa. Kwa hiyo, naomba tuendeleze amani, amani za majirani zetu ndiyo amani yetu sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto za elimu bure ambapo ni kazi yetu kuzifanyia kazi ili tuzimalize. Suala la madawati si suala la Serikali peke yake, ni suala letu sisi wote, wa vyama vyote vilivyoko nchini mwetu. Tushirikiane na Serikali yetu tutafute njia mbadala. Watoto hawa ni wetu, mtoto wa mwenzio ni wako. Kwa hiyo, suala la elimu bure na hii changamoto ya madawati tuisaidie Serikali, tuje na hoja *positive* za kuisaidia Serikali iweze kutatua tatizo hili na changamoto hii iishe ili watoto hawa waweze kusoma na nchi yetu iweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mchango mkubwa kama kawaida yangu, nazungumzia Benki ya Wananchi ya Dar es Salaam *(Dar es Salaam Community Bank)*. Benki hii imeanzishwa kwa mtaji wa Halmashauri nne, Halmashauri za Manispaa ya Ilala, Kinondoni, Temeke na Jiji la Dar es Salaam. Tume-*sacrifice* miradi yetu kuweka mtaji kuanzisha benki hii. Hawa watendaji wa sasa hivi walikuwa wanakuja pale Jiji mikono nyuma wanaomba kazi. Baada ya Halmashauri hizi nne kujinyima kwenye vyanzo vyake, tumewanyima wananchi wetu mikopo kwa kutegemea benki hii sasa iwe chombo cha kusaidia wakazi wetu kuwakopesha ili na wao wanyanyue maisha yao. Asilimia kubwa ya mtaji wa benki hii imefanywa na wananchi wa Dar es Salaam wenyewe kupitia kwenye Halmashauri zao. Ni wanyonge ndiyo waliochangia benki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini habari ya benki hii baada ya wataalam hawa kuingia, baada ya ya benki kusimama kwa hela za wananchi wa Dar es Salaam wenyewe ikiwa kama ndiyo mchango wa kwanza, wameanza kutuingiza katika masuala ya *financial regulations*, kuna masuala ya mitaji na

kipindi kile walisaidiwa wakaanza kutu-*dilute*. Mtaji wetu sasa hivi wa Halmashauri hizi nne umeshuka mpaka sasa ni asilimia tisa. Wametutoa kwenye umiliki wa benki hii mpaka kutufanya sasa ni watu wa chini kabisa wa benki hii. Benki hii ilifanya mambo haya kwa kutumia vigezo vya mitaji ambayo Halmashauri na uwezo mdogo wa watu kuelewa masuala ya *financial services* na *banking* zilivyo hawakuelewa na kila mwezi kila kwenye mikutano mikuu tukanza kushushwa mpaka sasa hivi hatuna mali, hatuna chochote kwenye benki hii. *(Makofi)*

Naiomba Serikali Mheshimiwa Waziri na wewe ni mtaalamu wa majipu, tunataka benki hii ifanyiwe uchunguzi, tunataka benki hii iende kwa CAG ili sasa hatma na heshima ya wananchi na Halmashauri hizi nne za Dar es Salaam zirudi kumiliki benki hii kama tulivyoianzisha. Haiwezekani wenye mtaji, watu maskini wanyang'anywe benki hii, ni dhambi kubwa sana ambayo imefanywa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri ulichukue hili, kwa vile benki hii imechangiwa na Halmashauri zako, naomba sasa lifanyie kazi ili tuweze kuimiliki benki hii na kuichukua tena iwe mali ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya machache, naunga mkono hoja. Kama kawaida yangu mimi huwa nasema kidogo lakini nasema makubwa. Nakushukuru na nina-*save* muda ili wengine nao waweze kuchangia. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nashukuru sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu atafuatiwa na Mheshimiwa Kiswaga Boniventura Destery na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah ajiandae. Naona Mheshimiwa Dkt. Kafumu hayupo tunaendelea na Mheshimiwa Kiswaga.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu anayeneemesha neema nyingi nami akanineemesha neema ya kuwa Mbunge wa Jimbo la Magu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze hotuba za Waheshimiwa Mawaziri wote wawili kwa kadri zilivyojielekeza kuhudumia na kutatua kero za wananchi. Nianze na eneo la elimu bure. Safari moja huanzisha nyingine, tumeanza, pamoja na changamoto, inapaswa sasa kama Serikali ione namna ambavyo itaongeza fedha hizi ili ziweze kukidhi mahitaji ya uendeshaji wa shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati suala hili la MEM linaanza 2002 *capitation* tulikuwa tunapeleka dola kumi kwa kila mwanafunzi. Wakati huo *exchange rate* ilikuwa ni shilingi1000 leo ni shilingi 2000. Maana yake kwamba ili zitosheleze lazima tupeleke mara mbili. Naishauri Serikali iweze kuliona hili ili iweze kuongeza kiwango hiki kinachotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bure chekechea hadi kidato cha nne ni sahihi. Mimi najiuliza hivi mtoto wa maskini huyu anapofika kidato cha tano anatajirika? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Hapana.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iangalie kwa upana wake hata kama siyo bajeti hii, bajeti ijayo iweze kuwaangalia watoto hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye jambo la maji, maji ni hitaji la kila mmoja wetu tulioko mahali hapa. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji alitembelea Wilaya yangu ya Magu kwa kweli alinitendea haki na Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Serikali ijielekeze kuhakikisha kwamba wale ambao tunazungukwa na Ziwa Victoria tunapata maji ya kutosha na wengine ambao wanazungukwa na Ziwa Tanganyika nao wapate maji ya kutosha. Haiwezekani watu tunasimama tunaliangalia ziwa lakini maji hatuna, hamtutendei haki.

Naishauri Serikali hii iangalie kwa sababu uchumi wa nchi hii wachangiaji wakubwa ni akina mama lakini inapofika saa tisa za usiku akina mama wanaondoka kwenda kutafuta maji. Ninapotembelea vijiji vyangu wanalalamika wanasema hata watoto asubuhi hawawaoni hawa akina mama. Naomba sana Serikali iangalie hata kama ni kukopa kwenye mifuko ya fedha tuwekeze kwenye maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishati. Namshukuru sana Naibu Waziri wa Nishati na Madini alitembelea Jimbo langu, tukatembea naye siku moja vijiji kumi, alinitendea haki Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uchumi ukue umeme unahitajika kila mahali. Tunapozungumzia viwanda vidogo wakati mahali ambapo vinahitajika viwanda hivi vijengwe umeme haupo. Niombe Serikali kwa jitihada ilizonazo kupitia *REA Phase II* na *III* tuweze kukamilisha vijiji vyote kwa kuvipatia umeme. *(Makofi)*

Naomba nizungumzie afya. Hotuba ya Waziri inasema vijiji 8,043 havina zahanati. Wewe ni shahidi kwenye vijiji vyako Jimbo la Bariadi ni vijiji vikubwa sana ukizingatia na Jimbo langu la Magu nalo lina vijiji vikubwa, kuondoka kijiji kimoja kufuata huduma ya afya kijiji kingine unachukua kilometa 15 na hakuna hata zahanati za *private,* hakuna hata maduka ya dawa. Niishauri Serikali kwa sababu wananchi wa Wilaya ya Magu wameanzisha maboma ya kutosha ya

zahanati tupewe fedha za kukamilisha zahanati hizo ili wananchi waweze kupata huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la viongozi wa kisiasa kwa maana ya Wenyeviti wa Vitongoji, Wenyeviti wa Vijiji na Waheshimiwa Madiwani. Katika uongozi mgumu duniani sijui dunia au Tanzania hii, hakuna uongozi mgumu kama Mwenyekiti wa Kitongoji, Mwenyekiti wa Kijiji na Mheshimiwa Diwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa lazima tuelewane vizuri na naomba Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu kuna kipengele kwenye viapo vyenu kinasema utamshauri Mheshimiwa Rais kwa hekima, hapa ndipo mnatakiwa mumshauri kwa hekima. Mwenyekiti wa Kitongoji yeye ndiye anayefanikisha ujenzi wa madarasa, ujenzi wa zahanati na vitu vyote vilivyoko kule. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kitongoji leo mwananchi akikamatwa mahali popote yeye ndiye anayekwenda kuandika dhamana adhaminiwe, huyu ni mtu muhimu sana. Mimi leo nikitaka kufanya ziara yeye lazima aweko. Naomba Serikali tuelewane iweke siyo fedha nyingi, tuanze na za kuanzia ili hawa watu waweze kupata posho zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mheshimiwa Diwani mimi nimetokea huko niseme tu kwamba hawa watu ndiyo walionileta hapa kwamba tumpeleke mwenzetu anayetufahamu. Diwani aliyefanikiwa kuwa na gari halali usiku kucha gari yake ndiyo *ambulance* kupeleka wagonjwa hospitali. Leo maslahi yake tunayaona kama yanatosha hayatoshi. Niombe sana wasaidieni watu hawa na ndiyo wanaojenga siasa kwenye maeneo yetu, ni Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji na Madiwani. Naomba tuelewane vizuri hapa katika bajeti hii au bajeti ijayo. *(Makofi)*

Niendelee kusema kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano ndiyo ambayo wananchi walikuwa wakiingoja, ni Serikali shupavu, Serikali ya kazi tu. Mwaka fulani Mheshimiwa Rais Nyerere alitangaza Kilimo cha Kufa na Kupona, Rais Magufuli ametangaza kazi ya kufa na kupona, huyo lazima tumpongeze. Wale wanaobeza ni mioyo ambayo haina shukurani. Maandiko Matakatifu yanasema mioyo ambayo haina shukurani hukausha mema mengi. Naiomba Serikali hii ya Awamu ya Tano, wale watu ambao hawashukuru ikaushe miradi ya maendeleo isipeleke kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu aombaye hupewa, huwezi kuwa unasimama unatukana Serikali inayokujali halafu unapewa miradi. Naomba Serikali hii isiwape miradi watu hawa ambao hawana shukurani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikuwa wakisema Serikali hii haina meno, Serikali imeanza kutumbua majipu wao wanakuwa mawakala wa wale waliotumbuliwa. *(Makofi)*

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Haiwezekani, tuipe heshima Serikali iweze kufanya kazi.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Naomba tunapopanga miradi hii isimamiwe…

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Na Wizara ili tuweze kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

MHE. ESTHER N. MATIKO: Fedha za maendeleo ni kodi ya Watanzania, njuka wewe.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea.

MBUNGE FULANI: Kasemaje?

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Masala na Mheshimiwa Aeshi Hilaly ajiandae.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichangie machache katika bajeti hizi za Wizara mbili. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia jioni hii ya leo kusimama katika Bunge hili na kuchangia bajeti iliyoko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kuhusu ufinyu wa bajeti. Takribani Wizara zote katika bajeti hii zimekabiliwa na ufinyu mkubwa wa bajeti. Kwa hiyo, ni vyema Serikali katika vyanzo vyake vya mapato vilivyopo na vile ambavyo inaendelea kuvibuni siku hadi siku ndani ya bajeti hii iweze kufikiria Wizara tofauti tofauti, hizi tunazozijadili na kuwaongezea ili ziwe na bajeti za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua majukumu waliyonayo Wizara hizi lakini pia nataka nijikite katika Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma pamoja

na ile Tume ya Ajira. Tume hizi zimekuwa zikifanya kazi kwa nguvu zote kwa maslahi ya wananchi na viongozi wa umma walioko katika nchi hii. Tume hizi zimekuwa zikikabiliwa na ufinyu wa bajeti mkubwa na zaidi majengo au ofisi wanazofanyia kazi ni za kupangisha kwa bei ya juu. Vitendea kazi vya kutosha hawana na ukiangalia bajeti yao ilivyo na ukiangalia mahitaji ya fedha ambazo zinatakiwa kulipwa kwa ajili ya ofisi wanazofanyia kazi basi utashangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunatembelea ofisi hizi, kuna Mheshimiwa mmoja wakati wanatoa changamoto zao alijitolea kuchangia kompyuta pamoja na vifaa vyake. Hii ni aibu jamani, sisi tunakwenda kule kuwapa ushauri na mambo mengine lakini pia sisi sio watu wa kuchangia vifaa vya ofisi hizi wakati ofisi hizi ni muhimu sana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma imekuwa ikifanya kazi kwa nguvu zote, lakini pia cha kusikitisha bajeti yake yote ikiwemo mishahara ya watumishi ni ufadhili kutoka nje, inasikitisha sana. Ni vema Serikali ikajitahidi na ikajikita katika suala la kuongeza bajeti katika ofisi hizi. Mara nyingi tumekuwa tukiwalaumu, tukiwakosoa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwamba hawatekelezi majukumu yao lakini kumbe hawana bajeti, hawana ofisi ya kufanyia kazi, wana-*share* ndani ya ofisi, wanakaa nje, hawana sehemu nzuri za kufanyia kazi, hawana vifaa vya kutosha lakini pia yote haya yanatokana na ufinyu wa bajeti unaozikumba ofisi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niende moja kwa moja katika mikoa na Halmashauri husika. Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wamechangia na kusema kwamba asilimia 30 ya kodi ya majengo ndani ya Halmashauri hazirejeshwi. Wanajitahidi kukusanya kodi hizi lakini pia mrejesho unakuwa hauwafikii. Serikali imewapangia makusanyo kupitia vyanzo vyao vya mapato asilimia 30 kwa mujibu wa bajeti na Halmashauri zimekuwa zikijitahidi sana kukusanya lakini leo kutokana na kuwa hawana mrejesho katika makusanyo kama haya au kodi hizi kwa hiyo imefikia hatua hawawezi kutumia au hawawezi kufaidika na fedha hizi. Pia Halmashauri zetu zina upungufu wa Maafisa Ugani, zina upungufu wa wataalam wa kilimo na hakuna watafiti wa kilimo. Kwa hiyo, ni vyema tukazipa uhuru Halmashauri hizi ili ziweze kujitegemea na kile wanachokikusanya pia tusiwabane sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuweka mfumo sahihi wa matumizi ya *electronic* kwa kusambaza vifaa vya *electronic* katika Halmashauri zote ili kuhakikisha kwamba mapato ndani ya Halmashauri hayawezi kuvuja. Yote yanatokana na kuwa hakuna mashine za *electronic* na ndiyo maana tukaona mapato yanapotea siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la wastaafu. Mara nyingi wastaafu wamekuwa wakiilalamikia Serikali kwamba wanapata usumbufu mkubwa katika kufuatilia haki zao. Baadhi ya changamoto wanazozieleza wastaafu moja ni kutokana na kuwa waajiri hawatekelezi wajibu wao kwa wale wafanyakazi ambao wamejiunga na Mifuko ya Hifadhi jamii ambapo wanakuwa hawafikishi fedha zile mpaka inafikia mfanyakazi anafikia kustaaafu. Pia kuna tatizo la kuchelewa kufikisha nyaraka Hazina. Yote haya inawasababishia wastaafu kuchelewa kupata haki zao na kuja kupata usumbufu baada ya kustaafu. Niiombe sana Serikali kuwafikiria kwanza wastaafu hawa au wastaafu watarajiwa na kuwaomba hizi ofisi kwamba itakapofikia mtu karibu na kustaafu ndani ya miezi mitatu kabla basi nyaraka ziweze kufikishwa mapema kunakohusika ili wastaafu hawa itakapofikia kustaafu waweze kufaidika na wasipate usumbufu. *(Makofi)*

Kuhusiana na suala la MKURABITA, niipongeze sana Serikali kwa jitihada zake za kufanikisha na suala hili. Pia nitoe pongezi kwamba imeenea katika maeneo mengi Tanzania Bara na kule Zanzibar, wengi wameweza kupimiwa maeneo yao na kupata hati miliki za kimila. Pia niombe sana Serikali kupitia hati hizi za kimila kwa vile tumefungua Benki ya Kilimo wananchi waruhusiwe kuzitumia kama dhamana pale wanapohitaji mikopo kwa ajili ya kuendeleza kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye *TASAF*, mfuko huu ni muhimu sana katika Taifa letu lakini cha kusikitisha pamoja na kazi kubwa inayofanywa lakini pia jamii ni pamoja na wananchi waliotuzunguka katika Majimbo yetu. Sisi Wabunge mara nyingi hatujui nini mfuko unafanya wala kushirikishwa maendeleo yanayopatikana na hata tukihoji basi inakuwa ni kazi ngumu kupata majibu. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali iwashirikishe Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wawe wa Viti Maalum au wa Majimbo katika maeneo wanayotoka kushirikishwa kwa miradi yote na kwa namna yoyote au hata katika Kamati za *TASAF* zinazopanga utaratibu mzima kuhusiana na masuala yale ya kijamii na uwezeshaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Anafuata Mheshimiwa Masala badaye Mheshimiwa Aeshi Hilali.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Mwenyekiti…

MHE. KHALIFAN H. AESHI: Chikawe ni mimi.

MBUNGE FULANI: Hapana ni Masala halafu baadaye wewe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masala.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko Mezani. Kabla ya kuendelea mbele naomba nijumuike na wenzangu waliotangulia kutoa shukrani lakini pia kutoa neno la pongezi kwa Serikali yetu ya Awamu ya Tano ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Magufuli kwa kazi kubwa na kazi nzuri ambayo imekuwa inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote wa Wizara zote mbili kwa uwasilishaji mzuri na yale waliyoyawasilisha ambayo leo hii tunayajadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie maeneo makubwa yasiyopungua matano lakini nitajielekeza zaidi katika Jimbo ambalo natokea la Nachingwea, lakini wakati huo huo tutakwenda kuangalia namna gani ambavyo yana-*reflect* Taifa kwa ujumla katika kuhakikisha tunasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ambalo napenda kuchangia ni elimu. Katika Jimbo la Nachingwea na kwa ukongwe wa Wilaya ya Nachingwea tuna kazi kubwa ambayo tunatakiwa tuendelee kuifanya pamoja na jitihada ambazo Serikali imeendelea kuzifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kwenye suala la elimu bure ambayo imeanza kutolewa mwaka huu ni jambo ambalo limepokelewa vizuri sana na wananchi wa Jimbo langu la Nachingwea. Nimefanya ziara katika kata zangu zote 34, maeneo yote niliyopita takwimu za uandikishaji zimekwenda juu, hii tafsiri yake ni nini? Kwa mwananchi wa kawaida ambaye alishindwa kupeleka mtoto wake shule sasa hivi jambo hili limepokelewa kwa namna ambayo kwetu sisi wanyonge limekuwa ni jambo la kheri. Kwa hiyo, lazima tuipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi hii ambayo imeamua kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kupokelewa kwa elimu bure, yako maeneo ambayo nimeona kuna changamoto ambazo ningependa kuishauri Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni kuangalia namna gani tunaweza tukaongeza bajeti ili tuweze kukabiliana na hizi changamoto ambazo tumeanza kuziona katika kipindi hiki cha mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo sasa hivi watoto wanakaa chini kama ambavyo tumezungumza, hii ni kutokana na ukosefu wa madawati lakini pia yako maeneo ndani ya Jimbo la Nachingwea watoto wanasomea nje kwa

maana hawana madarasa. Kwa hiyo, naomba niungane mkono na wale wote waliotangulia kuomba Wizara ya TAMISEMI ijielekeze kwenye kuongeza bajeti ili tuweze kupata majengo ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba wananchi wanaendelea kutu-*support* kufyatua tofali na kujitolea wao wenyewe kujenga miundombinu hii, lakini ni muhimu pia Serikali ikaona umuhimu wa kuongeza jitihada ili tuweze kupata pesa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuishauri Serikali ni eneo ambalo linahusiana na uendeshaji wa mitihani. Nimefanya mazungumzo na walimu katika shule zote za ndani ya Jimbo langu. Moja ya changamoto kubwa ambayo naiona ni lazima tuiwahi, ni eneo la ukosefu wa pesa za uendeshaji wa mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitihani hii kwa kipindi cha nyuma kwa sehemu kubwa ilikuwa inategemea michango ya wazazi, sasa hivi baada ya kuondolewa, tayari pesa inayopelekwa kwa idadi ya wanafunzi katika shule, haiwezi kutosheleza kuendesha mitihani mitatu mpaka minne kwa mwaka. Na mimi kama mwalimu natambua umuhimu wa kutoa mazoezi kwa watoto. Usipotoa mazoezi kwa watoto, watakwenda kufanya mitihani vibaya.

Kwa hiyo, ni lazima tujielekeze kutenga pesa ya ziada ambayo itaelekezwa katika kutoa huduma hii ya mitihani ili kuwapima watoto wetu waweze kufanya vizuri katika mitihani yao ya mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine katika upande wa elimu ni ujenzi wa maabara. Ujenzi wa maabara umefanyika Tanzania nzima. Kwa Jimbo la Nachingwea, ndani ya kata 29 tayari wananchi walishapokea wito wa kujenga maabara. Maabara hizi zitatupelekea kupata walimu wa masomo ya sayansi; na hili ndilo tatizo kubwa sasa hivi tulilonalo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Jimbo la Nachingwea walimu wa masomo ya sanaa siyo tatizo, sasa hivi tatizo ni walimu wa masomo ya sayansi. Ili tupate walimu wa masomo ya sayansi ni lazima tukamilishe ujenzi wa hizi maabara ambazo zimejengwa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Simbachawene, una kazi ya kufanya sasa kaka yangu ili tuweze kupambana. Pale wananchi walipofanya na wameshamaliza nguvu zao, sasa ni muhimu na sisi tukaelekeza pesa ambayo itaenda kumalizia ujenzi wa haya majengo, lakini pia tupate vifaa ambavyo tutakwenda kufundisha watoto wetu kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili liende sambaba na suala zima la uboreshaji wa stahiki za walimu. Walimu wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu. Tunahitaji kulipa madeni yao yote ambayo wanatudai. Nakubaliana kwamba madeni hayawezikuisha kwa sababu kila siku walimu wanaajiriwa na hii ni sekta kubwa ambayo imebeba watumishi wengi, lakini ni muhimu tukahakikisha tunalipa madeni ya walimu wetu kwa wakati ili waweze kufanya kazi na waende sambamba na hili suala la utoaji elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo napenda kulichangia ni suala la maji. Nachingwea kuna tatizo la maji. Nachingwea ni Wilaya kubwa kama ambavyo nimesema, lakini pia nachukua nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri wa Maji, Mzee wangu Mheshimiwa Kamwelwe; alifika Jimbo la Nachingwea akajionea hali halisi ya pale. Ipo miradi ya *World Bank* ambayo inatekelezwa ndani ya Jimbo la Nachingwea, lakini bahati mbaya tulishamwambia, miradi saba iliyopo ndani ya Jimbo la Nachingwea haifanyi kazi mpaka sasa hivi, pamoja na kwamba pesa nyingi imetumika kujenga miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mzee Kamwelwe, lakini pia naomba niseme Mheshimiwa Waziri wa Maji, ambaye nafikiri atakuwa ananisikia, wananchi wa Nachingwea bado kuna ahadi walipewa na wanasubiri majibu juu ya miradi hii ambayo nimeisema ambapo inaonekana kuna uzembe wa baadhi ya watendaji wameamua kutumia pesa kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hizi, jibu linasubiriwa na wananchi wa Nachingwea, na mimi nimetumwa, naomba niliwasilishe mbele yenu ili tuweze kusaidiana kulifanyia kazi, tuhakikishe tunachukua hatua pale ambapo mambo hayajaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine katika upande wa maji, ni ukamilishaji wa mradi wa maji ya Mbwinji ambayo unatoka Masasi, lakini inagusa Vijiji vya Nachingwea na Vijiji vya Ruangwa ambako anatoka Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hali ya maji katika baadhi ya maeneo ndani ya maeneo yanayopita mradi wa Mbwinji siyo nzuri. Kwa hiyo, naomba nikumbushe Serikali yetu, katika bajeti hii tunayoenda kuipitisha, ni lazima miradi hii twende tuifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ambalo napenda kulizungumzia; na hili nitoe ushauri; ni miradi ya *TASAF*. Naomba niungane na Watanzania wote kuthamini na kutambua kazi kubwa ambayo inafanyika katika kutekeleza miradi ya *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo ambayo nimeona kuna upungufu. Wakati pesa za kutoa kwenye kaya masikini zinatolewa, kuna ushauri tuliutoa, lakini haukupokelewa. Sasa hivi naona kuna umuhimu Serikali hii ya Awamu ya Tano ifikirie namna ya kuboresha eneo hili. Pesa hii kuwapa wale wananchi mkononi kama ambavyo inafanyika sasa hivi, haina tija. Nimezunguka katika vijiji vyangu, nimefanya tathmini kuona ni kwa namna gani wananchi wananufaika na hizi pesa, bado sijaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Mheshimiwa dada yangu Angellah, kama tunaweza kubadilisha mfumo, ni vizuri pesa hizi sasa hivi na hasa kwa wananchi wa Jimbo la Nachingwea, tukawanunulia matrekta badala ya kuwapa pesa. Matrekta haya yatawasaidia wao wenyewe katika vijiji vyao, kwa sababu kutibulisha ekari moja shilingi 50,000; wanaweza wakatibulisha kwa shilingi 20,000 au shilingi 30,000 tukapunguza gharama. Baada ya kufanya hivyo, nafikiri tunaweza tukaona tija ya pesa hii badala ya kuwapa pesa mkononi ambayo mwisho wa siku wanatumia kutafuta chakula na bado wanaendelea na umasikini wao. Kwa hiyo, hili niliona nilitoe kama ushauri. Eneo hili pia naomba liendane na ile shilingi milioni 50 ambayo inaenda kutolewa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi milioni 50 hii lazima tuwe makini, nayo pia tuwe makini; nayo tungeiratibu, siyo kwa kwenda kutoa katika vikundi kama ambavyo imeshauriwa. Hii bado nilikuwa naona vijiji vipewe maelekezo ya namna gani vinaweza vikabuni miradi ambayo itaenda kunufaisha kijiji na ikasimamiwa na kijiji, badala ya kuwapa pesa ambazo tuna hakika zinakwenda kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikundi vingi sasa hivi vinafufuliwa kwa sababu kuna hii pesa. Baada ya hii pesa kutolewa nina hakika vikundi hivi vitakufa na vitapotea kitu ambacho sioni kama tutakuwa tumeisaidia nchi yetu na Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia, ni afya. Zipo changamoto ambazo tunaziona lakini bado tunahitaji kuendelea kuiunga mkono Serikali yetu. Kuna eneo la *CHF*…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Aeshi, atafuatiwa na Mheshimiwa Jacquline Msongozi.

MHE. KHALFAN H. AESHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia. Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Sumbawanga Mjini kwa kunipa nafasi tena kwa mara ya pili kuwa Mbunge wa Jimbo la Sumbawanga Mjini. *(Makofi)*

Jambo la pili naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya, ninaamini Watanzania wote tuko nyuma yake kumwombea Mungu ili aendelee na kazi hii nzuri aliyokuwa ameianza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la tatu, nawapongeza Mawaziri wote walioteuliwa. Naomba niwakumbushe tu wengi wenu tulikuwa huku nyuma, tunakaa pamoja, lakini mmetuacha, mmetangulia, naomba mtumtendee haki kwa sababu na sisi ipo siku tutakuja kukaa huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie masuala matatu, lakini katika masuala hayo yapo ambayo inawezekana kwa njia moja au nyingine isiwaguse Mawaziri waliopo mbele yetu hapo; Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Angellah Kairuki, ni kutokana na majukumu niliyonayo. Inawezekana wakati huo wa kuchangia muda mwingine nisiwepo, Mawaziri waliokuwepo waya-*note*, wayachukue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la kwanza ni kuhusiana na uwanja wa ndege. Sumbawanga tumejaliwa kuwa na mambo mengi, lakini yapo mengi ambayo tumeyatekeleza kwa mwaka 2010/2015, lakini yapo machache ambayo tulikuwa hatujayakamilisha, ni pamoja na uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeiona bajeti hii ambayo ninaamini tumepata fedha za kujenga uwanja wa ndege, lakini kuna shida moja naomba ichukuliwe kwa sababu wakati tunafanya tathmini ya yale majengo ambayo wananchi wanatakiwa walipwe fidia, tathmini ile imechukua miaka saba sasa. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kwenye bajeti hii tumetenga fedha za uwanja ndege, lakini tumetenga fedha kwa tathmini ya miaka sita iliyopoita. Kwa hiyo, naomba sasa tathmini ile ifanywe upya ili wananchi wapate haki yao na waweze kujenga kutokana na gharama zilizopo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili ambalo ni kero kwa wananchi; na kwa hili naomba nichukue nafasi kumpongeza Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi, kwa kazi kubwa aliyoifanya mpaka hapa tulipo leo. Isipokuwa shamba lile la Malonje limekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi na Mheshimiwa

Waziri alisema atakuwa ni mtu wa mwisho kuongelea shamba lile. Sasa nataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, alifanyie kazi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimpe nguvu tu Mheshimiwa Waziri, kwa sababu shamba hili linahusiana na watu wa TAMISEMI na Mheshimiwa Waziri unanisikia, basi naomba tulifanyie kazi ili wananchi waweze kupata shamba lile lililokuwa ni kero kubwa na sisi tunazingatia kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo, lakini naamini kabisa kilimo ni ajira. Tukiwapa ardhi wale wananchi, wanaweza wakalima na wakapata mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Rais, mgombea wetu alipokuja Sumbawanga kwenye kampeni aliniahidi, akasema endapo mtamchagua Aeshi, chochote atakachoniomba nitampa. Mimi naomba nimwambie Mheshimiwa Rais, sihitaji Uwaziri, wala Unaibu Waziri, naomba anisaidie shamba lile liweze kurudi kwa wananchi. Ninaamini uwezo huo anao na anaweza akatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la tatu, ni maji. Mheshimiwa Waziri tuna mradi mkubwa sana wa maji wa shilingi bilioni 32, mradi ambao tumeweza kujenga miundombinu yote, lakini shida imekuja kila tukichimba kisima hakina maji. Sasa nataka niseme maji ya kutoka *Lake Tanganyika* tungeweza kuyapata kwa sababu kutoka *Lake Tanganyika* – Kasanga kuja Sumbawanga ni kilometa 90. Ninaamini kabisa endapo tukipata fedha, tukajenga mradi ule wa maji wa kutoka *Lake Tanganyika* - Kasanga ukapita Matai na Sumbawanga vijiji vyote vitaweza kufanikiwa kupata maji. Kwa hiyo, nataka niseme tu, jambo hili tuliangalie kwa umakini, endapo tutapata fedha, basi tujaribu kutafuta njia moja ama nyingine ya kuweza kutoa maji *Lake Tanganyika* ambayo yataweza kuwanufaisha watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni kuhusiana na umeme. Tumepeleka vijiji vingi sana lakini bado vijiji vichache ili tuweze kufanikisha Jimbo lote la Sumbawanga mjini kuwa na umeme. Kwa hiyo, Waziri anayehusika na dhamana ya umeme, naomba naye alichukue kwa sababu kwa upande wa CCM kwa sababu tupo wengi, inakuwa ni vigumu sana kupata nafasi ya kuchangia mara ya pili.

Mwisho kabisa ni kuhusiana na meli *MV. Liemba*. Tumeona kwenye bajeti kwamba *MV. Liemba* itafanyiwa marekebisho, nasikitika sana! Meli ile mara ya mwisho nilipanda nikaona kuna jenereta imewekwa juu kabisa kule, ipo nje na ni hatari kubwa. Vilevile meli ile imekuwa ni ya muda mrefu sana, ina umri zaidi ya miaka 120, wananchi bado wanaendelea kuitumia meli ile, ni hatari kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama tumeweza kununua meli Ziwa Victoria, basi ni vizuri sasa na *Lake Tanganyika* tukakumbukwa angalau kwa meli moja ya kuanzia. Baada ya kusema hayo machache, naomba haya machache niliyoongea, naamini ni ya muhimu ndani ya Jimbo langu la Sumbawanga Mjini, mengi nimeyafanya kama Mbunge, mengi nimeyakamilisha, haya machache ukiyakamilisha mwaka 2020 napita bila kupingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nashukuru sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Jacqueline, atafuatiwa na wafuatao; Mheshimiwa Saed Kubenea, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe na Mheshimiwa Halima Ali Mohammed wajiandae. Tunaendelea Mheshimiwa Jacqueline! Hayupo, haya tunaendelea, Mheshimiwa Saed Kubenea!

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Kwanza niseme kwamba siungi mkono bajeti hii kwa sababu haitekelezeki.

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI na nilisema kwenye Kamati kwamba baadhi ya Mikoa iliyoleta bajeti kwenye Kamati, bajeti yao walipunguza kwa zaidi ya asilimia 60. Kwa hiyo, kwa maoni yangu, bajeti hii haitekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie suala zima la Shirika la Usafiri la Dar es Salaam (UDA) pamoja na mradi wa mabasi yaendayo kasi ya *DART*. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kikao cha Baraza la Madiwani cha Kamati ya Uongozi cha Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Serikali yenyewe na Msajili wa Hazina, zimejiridhisha kwamba hisa za UDA ziliuzwa kinyume cha taratibu kwa anayejiita mwekezaji Kampuni ya *Simon Group Limited*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali za UDA zinazohamishika na zile zisizohamishika, zimetapakanywa katika mabenki mbalimbali kwa kuwekwa dhamana. Naye Mwanahisa mkubwa Hazina, hakuridhishwa na uamuzi wa kuuzwa UDA. Mkutano Mkuu wa Wanahisa wa tarehe 10 Juni, 2011, uliosimamiwa na aliyekuwa Meya wa Jiji la Dar es Salaam kuidhinisha uuzaji wa UDA haukuwa halali. Serikali inalijua hili, Bunge la Jamhuri wa Muungano linalijua hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano uliitishwa na watu wanne, haukutimiza akidi na ulisimamiwa na mtu mmoja anayeitwa Didas Masaburi, aliyekuwa

Meya wa Jiji la Dar es Salaam; Robert Kisena, Mkurugenzi wa *Simon Group;* Mwanasheria wa Jiji, Issack Nassoro na Mkurugenzi wa Jiji, Philips Mwakyusa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mkutano huo, ndipo ikatangazwa kwamba UDA, *Simon Group* imetimiza masharti. Taarifa ya Serikali ya Agosti 3, mwaka 2011, kwenda kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba niinukuu na inasema: "Mkutano ulikuwa batili kwa kuwa ulikiuka Katiba ya UDA Kifungu 45 kutokana kwa kutotimia kwa akidi na kukosekana kwa Msajili wa Hazina. Serikali inakiri kikao hicho hakikuwa na mamlaka ya kufanya maamuzi na maazimio yoyote yaliyofikiwa yalikuwa batili." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi wakati kikao cha kugawa hisa za UDA kinafanyika, Meya wa Jiji alipokea barua ya tarehe 28 Februari, 2011 kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, iliyomwagiza kusitisha mara moja mchakato wa kuuza hisa za UDA ambazo hazijagawiwa. Barua kutoka Serikalini (Ofisi ya Waziri Mkuu) ilibeba Kumb. Na. 185/295/07/27.

Barua hii ipo Ofisini mwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ipo Hazina, lakini Serikali imeendelea na mchakato wa uuzaji wa UDA kinyume cha taratibu; Serikali imeendelea kumilikisha mali ya umma kinyume cha sheria. Wanakiri katika nyaraka zao zote kwamba mbia hakutimiza masharti yote ya mkataba, lakini bado Serikali inaridhia na tayari *Simon Group* amelipa shilingi bilioni tano kwenye akaunti ya Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya kumiliki hisa za UDA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba maamuzi yaliyofikiwa na Kikao cha Kamati ya Uongozi na Fedha, kilichofanyika juzi cha kuzuia hisa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuuzwa ninaunga mkono kwa asilimia mia moja. Fedha zilizowekwa katika akaunti ya Jiji hazitarudishwa mpaka hapo Jiji la Dar es Salaam litakapofanya hesabu zake na kuona *Simon Group* ametumia leseni ya UDA na mali za UDA, ameweka Benki, amepata faida. Tufanye ukaguzi wa ndani kujua ni kiasi gani cha faida alichopata, hapo ndipo tunaweza tukarudisha hizo hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli uuzaji wa hisa za UDA na UDA yenyewe na *DART* yenyewe imegubikwa na udanganyifu, ulaghai, utapeli na Serikali inakiri katika nyaraka zake; na Waziri anakiri na anajua kwamba mchakato wa UDA haukufuata taratibu; lakini wanaendelea na mradi wa uendeshaji wa mabasi yaendayo kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umetokana na mkopo wa fedha ambazo Serikali imekopa kutoka Benki ya Dunia, lakini anayetumia barabara zile ni mtu mmoja. Kampuni ya UDA inaulizwa hawa wenye daladala watatumia nini? Wanasema tutawaingiza katika huo mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri anapojibu alieleze Bunge hili Tukufu kwa nini mkopo huu ubebwe na Watanzania wote wakati barabara zinatumiwa na mtu mmoja? Ni vizuri mkopo huu ukabebwa na yule anayetumia barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimeona hapa Bungeni, baadhi ya Wabunge wenzangu wanasimama macho yakiwatoka, wakiunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais za kupambana na vita dhidi ya ufisadi. Baadhi yao ukiwaangalia, hawafanani na wanachokisema. Wengine sisi hatukuvamia hili treni la ufisadi, *records* zipo! Tumepambana Mwenyekiti unajua na Bunge hili Tukufu linajua. Kwa hiyo, sisi wengine tupo tayari kupambana na vita hii hadi mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja hapa imejitokeza na inazungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge, juu ya kuzuia vyombo vya habari kurusha matangazo ya moja kwa moja ya Bunge. Naomba niseme machache mawili na moja, naona Waheshimiwa Wabunge wanamtupia mzigo mkubwa, ndugu yangu Mheshimiwa Nape. Mheshimiwa Nape hahusiki na hili jambo, mnambebesha mzigo asiohusika nao; siyo wake! Tafuteni mwenye mzigo huu. Huu ni uamuzi uliofanywa na vikao vya juu, Mheshimiwa Nape ni wakala tu hapa. Shikeni hao! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba Bunge hili linafuata nyayo za Bunge la Uingereza, lakini chini ya Bunge hili, *TBC* ndiyo ambayo inaendesha hii *studio* ya Bunge. Kinachoitwa *studio* ya Bunge ni koti la *TBC* lililovaa Bunge. Wafanyakazi 15 waliopo hapa nawajua kwa majina, ni waajiriwa wa *TBC*.

Kwa hiyo, ni hatari sana kuona kwamba Bunge letu linaacha utaratibu wake wa kawaida. Hata huko Uingereza, Bunge linaonyeshwa *live*, vyombo vya habari vinaonyesha *Bunge Live*. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kusema kwamba mimi nadhani uamuzi huu ni lazima uangaliwe vizuri na busara itumike kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, jana Mheshimiwa Zitto amezungumza juu ya hoja ya watu ambao wanapata…

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68 (8)…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, sijakuruhusu!

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee nimalize...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, sijakuruhusu.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namaliza kwa kusema kwamba Mheshimiwa Zitto jana…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kubenea, muda wako umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, leo mtanisamehe sana kwa mambo ya Taarifa. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe atafuatwa na Mheshimiwa Halima Ali Mohammed, halafu tutarudi kwenye upande wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni; naunga mkono pia hotuba mbili za Utumishi na mambo ya TAMISEMI kwa Wasemaji wa Upinzani Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo kadhaa hapa ya kuzungumza. Kuna hoja hapa ya ndugu yangu, Mheshimiwa Angellah Kairuki aliyowasilisha, ya Utawala Bora; ndiyo nataka nianze nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora ambao unazungumziwa ni muhimu tungeanzia hata humu ndani kwenye Bunge hili kama kweli kuna utawala bora. Bunge limengolewa meno, limekuwa butu kweli kweli!

MBUNGE FULANI: Kibogoyo!

MHE. MWITA M. WAITARA: Bunge limekuwa kibogoyo! Bunge limekuwa na watu waoga kweli kweli! Wabunge hawana uhuru wa kuzungumza na kutoa maoni yao! Hili Bunge ni aina ya Mabunge ambayo hayajawahi kutokea, labda hii ndio kazi tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevya. Nimesikiliza Wabunge wa CCM wengi waliopangwa kwenye Kamati ile. Inaonekana walipangwa na Mheshimiwa Spika kwa maelekezo na naambiwa kwamba kikao kilikaa, wale wengi ambao

walikuwa wanamuunga mkono Mheshimiwa Lowassa walitupwa kwenye Kamati yangu na mimi naipenda sana, kama sehemu ya kuwaadhibisha. Maana yake hiyo kazi Spika aliifanya kwa maelekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Spika mwenyewe ningependa awe hapa. Jana alimwita Mheshimiwa Mbunge mwenzetu hapa bwege. Akamwambia aache ubwege! Yaani bwege asionyeshe ubwege!

MBUNGE FULANI: Al maarufu Bwege.

MHE. MWITA M. WAITARA: Kwenye kikao cha Bunge jana! Ilizungumzwa, wala siongei uongo. Hapa nitaongea mambo ya ukweli tupu. Alisema Mheshimiwa Bwege, naomba uache ubwege. Sasa wataalam wa Kiswalihi wanaweza wakasaidia. *(Makofi)*

Vilevile katika mazungumzo yake tunajua wapo Wabunge na nitawataja, wakati inazungumzwa hoja ya Wabunge wa CCM ambao wana tuhuma za kuomba rushwa kwenye Kamati mbalimbali, wanataka kupelekwa Mahakamani, Mheshimiwa Lusinde alipigiwa simu kwa maelezo yao na Mheshimiwa Rais Magufuli akimwambia kwa nini unaunga mkono hawa watu wasipelekwe Mahakamani haya majizi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, juzi ametoa hoja ya kuzungumzia mabonde ya Dar Salaam kwa nini nyumba zimevunjwa... **[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi]**

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Kuhusu Utaratibu!

MHE. MWITA M.WAITARA: Na yeye vile vile ametishiwa na watu wa CCM kwamba anaisema Serikali yake.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu!

MHE. MWITA M.WAITARA: Kwa hiyo, hapa hakuna utawala bora.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara, kuna suala la Mwongozo, naomba uketi tu.

MBUNGE FULANI: Utaratibu!

MWENYEKITI: Haya Mwongozo, nitakubali.

MBUNGE FULANI: Utaratibu! Kuhusu Utaratibu!

MWENYEKITI: Utaratibu eeh, Mwongozo alikuwa anaongea huyu!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatumia Kanuni ya 68(1) nitakwenda pamoja na Kanuni ya 64 ambayo inatoa makaripio na makatazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema hapa ni kwamba, kanuni ya 64 inatukataza sana kutumia jina la Mheshimiwa Rais kushawishi Bunge kukubaliana na jambo lolote lile kwa kutumia jina la Rais. Namheshimu sana Mheshimiwa Mwita, ana uwezo wa kujenga hoja yake, lakini anapotaka kuwafanya Wabunge wakubali yale anayosema kwa kutumia jina la Mheshimiwa Rais, hii inakatazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kanuni hii ya 64 na vifungu vyake vyote vinavunjwa, naomba Mheshimiwa Mwita ajielekeze kwenye hoja na aache kumtumia Mheshimiwa Rais kama hoja ya kulishawishi Bunge likubaliane na yale anayoyasema.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwita Waitara, Kanuni hiyo unaifahamu kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, sikuombwa Mwongozo kwa sababu Mwongozo mnajua ni lini unaombwa. Sasa hili ni katazo na ukiendelea kulitumia maana yake tunafuata *consequence* zake ni nini.

Sasa Mheshimiwa Waitara nakutaka usielekee huko, ufute sasa hayo mawasiliano kati ya uliyowataja ili twende vizuri na kanuni. Wewe ukisema tu nayafuta hayo, tunakaa vizuri, kwa sababu hatua ya pili ni kukutaka mawasiliano hayo utuletee hapa, siyo vizuri. *(Makofi)*

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuelewa na nitazingatia ushauri wako. Kwa hiyo, maneno yote yale yameondolewa eeh! Mnapenda sana hiyo eeh! *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Ahsante. Endelea kwa dakika zako zilizobaki.

MHE. MWITA M.WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu ulindwe.

Hoja yangu tu ni kwamba, Bunge hili Waheshimiwa Wabunge hawana uhuru, wanapigiwa pigiwa simu, haijalishi nani amepiga lakini wanapigiwa na watu wa ngazi ya juu kwa kuwatishatisha ili wasiwe na uhuru wa kutoa maoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa mbalimbali za ukaguzi inaonyesha kwamba hata Ikulu yenyewe kunakuwa na rushwa. Taarifa mbalimbali zipo, wala hili huwezi kupinga. Sasa kama Mheshimiwa Mwalimu Nyerere aliwahi kusema kwamba Ikulu ni mahali patakatifu, kama kuna chembe chembe za rushwa kwa nyakati mbalimbali, sasa huo utawala bora utawaelezaje watu wa kawaida kama kule jikoni kwenyewe chakula kinaibiwa, watu wananyofoa minofu jikoni...

MBUNGE FULANI: Mwenyekiti Taarifa!

MHE. MWITA M. WAITARA: Tutafanyaje katika mazingira hayo?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ulizikataa, nakushukuru sana.

MBUNGE FULANI: Kakataa!

MHE. MWITA M.WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kaka yangu, sisi watu wa kule kwetu huwa hatuogopi kusema ukweli. Namshauri Mwanasheri Mkuu wa Serikali, asiwe anatoa tafsiri za sheria za ki-CCM atoe tafsiri za kisheria za sheria *in profession*. Namshauri sana maana yake nimevumilia imebidi niseme tu hadharani kwamba ni muhimu Mwanasheria aseme sheria za kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hapa kuna mambo yanaelezwa, sisi tulichosema ni kushauri kwamba katika mambo kadhaa yaliyofanyika, Mheshimiwa Rais hajafuata utaratibu kwa maana ya kutumia mamlaka yake vibaya, kwa maana ya kufanya *reallocation* ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ushauri na sheria hizi zipo, utakuja na tafsiri nyingi sana kwa maana ya kuficha mambo, lakini ukweli unabaki pale pale. Naomba nitaje kwa mfano, Katiba ya Nchi Ibara 18(a), (b) na (c) kinaeleza uhuru wa kupata habari; tena unasema hata nje ya mipaka ya nchi. Hili jambo huhitaji kupata mkalimani, inaeleweka tu, kwamba Watanzania wamenyimwa fursa ya kupata taarifa ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapanga wananchi hawa walipe kodi, tunawashawishi namna gani? Hawa jamaa wa CCM wameenda wamekaa kwenye mkutano wao, wanaaminisha watu kwamba ooh, watu wa Upinzani tutaonekana. Hii siyo hoja! Ni hoja ya kitoto kabisa! Hoja hapa ni kwamba ni kwa nini kama kweli mnafanya kazi vizuri, wananchi wasiwe na uwezo wa kujadili na kuona tunachokiona? Nawa…

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

MWENYEKITI: Ahsante, muda wako… Aalah! *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Makatibu wamechakachua!

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kengele ya kwanza. Nakushukuru! Naona sasa unaanza kunitania! Aisee! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hoja nyingine, ukisoma Ibara ya Katiba ya 135, mambo yale ya Hazina inaeleza, Katiba ya Ibara ya 146(1) inaeleza, vitu vingi vimezungumzwa.

Niende kwenye hoja ya TAMISEMI; kuna jambo la bodaboda hapa; hawa vijana na hasa Dar es Salaam. Sasa hivi kuna uhalifu mkubwa, vijana wetu walishawishika, wengine wamechukua mikopo, wanajikopeshea fedha zao kwa watu binafsi na wengine VICOBAvile wanapata fedha ya kujiendeshea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mitindo wa kusumbuliwa sana Dar es Salaam pale! Kuna watu wameitwa Askari wa Jiji, nadhani wale tutawashughulikia kwa sababu Jiji la Dar es Salaam tunaongoza sisi, nami ndio Mwenyekiti wa Mkoa, naelekeza sasa, Meya wa Jiji la Dar es Salaam, hili jambo alifanyie haraka mapema sana. Hawa vijana wanapata shida kule Dar es Salaam, wanakamatwa hovyo, wanasumbuliwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameenda kuteua hawa Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, Ma-RAS waliostaafu Majenerali. Sasa hawa vijana ambao wanahitaji hapa ajira, si angewapa kazi hao vijana! Humu ndani kuna Wabunge wana vyeo viwili viwili; yaani mtu ni Mbunge halafu ni *DC,* halafu ajira ni shida! Hivi huyu mwenye vyeo viwili ana nini? Ana pembe kichwani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanyang'anywe vyeo, tugawane kilichopo. Mtu amefanya kazi, amestaafu, anapewa kazi nyingine tena, halafu mnataka ufanisi! Watu wameshachoka, wanasinzia ofisini mnawapa kazi nyingine. Hii kitu kwa kweli vijana hawa msiwanyanyase na utaratibu uwekwe sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti ya Manispaa ya Ilala tumekadiria kukusanya shilingi bilioni 85 ikiwepo kodi ya majengo na mabango lakini shilingi bilioni 28; Shilingi bilioni 18 majengo na Shilingi bilioni kumi ni mabango. Maana yake huu mpango, kwenye hotuba ya Waziri wa TAMISEMI inaeleza kwamba Halmashauri itasimamia, kwenye Mpango wa Waziri wa Fedha inaonyesha vinginevyo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind-up* hapa aeleze kipi ni kipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Ilala ilifanyiwa ukaguzi mwaka 2011/2012 - 2012/2013 lakini na hii ya leo nimeisoma, Manispaa ile inaonekana ni miongoni mwa hati isiyoridhisha. Sasa haya mambo, walikaguliwa watu 2011, Mkaguzi Mkuu alikagua, akaleta taarifa; lakini ninavyozungumza hapa, tuna vitengo na idara zaidi ya 18 lakini viongozi wale watano tu ndio wamethibitishwa, wengine wote wanakaimu. Nimejaribu kuhesabu hapa, karibu 13! Sasa katika mazingira hayo, tunafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Halima Ali Mohamed, atafuatwa na Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka na Mheshimiwa William Ngeleja.

MHE. HALIMA ALI MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mara ya kwanza kabisa kusimama katika Bunge lako hili Tukufu. Namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na utukufu kwa kunijalia afya njema. Nakishukuru Chama changu, Chama cha Wananchi *(CUF)* kwa kuniamini, nami nitajitahidi kuwatendea haki wananchi wote kwa kuwawakilisha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu afya. Suala la afya ni suala ambalo halina mjadala. Ni suala ambalo ni muhimu kwa maisha ya binadamu! Bila ya Afya, hakuna maendeleo. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, amezungumzia kuhusu idadi ya vituo vya huduma ya afya na vilevile akaelezea azma ya Serikali ya kuweza kuendeleza vituo vya afya katika ngazi ya kata, ngazi ya kijiji na ngazi ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kuna manung'uniko makubwa sana katika huduma ya afya; kuna matatizo lukuki katika huduma za afya katika zahanati zetu. Sasa hivi zahanati zetu ni kama madarasa matupu pamoja na mizani ya kupimia watoto. Kuna changamoto chungu nzima! Zahanati zetu hazina nyumba za madaktari, hakuna vifaa tiba, hakuna dawa, hata wafanyakazi hawatoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoboresha huduma za afya, basi umewasaidia wanawake na umewasaidia wananchi wote. Naishauri Serikali iboreshe miundombinu katika huduma za afya, lakini vilevile Serikali iongeze bajeti katika Wizara ya Afya na kuwe na ukaguzi wa zahanati zetu, vituo vya afya na hospitali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba nizungumzie kuhusu suala zima la fungu la UKIMWI. UKIMWI bado upo katika nchi yetu lakini vilevile ni tatizo na ni janga kubwa sana katika nchi yetu. UKIMWI unamaliza nguvukazi ya nchi yetu na ukitilia maanani zaidi wanaoathirika ni akina mama kwa sababu ndio wanaopata maambukizi kwa sababu ya maumbile yao na kama katika familia kuna wagonjwa, basi wanawake ndio wanaohusika katika kuhudumia wagonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako nitoe takwimu za maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI kwa baadhi ya Mikoa iliyopo Tanzania Bara. Kwa mfano, Mkoa wa Njombe una asilimia 18.8, Mkoa wa Iringa una asilimia 9.1, Mkoa wa Mbeya una 9%, Mkoa wa Rukwa una asilimia 7.2 na Mkoa wa Shinyanga una asilimia 7.4. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kwamba ni asilimia 40 ya wananchi wetu bado hawana taarifa kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Ni jambo la kusikitisha sana katika bajeti yetu hii yote hakuna fungu ambalo limetengwa kwa ajili ya wagonjwa wa UKIMWI. Tunategemea wafadhili ambao hawana uhakika! Tunategemea wafadhili ambao wana *interests* zao! Kwa hiyo, naishauri Serikali itenge fungu la mapato ya ndani kwa ajili ya ugonjwa huu wa UKIMWI, ugonjwa ambao ni hatari na ni tishio katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka nizungumzie kuhusiana na suala la 10% ya mapato ya Halmashauri zetu kutengewa makundi haya mawili ya wanawake na vijana. Hili ni agizo na wala siyo hiari Halmashauri kama wakipenda watenge na wasipopenda wasitenge. Hili ni agizo, lazima litekelezwe lakini kwa bahati mbaya agizo hili halitekelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itengeneze sheria ambayo itatia nguvu ili Halmashauri ambazo hazikutekeleza, basi ziweze kuwajibishwa. Vilevile nataka nisisitize kwamba katika fungu hili la 10% za wanawake, hizi ni pesa za walipa kodi wa nchi hii, kwa hiyo basi, ni budi fedha hizi zigawiwe bila itikadi za vyama. Wananchi wote ni sawa, kwa hiyo, wana haki sawa mbele ya sheria katika nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu miradi ya *TASAF III.* Mradi huu Serikali ilikuwa ina nia safi tu ya kusaidia kaya ambazo ni masikini, angalau basi na wao waweze kupata fedha kidogo ya kuweza kununulia angalau sare

za shule za watoto wao pamoja na kudiriki kuwapeleka watoto hawa wachanga *clinic*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unatumika kinyume na utaratibu. Kuna baadhi ya viongozi wanatumia fedha hizi kwa ajili ya kuboresha au kujijenga kisiasa. Hili ni kosa mbele ya sheria, lakini vilevile kuna tatizo kule kwetu upande wa Zanzibar. Upande wa Zanzibar Masheha wanatumika vibaya katika mifuko hii ya *TASAF*; wamepewa uwezo wa kuingiza majina wanayoyataka na yale wasiyoyataka wanayafuta. Wanakiuka, maana yake Masheha kule kwetu wana uwezo zaidi kuliko *CMC* ambao ndio wahusika wa huu mfuko. Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, naomba hilo ulichukulie kwa uzito wake uweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nilikuwa napendekeza kwamba posho ile ya shilingi 10,000/= ambayo wanalipwa wale vijana ambao wanasimamia ugawaji wa hizi fedha ambao ni *CMC,* haitoshelezi. Kwa hiyo, waangaliwe kwa jicho la huruma ili waweze kuongezewa kidogo, kwa sababu dhamana waliyonayo ni kubwa ya kusimamia fedha zile kuanzia Benki mpaka kuzigawa na wanapokosea mahesabu, basi wanafunguliwa kesi. Kwahiyo, ni vyema basi na wao wakaangaliwa kwa jicho la huruma ili wasiweze kufanya yale mambo ya kufanya wizi katika mfuko huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, halafu atafuata Mheshimiwa Ngeleja, Mheshimiwa Ngonyani, Mheshimiwa Kitandula, Mheshimiwa Vullu na Mheshimiwa Lusinde. Profesa!

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Tangu awali hapa ngoja niseme kabisa kwamba Bajeti iliyopo mbele yetu inastahili na ninaiunga mkono kabisa, ila sasa nachangia kwa mtazamo wa mwananchi wa Muleba Kusini na hasa Halmashauri ya Muleba kwa ujumla wake.

Imeshasemwa hapa kwamba kwa sisi ambao tunatoka kwenye Halmashauri ambazo ni kubwa na Majimbo makubwa, tuko katika hali ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Simbachawene atakaposimama hapa kufafanua, ajaribu kuoanisha mgao wa fedha zilizogawiwa na wingi wa watu na ukubwa wa eneo. Kwa maneno mengine, tunataka *weighted average;* kwa sababu haitoshi kusema fedha kadhaa zinapelekwa mahali, ni lazima uangalie *per capita;* wale wananchi

walio mle wanapata kiasi gani? Uone kama zinatosha kusukuma maendeleo au hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipofanya hivyo, tunajikuta katika hii *pressure* inayozidi kuongezeka ya kugawa Mikoa, Majimbo na Wilaya lakini mwisho wa siku tunakuwa na viongozi ambao sasa hawana *OC* ya kufanyia kazi, hili ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri ajaribu kutusaidia kama siyo sasa huko anapokwenda kuliangalia jambo hili, ni la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Muleba ndiyo kubwa katika Mkoa wa Kagera, ina Kilomita za mraba 10,500, theluthi mbili zikiwa ni maji, mimi hapa nina Kata 25; nina wananchi 600,000; nina wapigakura 264,000 na kadhalika na kadhalika. Sasa katika hali hiyo bajeti ambayo iko mbele yetu, kitu cha kwanza nakubaliana na Serikali. Serikali haiwezi kugawa fedha ambazo hazipo. Sisi kama Wabunge tunapenda sana kusema kwamba tuongeze bajeti, lakini nimeangalia katika majedwali ambayo Waziri ameleta hapa na yamekaa vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia jedwali namba 11, linaonyesha vitu muhimu. Kitu kinachokosa ni uwiano na wananchi katika lile eneo husika, hilo halipo. Isipokuwa utaona kwamba kwa ruzuku ambazo zimekwenda, kwa mfano kwenye *Road Fund*. *Road Fund* nadhani kila Mbunge hapa anaitegemea sana, lakini ni asilimia 5.25 ya fedha ambazo zililipwa zilizopelekwa kule.

Sasa unaona kwamba unapokuwa katika hali ya kupanga bajeti kubwa, watu wakawa na matumaini, Halmashauri zikafikia kwamba fedha zitatoka katika bajeti kuu, fedha hizo zisipokwenda tunarudi nyuma. Kwa hiyo, napendekeza kwa Mheshimiwa Waziri alifikirie hili atakapokuwa anajumuisha *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru zaidi na hapa ninapoangalia, Waziri wetu wa Utawala Bora na *decentralization*, dhana nzima ya kugatua madaraka ni kupeleka wajibu kwa hawa watu. Wajibu huwezi kupeleka wajibu bila kuwapa watu uhuru na kuwaamini. Nimemshukuru sana Waziri Mkuu aliposimama hapa na kusema sasa bajeti chini ya shilingi bilioni moja itaweza kuamuliwa yaani mikataba itaweza kuamuliwa kwenye Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia na Mawaziri wetu mwangalie suala la ajira kwa mfano, *process* ya kuwaajiri watu kwenye Halmashauri, eti watu wanatoka Dar es Salaam kuwaajiri Watendaji wa Vijiji Muleba. Jamani, mambo mengine Mheshimiwa Mwalimu Nyerere alisema kuna maendeleo ambayo hayahitaji pesa. Mtu atoke Dar es Salaam kusimamia eti kumwajiri Mtendaji wa

Kijiji. Sehemu nyingine Kiswahili ni lugha ya Taifa, lakini sehemu nyingine Mtendaji wa Kijiji ni vizuri pia akajua mazingira ya pale ambapo anaajiriwa. Kwa hiyo, unaona mantiki ya kuwa na Serikali za Mitaa ni nini. Kama tutaendelea na *control* ya namna hii, maana yake hii *central control* inafuta dhana nzima ya *decentrelization. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu limezungumziwa sana, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais ameshavuna *a low hanging fruit*. Kwa kutamka tu elimu bure, watoto walioandikishwa wameongezeka kwa asilimia 32. Nimeona hapa Mheshimiwa Waziri ameleta takwimu ziko *very clear*. Watoto walioandikishwa Darasa la Kwanza wameongezeka kwa 32%; kutoka bilioni 1.3 mpaka bilioni 1.8; ni maendeleo makubwa. Katika Mkoa wa Kagera wameongezeka kwa 44% na Muleba kwangu wameongezeka kwa 69% kwa tamko tu yaani hii ndiyo Mwalimu Nyerere alisema mendeleo yasiyohitaji pesa. Watoto kuletwa shuleni ni maendeleo, hayo tumeyaona. Sasa mtu anaposimama hapa kusema kwamba elimu bure haijaleta tija, huyo hawezi kuwa anakwenda na takwimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa ufahamu wangu wa mambo nasema kwamba *indicators* ya mafanikio ndiyo hizo kwamba watoto wameletwa shule. Sasa sisi tuwezeshwe na wahusika Mawaziri, tujitegemee. Kuna dhana ya kujitegemea. Hii *notion* kwamba Serikali italeta fedha, Serikali haiwezi kuleta fedha ambayo haina, hilo nalo tulijue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi kama Halmashauri nimeona kuna Halmashauri nyingine zimekopa, zimekuwa *pro-active* zimekazana. Halmashauri nyingine zimesubiri kwa sababu tunakosa mwongozo. Tunaomba Mheshimiwa Waziri utuletee mwongozo kuhusu waraka wa hii dhana ya elimu bure. Elimu bure haitaweza kujenga madarasa yote, haitaweza kujenga maabara zote, lakini wananchi tuko katika hali ngumu au siyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu niko katika hali ngumu. Siwezi kusimama Muleba nikawaambia wananchi wachangie, wakati wanasema kwamba Serikali imesema kila kitu ni bure. Nafikiri ingekuwa ni vizuri tukapata waraka sasa kutoka kwa Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa Elimu kufafanua *responsibility* ya mzazi ni nini na *responsibility* ya Serikali ni nini. Katika hili niseme waraka ambao ulitolewa na Wizara mwezi Disemba ulisema wazazi wanagharamia chakula, mimi kama mwalimu wa siku nyingi, naomba kama mtu mwenye umri hapa, maana yake na sisi wazee tuna kitu cha kuwaambia hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikisoma *primary* enzi za mkoloni, hakuna mtoto alikuwa anaruhusiwa kwenda shuleni bila chakula. Kulikuwa hakuna *hotpot,* hakuna kitu chochote, lakini mama anachemsha kiazi unakwenda nacho; mama anachemsha muhogo unakwenda nao; mama anakupa

kipande cha ndizi, unakwenda nacho. Sasa sisi tumekuwa Taifa, watoto wanashinda na njaa. Eti watoto watasomaje hawajala kitu chochote? *It is not serious! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo, nafikiri tungepata waraka ukafafanua mambo, sisi tuko tayari kuwajibika; Muleba Kusini tuko tayari kuwajibika lakini sasa ngazi za juu zisituchanganye. Mnatuchanganya kwa kusema kwamba mambo yote yatafanywa bure wakati uwezo wa kufanya bure hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo mchango wangu na ninautoa nikiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kabisa kwa sababu najua kwamba ndivyo hali ilivyo. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, watoto wa miaka minne kwenda kwenye chekechea, Mheshimiwa Waziri naomba uliangalie, labda umri ungepanda kidogo, kwa sababu watoto wanakuwa wengi, madarasa hayapo, walimu hawapo, *service ratios* haziwezi! Sasa unakusanya watoto wadogo 50 au 80 kwa mwalimu mmoja, ataweza kufanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi nyingine unasema kwamba watoto wawe miaka mitano au sita au saba kwa sababu inapunguza *pressure* kusudi uweze kujiandaa na kuweka *services* zinazohitajika.

Baada ya kusema yote hayo, naunga mkono hoja moja kwa moja, Muleba Kusini usitusahau Mheshimiwa Waziri, karibu ututembelee. Na wewe Mheshimiwa Mama Angellah Kairuki, njoo ututembelee, uje uangalie sasa Watendaji wa Vijiji walioajiriwa kutoka Dar es Salaam, kwa kweli ni kizungumkuti! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante, nakushukuru. Mheshimiwa William Ngeleja, atafuatiwa na Mheshimiwa Ngonyani.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote naendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kujaalia yaliyotokea mwaka 2015 na hatimaye kupitia wananchi wa Jimbo la Sengerema wakaendelea kuniamini na sasa naungana na timu ya kikosi cha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea maeneo matatu; la kwanza, nina masuala yangu ya Jimbo ambayo naamini Serikali kupitia Mawaziri husika

wanaendela kuyafanyia kazi. Pia nitatoa ushauri kidogo na mwisho nitauzungumzia utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Waheshimiwa Wabunge wengi hapa kuunga mkono hotuba na mapendekezo ya bajeti yaliyoletwa hapa mbele yetu kupitia Mawaziri wawili hapa Mheshimiwa Simbachawene pamoja na Mheshimiwa Angellah Kairuki na wasaidizi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hizi za Waheshimiwa Mawaziri hawa zimebeba mambo mengi sana; na kwa kadiri michango inavyoendelea inaonekana tu wazi ni dhahiri kwamba mambo mengi yamefanyika na kwenye mipango kuna mambo mengi yamepangwa kufanyika.

Mheshimiwa Simbachawene pamoja na Mheshimiwa Angellah Kairuki, nafahamu ninyi mnawakilisha, lakini kuna mambo mnayoyasimamia ninyi yanaingiliana, ni maeneo mtambuka na maeneo mengine na sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo nataka niikumbushe Serikali, pale Sengerema nina ombi langu la muda mrefu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema. Hospitali yetu teule iliyoko pale imezidiwa. Ruzuku inayotolewa pale haitoshi. Nimekuwa nikiomba na leo nakumbusha tena, ni mwaka wa tatu nakumbusha. Ile ruzuku ambayo iliyotumika kipindi kile wakati hospitali ilikuwa na vitanda 150, sasa ina zaidi ya vitanda 375. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ombi hili liendelee kufanyiwa kazi na ninaamini, nimeshazungumza na Mheshimiwa Ummy pamoja na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, naamini wako hapa wanaendelea kulifanyia kazi, lakini nasisitiza kwamba wananchi wa Sengerema wanahitaji kuona matokeo ya ombi letu yakifanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka nikumbushe, tuna ombi letu pale Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini sasa limerudi kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu viongozi hawa wako mbele yetu, Mawaziri hawa walioko katika Ofisi ya Rais, naamini kwamba, wanalifahamu. Tuna ombi la kupandisha hadhi Mji wa Sengerema kutoka Mamlaka ya Mji hadi Halmashauri ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusisitiza ni kwamba ombi lile pia limebaki kuwa la muda mrefu. Limechukua miaka kadhaa lakini ahadi za Serikali zimekuwa zinafanyiwa kazi. Naomba nisisitize kwa mara nyingine kwamba wananchi wa Wilaya ya Sengerema wana hamu kubwa kuona Mji wa Sengerema unapandishwa hadhi kutoka Mamlaka ya Mji kuwa Halmashauri ya Mji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia hizi bajeti lakini tukitambua katikati yake zipo Halmashauri ambazo hivi karibuni zimegawanywa, kumezalishwa Halmashauri nyingine ndani ya iliyokuwa Halmashauri moja. Ombi langu la ujumla, siyo kwa Wilaya ya Sengerema tu ambapo tumepata pia Halmashauri ya Buchosa, naomba Serikali itafakari, ione namna ya kuziongezea bajeti, kwa sababu bajeti tuliyopitisha mwishoni, Halmashauri zote ambazo ndani yake kumetokea Halmashauri nyingine ikiwemo Halmashauri ya Sengerema na Halmashauri ya Buchosa, nimesikia pia Halmashauri ya Chalinze na nyingine. Hili ni ombi la ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kuhusu suala la madawati. Kwa hali ilivyo na kwa mahitaji ya madawati yanayohitajika katika nchi yetu ya Tanzania, Halmashauri zote kwa vigezo vya mapato vilivyopo sasa, siyo rahisi sana kuliweza hilo jambo. Tunaomba Serikali izidi kutafakari kwa siku zilizobaki hizi mpaka mwezi wa sita. Kama katika bajeti hii tunapokwenda kupitisha tunaweza kufanya *adjustment* katika baadhi ya maeneo, tuziwezeshe Halmashauri zetu kupata fedha za kutengeneza madawati ili tuongeze kasi ya kutengeneza madawati kwa kuhudumia wanafunzi ambao sisi tunawalea kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano wa Jimbo la Sengerema. Jimbo la Sengerema tunahitaji madawati 23,000 leo. Maana yake unazungumzia zaidi ya shilingi bilioni moja; kwa hakika hatuwezi kuzipata kwa miezi michache iliyobaki pamoja na juhudi ambazo zinaendelea. Sisemi kwamba wananchi wakae au Halmashauri na viongozi wa Mkoa wakae tu, lakini ninachosisitiza ni kuona ni namna gani ambapo sisi kama Bunge tunaweza kushirikiana kurekebisha bajeti iliyoko hapa ili tuokoe pia tatizo ambalo ni la Taifa na siyo tatizo la eneo moja moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo, nashauri kwamba tunapokwenda kuhitimisha mgawanyo wa mafungu huko mbele ya safari, tutafakari suala la kuwezesha upatikanaji wa madawati kwa kurekebisha bajeti zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine mimi niko kwenye Kamati ya Sheria Ndogo. Tumemsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu jana ameliarifu Taifa habari njema sana, kwamba sasa wameongeza *threshold* ya Mamlaka ya Halmashauri kupitia vitengo vyao vya sheria kwa maana ya ile mikataba kwamba sasa Halmashauri zote zishughulikie mikataba yote isipokuwa inayozidi kuanzia shilingi bilioni moja na kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba eneo hili tulipe uzito, tukiwezeshe kitengo cha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na hasa Wanasheria walioko katika Halmashauri zetu. Tunaofanya nao kazi, tunaona udhaifu ulioko pale, lakini wakati mwingine ni kwa sababu ya matatizo ya kibajeti. Kwa hiyo,

ninachoshauri hapa ni kwamba bajeti yao tuiongeze kwa Kitengo cha Sheria kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili wanasheria walio kule kwenye Halmashauri zetu waweze kufanya kazi zao vizuri zaidi. Siyo zaidi ya hapo tu, pia kuongeza ikama ya Watumishi katika Halmashauri zetu. Tukifanya hivyo tutafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamesemwa sana kuhusu utawala bora, lakini naungana na Watanzania walio wengi kuunga mkono hatua zote zinazochukuliwa na Mheshimiwa Magufuli kwa sasa kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuliweka sawa Taifa letu. Historia inaonyesha, nchi zote duniani ambazo zimefanikiwa kupata maendeleo ya kasi, zimepitia vipindi vigumu lakini pia baadhi ya hatua zilizochukuliwa na viongozi wao wa kitaifa ni pamoja na hizi ambazo amechukua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, nitatolea mfano wa nchi ya Singapore. Wote tunafahamu wanaofuatilia historia. Yule Waziri Mkuu wao wa kwanza aliyeiongoza ile nchi kwa miaka 31, yule Lee Kuan Yew aliongoza toka mwaka 1959 mpaka mwaka 1990. Mojawapo ya changamoto alizokutana nazo kipindi kile ni wakati ambapo walivunja muungano wao na nchi ya Malaysia wa mwaka 1965, ni muungano uliodumu kwa miaka miwili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuvunjika, Waziri Mkuu Yew alipata shida sana kutafakari nini kitafuatia, kwa sababu ni nchi ndogo ambayo ukubwa wake ni sawa sawa na nusu tu ya Jiji la London. Alijiuliza kwa sababu walikuwa hawajajiandaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zinazochukuliwa leo na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ni kwa ajili ya manufaa ya Taifa hili. Nazungumza haya bila kubeza na kwa namna yoyote ile bila kudharau kazi iliyofanywa na watangulizi wake.

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba ni kengele ya kwanza hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya bila kubeza kazi iliyofanywa na watangulizi wa Mheshimiwa Rais wa Awamu Tano, lakini kwa hakika Taifa tulipokuwa tumefikia na sisi wote ni mashuhuda, Taifa hili linahitaji kuumbwa upya. Tunalifinyanga upya ili tusonge mbele kwa pamoja. Kama alivyofanya Waziri Mkuu wa Singapore, Taifa hili linahitaji juhudi hizo. Waziri Mkuu wa Singapore yule baada ya ule muungano wa Malaysia kuvunjika, alijifungia wiki sita, akaenda Kisiwani kule akakata simu hakuwa na mawasiliano na Baraza

lake la Mawaziri, hakuwa na mawasiliano na Wabunge wenzake, akasema yeye anajifungia kutafakari mustakabali wa Taifa lile.

Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya kuapishwa, aliendesha hii nchi pamoja na Waziri Mkuu kama jeshi la mtu mmoja, akitafakari mustakabali wa Taifa hili. Hatua zinazochukuliwa leo zisitufanye sisi kama Taifa kutoka njia kuu. Tunafahamu hapa wapo watu wanalalamika kwamba hatua anazozichukua zinazidi kiwango, lakini fikiria yanayotokea! Soma taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali, yanayosemwa haya, ni nini kifanyike kudhibiti? Kwahiyo, naungana na wenzangu na ninawashawishi wenzangu kwamba tuungane pamoja kumuunga mkono Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia habari za wenzetu kusema Ibara ya 18 ya Katiba imevunjwa. Tuache kuwapotosha wananchi. Kinachosemwa kwenye Ibara ya 18 hapa, ni wananchi kupata kuwa na haki ya kupata taarifa, utaratibu umeandaliwa na Bunge hili. Kilichobadilika ni ratiba tu. Kwa nini tunang'ang'nia *live?* Kuna haki gani inayosemwa "*live*" katika Katiba yetu? Hakuna haki *live* inayooneshwa katika Katiba yetu. Kwa nini hawa wenzetu wanapiga kelele? Mambo mengine yanakatisha tamaa sana. *(Makofi/Kelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma ukurasa wa 17 wa taarifa ya wenzetu, wanasema Serikali isafishe mtandao wa ufisadi uliojengwa na Wakurugenzi wa Halmashauri na wahasibu wao wa kutoa *tender* kwa upendeleo. Unalikuta jambo hili limeandikwa katika taarifa ambayo inawasilishwa hapa na inajenga historia ya maamuzi na mapendekezo yanayotolewa na Kambi ya Upinzani. Ni jambo la aibu! Kwa sababu jambo hili la *tender* kutolewa, sisi Waheshimiwa Wabunge hapa ni sehemu ya Madiwani kule, ni jambo la kusimamia sisi; siyo jambo la kuja kulalamika hapa. Unamlalamikia nani? Kama ni udhaifu wa Halmashauri yenu, ni wa kwenu. Miongozo na taratibu zipo wazi hapa! *(Makofi)*

Mhesimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema tu kwamba tusiwapotoshe Watanzania kwa sababu ya hasira tulizonazo. Wote tunafahamu tulivyokumbushwa, huu mchezo hauhitaji hasira, ni lazima uwe tayari. Ukiwa na hasira utapata taabu kidogo, kwa sababu ya mambo yanavyokwenda. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Kicheko/Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Ngonyani! *(Makofi/Kelele)*

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja asilimia mia moja. Hii Serikali yetu wote, tunatakiwa tuwaunge mkono kwa kila kona katika matukio yote wanayoyafanya kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. Ila nilete kwako masikitiko yangu makubwa kutokana na kitendo alichonionesha Mheshimiwa Naibu Waziri asubuhi. Sikutarajia kama ningepata majibu ya namna ile, lakini nataka nimwambie kwenye siku ya Wizara yake, shilingi yangu hataiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona nimeleta maneno hapa Bungeni, maana yake ni kwamba kule Wakurugenzi, watumishi wa Halmashauri wameshindwa kuyafanya yale mambo, ndiyo maana nayaleta hapa ili nipate msaada zaidi. Kuna lugha nzuri za kuweza kutufanya sisi ambao tunatumwa na wananchi tuyalete hapa ili mtuelekeze ni namna gani ya kwenda kuongea na wananchi watusikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu, Wakurugenzi zaidi ya tano; toka nimeingia Bungeni, Wakurugenzi kwangu wanakaa miezi sita sita, hii taarifa ya ardhi wao wataipata wapi? Muda wa kukusanya habari, wao watazipata wapi? Mkurugenzi akikaa miezi sita kaondolewa; akikaa mwaka mmoja, kaondolewa! Kuna watumishi wengine wanakaa miaka, hawaondolewi! Sasa narudi kwenye hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwenye upande wa TAMISEMI. Naomba kwanza wafanye marekebisho ya Sheria ya Manunuzi. Hapa tutakuwa tunadanganyana, hakuna Mbunge anayeingia hapa kuangalia kwenye ile Kamati ya Sheria ya Manunuzi, Wabunge wote tunakaa nje. Wanayojadili mpaka kununua vitu, wananunua watumishi wa Halmashauri, sasa sisi Wabunge tunakwenda pale, tunaambiwa Jimbo lako halifanyi kazi. Kama leo kujenga nyumba inaandaliwa na watumishi wa Halmshauri, unaambiwa shilingi milioni 35, wewe Mbunge hushirikishwi, halafu tunakuja huku tunaambiwa sisi ni mafisadi, ufisadi wetu unaletwa na nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuangaliane kwamba Sheria ya Manunuzi ikirekebishwa na sisi Wabunge tunaingia pale tunatoa hoja zetu. Tukiona mahali hapaendani na jinsi ilivyo, tunapinga. Sasa sisi Wabunge tunakuja kulalamikia Bungeni, kule hakuna mahali tunaingia. Eti wataalam ndio wanakaa, wanamtafuta mkandarasi, wanamweka pale, ananunua vitu; nyumba ya kujenga shilingi milioni 30 anajenga kwa shilingi milioni 90, wewe Mbunge utalalamikia wapi? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nasikitika, tunaletewa hela sana na Serikali, lakini zinaletwa siku za mwisho mwisho. Ikifika siku ya mwezi wa saba tarehe 1, hela zinatakiwa zirudi huko. Kwa nini hizi hela kama mnatuamini

mnatuletea, zisibaki Halmashauri ili wananchi wakaendeleza ile miradi ambayo ilikwama kwasababu hela zilikuwa hazipatikani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaashangaa hela zinakuja; Serikali haiwezi kukusanya hela kwa wakati mmoja na ikagawa kwa sehemu moja. Hela ni lazima igawanywe kwa kila sehemu. Wanasema kakondoo kadogo kanaliwa na kila mtu, sasa lazima kila sehemu zipewe lakini inafika mahali kwamba tunaletewa pesa zile, baada ya siku mbili unaambiwa hela zinatakiwa zirudi Hazina; hazijafanya kazi yoyote, hatujapanga mikakati ya aina yoyote, halafu leo tunakuja kulaumiwa kwamba Wabunge hatusimamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili suala Mheshimiwa waziri utakapokuja tueleze; kama hela mnaamini; mimi naamini Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Pombe Magufuli hakuna mahali mtu atapita kuchukua hata thumni kwa jinsi mlivyojipanga safari hii Mawaziri wetu. Mmnejipanga vizuri, mnafanya kazi vizuri na watendaji wenu ni wazuri. Sasa kama Watendaji ni wazuri, mna wasiwasi gani hela zisibaki Halmashauri? Mimi kwangu zilikuja hela za maji, Benki ya Dunia, mabomba yametengenezwa, hayakwisha, lakini hela zinatakiwa zirudi, zinakwenda kufanya kazi gani? Kama zililetwa kwa ajili ya Watanzania na Serikali ya Tanzania itazilipa fedha zile, kwa nini zisibaki pale ili tukijua kwamba zimebaki pale, ziendeleze miradi mingine ya maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niseme kwasababu sasa hivi kuna hospitali, tuna zahanati nyingi ambazo tuliziahidi kwamba zitaboreshwa, mpaka sasa hivi hatujaboresha. Tulikuwa tunaomba vilevile maabara, wananchi wamechangishwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yangu tukufu tuongeze mtaji ili zile maabara ambazo wananchi walijitolea kwa nguvu ili mwongeze hata ka-*percent* kidogo wananchi waone Serikali yao inavyofanya kazi, kwasababu Serikali hii ni sikivu na kama Serikali ni sikivu, lazima tuwe kwa kila kona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kuna suala la Mombo. Mombo toka mwaka juzi ilikuwa iwe Halmashauri, lakini kila siku naomba katika Ufalme wako Mheshimiwa Waziri na hilo naomba uliangalie sana. Niko chini ya miguu yako, Mombo. Katika vitu ambavyo vinaumiza kichwa wananchi wa Korogwe Vijijini, Mombo, iweke iwe Halmashauri ya Mji. Watu tumezunguka kila kitu tumefanya tumefanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye utawala bora. Ukimkuta mtu anawasema watu wa TAKUKURU akili yake kidogo imepungua, wanafanya kazi sana. Ukimkuta mtu anasema watu wa Kamati ya Maadili, wanafanya kazi sana. Naomba tuboreshe ofisi zao, naomba tuwape nguvu, naomba badala ya kupitia kwa Mkurugenzi wa Mashitaka, wapewe ruhusa, wao wenyewe

wapeleke watu mahakamani. Tunaogopa nini? Kama mtu huna tatizo ambalo umelifanya, wao mpaka kesi waichukue, waijadili, waichunguze wakishaichunguza halafu inapelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashitaka. Sasa kama hamwaamini, mliwapa kazi za nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maadili wanafanya kazi. Juzi nilikwenda Kibaha, nimeangalia Ofisi ya Maadili ya Kibaha, utafikiria ni nyumba ya Mganga wa Kienyeji, tena ni nyumba ya kukodi na wakati watu wanafanya kazi kuhusu maadili yenu kuwa mazuri! Kwa nini tusiwaboreshee ofisi zao na kila Mkoa kukawa na ofisi? Wanapokuwa wanafanya kazi na ukiwawekea ofisi nzuri, nao wanakuwa nguvu ya kufanya kazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa usalama. Leo hii Usalama wa Taifa tunatakiwa tuwaongeze posho, kwa sababu wanapofanya kazi ni kwa ajili ya maslahi ya Watanzania. Ninyi hamjakaa Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekaa Kenya miaka 15. Kuna wakati Mtanzania analala saa 6.00, kwa nini? Kwa sababu usalama wao ni mdogo. Leo hapa Tanzania watu wa usalama wanafanya kazi vizuri, tunawaangalia, hatuwapi matumaini, tena tukiwaona tunawadharau. Tusifanye kazi kwa mazoea. Tufanye kazi kama Mheshimiwa Pombe Magufuli anavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona niyaseme haya kwasababu hii ndiyo demokrasia yetu. Mheshimiwa Lukuvi ni rafiki yangu, siondoi shilingi hata siku moja, wala siwezi kuipinga Serikali yangu. Kwa hiyo, kukwambia kwamba nitakuja kuondoa shilingi, siondoi tena naunga mkono moja kwa moja.

MWENYEKITI: Ongea na Kiti Mheshimiwa. Ongea na Kiti!

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mtuunge mkono sisi Wabunge. Tunakaa katika mazingira magumu sana huko vijijini. Mnapokuwa katika Bunge hili, mjue kwamba ninyi wote ni Wabunge kama sisi. Angalieni kauli za kutujibu. Itafika mahali na sisi tutaonekana kama watu ambao tumetoka nje ya Bunge hili; na hatupendezewi, hatufurahishwi tuonekane kama Wabunge tumekuja hapa kujipendekeza au kupendeza baadhi ya watu, tuonekane tunaiponda Serikali yetu. Serikali yetu ni sikivu, inafanya kazi vizuri, Mawaziri safari hii ni Wazuri, naomba muendelee kutujali na kututhamini katika majibu yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape nafasi wengine; nakushukuru kwanza wewe binafsi kwa kukuomba ombi langu kwamba naumwa sana mguu niasidie na umenikubalia, Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Dunstan Kitandula; halafu nibadilishe kidogo tu, atafuatwa na Mheshimiwa Lusinde, halafu Mheshimiwa Vullu.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili nami nipate wasaa wa kuchangia kwenye Bajeti iliyoko mbele yetu. Namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma kwa kunipa tunu ya uhai. Kwa namna ya kipekee niwashukuru wananchi wa Mkinga kwa heshima waliyonipa ya kuwa mtumishi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kugusia eneo la afya. Mwezi Februari, tulizindua taarifa ya tathmini ya utoaji wa huduma za afya nchini. Taarifa ile ukisoma inakupa matumaini kweli kweli. Ni taarifa inayosema kwenye vituo vya afya vya *private sector*, huduma za afya za mtoto zinatolewa kwa asilimia 80, lakini kwenye vituo vya Serikali huduma za kisasa za huduma ya mama na mtoto zinatolewa kwa asilimia 97. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali lakini napongeza yale yaliyomo kwenye taarifa ile. Nilipokuwa nikiisoma taarifa ile nikasema hapa barabara, kwenye suala la *universal health* tunakwenda vizuri; lakini nikapata mashaka makubwa nilipokuja kuiona hotuba. Nilipokwenda ukurasa wa 32, ukajaribu kunionyesha mambo tofauti. Ukurasa ule utuambia katika Halmashauri 181, Halmashauri 84 ndiyo zina hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri 97 zinapata kudra ya Mwenyezi Mungu ya huduma kutoka kwa Taasisi za Mashirika ya Dini na kadhalika. Hili likanishtua kwa sababu Mkinga leo hii tunapozungumza, Wilaya iliyoanza mwaka 2005 na kupata hadhi ya kuwa Halmashauri mwaka 2007 mpaka leo hatuna Hospitali ya Wilaya. Tunapata huduma kutoka Tanga kwenye Hospitali ya Bombo, tunapata huduma kwenye Hospitali ya Wilaya ya Muheza. Tumekuwa tukitenga kwenye bajeti fedha kwa ajili ya ujenzi tangu mwaka 2011, fedha haziji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndani utaambiwa kwamba nendeni mkatenge kwenye bajeti. Tunatenga, fedha haziji! Tusaidieni! Tusaidieni ili watu wetu waweze kupata huduma hizi, maana Serikali ina wajibu wa kulinda maisha ya watu wake. Wananchi wametuamini, tuwatendee haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hotuba hii ukurasa wa 32 ule, unatuonyesha kwamba tunatakiwa kuwa na *direction* mpya ya kuhudumia mambo. *Sweeping statement* kwamba tunataka kila kijiji kiwe na zahanati, tunataka kila kata iwe na kituo cha afya, pekee haitoshi tunatakiwa tufanye zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zile ukiziangalia zinaogopesha! Vituo vya afya 484 katika kata 3,506. Maana yake, tumeweza kujenga vituo vya afya 12% tu katika maeneo yetu, hii haikubaliki hata kidogo! Tuna vijiji 12,500 na kitu, vijiji 8,043 havina zahanati. Maana yake nini? Maana yake tumeweza kupeleka huduma hii kwenye vijiji siyo zaidi ya asilimia 36. Lazima tubadilike! Mkakati wetu wa kutufikisha kwenye kutoa huduma hizi una walakini. Mawaziri mliopo kwenye Wizara hizi, tunawaamini, tunaamini mtatoa uongozi utakaotutoa hapa twende mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Nataka ni-*declare interest*, mimi nimetoka kwenye huduma hizi za fedha. Kumbukumbu zangu zinanionyesha, zimekuwepo jitihada mbalimbali za kupelekea huduma za kifedha kwa wananchi, kuwawezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbukumbu zangu za haraka haraka zinaniambia tumekuwa na miradi takribani 17 yenye lengo la kutoa huduma za kifedha kwa wananchi. Utazungumzia *SELF*, utazungumzia *PRIDE*, utazungumzia mradi wa huduma za kifedha vijijini, utazungumzia miradi ya vijana; miradi karibu 16, yote hii inafanyika kwa lengo zuri la kuwawezesha wananchi, lakini changamoto tuliyonayo, mitaji hiyo haitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja na Shilingi milioni 50 hizi kwa kila kijiji; tusiende kichwa kichwa. Wapo wenzetu walikwenda hivi wakaumia. Uganda walianzisha mradi wa namna hii wakiuita *Entandikwa*. Mwaka 2000 nilikuwa Uganda nikaenda kuungalia, *repayment 0%,* hakuna hela ilirudi. Wenzetu wa Thailand walifanya kitu cha namna hii, lakini wao walikuwa makini kidogo, mambo yao yamekwenda vizuri. Tusiwe na haraka ya kutoa fedha hizi bila ya kuwa na utaratibu makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mifumo yetu ya kifedha, Bunge lililopita tulikuwa tunalalamika hapa, tunasema tupewe mitaji ya kuwezesha kuanzisha *community bank*. Leo hii *community bank* ukitaka kuianzisha, unazungumzia shilingi bilioni mbili. Kama tungekuwa makini, tungeweza kujipanga. Mimi nina vijiji 85, ukiniambia unapeleka shilingi milioni 50 kwenye kila kijiji, ni shilingi bilioni nne na kitu. Ningeweza kukwambia peleka Shilingi bilioni mbili ifunguliwe *community bank* ambayo kila mwananchi katika Wilaya yangu atakuwa na hisa kwenye benki hiyo na hizi fedha nyingine tuweze kuzikopesha. Tungekuwa na uhakika kwamba fedha hizi zitawafikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeambiwa mtakuwa na *pilot* katika kugawa fedha hizi. Twendeni kwenye hiyo *pilot,* lakini tuangalie vile vile uwezekano wa kuanzisha *community bank* kupitia fedha hizi. Wale tutakaoweza kuwa na *regional bank,* tukikubaliana mimi na Mheshimiwa January na wenzangu wengine wa Tanga tuwe na *regional bank* katika Mkoa

wa Tanga, tukikubali kwamba mafungu yatoke kwenye fedha hizo ambayo inafikia shilingi bilioni tano kwa kuwa na *regional bank,* mtukubalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji. Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga hayana maji. Kuna mradi pale tumebuni chanzo cha Kinyatu, tumeambiwa tutapata ufadhili wa Benki ya Dunia. Tumepeleka maandiko yanayotakiwa tupate mshauri mwelekezi tangu mwaka 2011, hakuna kitu! Tusaidieni watu wa Mkinga tupate huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Kitandula. Mheshimiwa Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Vullu.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo na mimi niweze kusema mambo machache ya muhimu kuhusu hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kaka yangu Mheshimiwa George Boniface Simbachawene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais ameonesha namna gani anataka kuirudisha Tanzania kwenye msimamo hasa wa nidhamu, uwajibikaji na uadilifu. Kwa sisi Wagogo tuna usemi unasema; *mdabula nhili mwana na kalanga ganyina mmeso.* Ukitaka kuonja uji wa mtoto, mtazame kwanza mama yake usoni. Ukimwona namna alivyokaa, unaweza ukaamua aidha, uonje au usionje. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Magufuli ameonesha yuko makini na mkali sana kwenye matumizi ya hovyo hovyo. Nataka niseme haya mnayoyaona wengine kushindwa kumwelewa ni kwa sababu Rais Magufuli amewashangaza wengi katika utendaji wake wa kazi. Ndiyo maana mtasikia mengi! Mtasikia Katiba imevunjwa, mtasikia nini! Kwa sababu wengine hawana namna ya kusema, inabidi waseme hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Waziri, tunakufahamu kwa msimamo wako Mheshimiwa Simbachawene. Tuna hakika utaitendea haki kama ambavyo umeonesha tangu mwanzo Wizara hiyo, ni Wizara kubwa, tuna hakika mkijipanga vizuri na Jafo kama mlivyokaa, mna uwezo wa kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele. Tunawapa *big up,* tunawaomba mwendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme maneno machache hapa. Tunapozungumzia pengine kuna mtu hapa ameshindwa kuelewa anasema Mwanasheria Mkuu wa Serikali anatafsiri mambo ki-CCM. Ndugu zangu, nchi hii Ilani inayotekelezwa ni ya CCM. Nchi hii hakuna Sera ya Serikali peke yake tu inayojiendesha! Mlikataa wakati wa Bunge la Katiba. Tulipowaambia tuwe na Sera ya Serikali tuachane na Sera za Vyama, mkakataa! Leo tumeenda kuuza sera kwa wananchi; CHADEMA walikwenda nayo, *CUF* walikwenda nayo na CCM walikwenda nayo. Wananchi wamechagua ya CCM. Sasa mtu anaposema unaongea ki-CCM hata wewe Mbunge unatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Tuelewane hapo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala tusitake kuzungumza hapa vitu kama vile tunaimbiana mapambio. Upinzani watakuwa wanafanya kazi kama vile ambavyo tunaweza tukasema, wanafanya kazi waki-*support* kazi ya shetani, kwamba unapinga lakini wenzako wanaotawala wanafanya kazi ya Mungu. Wakati unaeleza upungufu, kwanza unashukuru kwa vichache vilivyotolewa. Hawa kazi yao ni kuponda, halafu baadaye wanaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kazi yetu ni kusifu baadaye tunaomba. Wote kazi yetu ni moja, lakini utajiuliza mwenyewe, je, wa kuponda anafurahisha? Maana kwanza anaponda, halafu baadaye anapiga mzinga. Sisi tunasifu baadaye tunapiga mzinga. Kwa hiyo, tunafanya kazi ya Kimungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namwomba Mungu sana, anipe uwezo watu wanielewe. Sitaki kuingia kule kwenye siasa ambazo watu wamepanga; anasema tu kwa sababu Lusinde tumemwona, yeye anataka kuhamisha vita kutoka kwa Mawaziri kuja kwake; tutampakazia! Wewe useme kwamba Lusinde amepigiwa simu ya Mheshimiwa Rais, kaambiwa asiwatetee. Mimi Wakili? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo Wakili, sifanyi kazi ya Mahakama na wala simtetei mtu yeyote katika Mahakama yoyote ya nchi hii. Kwa hiyo, unaweza ukaona; na mimi nataka niwaambieni mkitaka kuleta siasa za uzushi mimi ndiyo natisha kwenye upande huo. *(Makofi)*

Nirudie tena kuwaonya, mimi mtu kunitaja namruhusu kwasababu hili jina kubwa na nimelitengeneza kwa gharama kubwa. Kwa hiyo, kuna watu watajitahidi kutaka kulifikia jina hili, lakini ni kazi ngumu sana. Waitara nimemfundisha siasa akiwa CCM, leo tena yuko CHADEMA nitaendelea kumsaidia taratibu lakini asifikie huko; Rais ni matawi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, humu ndani tunafanya kazi mbili tofauti. Wako Wabunge ambao kazi yao tangu anasimama mwanzo, ataponda halafu mwishoni anakuja kwenye kiti, nisaidie maji. Yupo Mbunge

atasimama, atasifu halafu baadaye atatoa shida zake. Ndiyo tofauti! Ninyi Mawaziri mtapima, yupi anayezungumza vitu vya msingi? Mtapima maana mimi siamini, hata kutafuta mchumba umkute msichana wa watu, umwambie dada una sura mbaya, lakini naomba nikuoe. Akikubali, ujue huyo hana akili. Hana akili huyo! Lazima umsifu kwanza! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewaeleza juzi kwa uchungu sana, nikasema nchi yetu tunajenga demokrasia, tuangalie kwa umakini sana. Hii nchi inapita kwenye mawimbi makubwa ya kujengwa demokrasia. Tunapojenga demokrasia, ni lazima hivi vyama tuvipe uhuru mkubwa wa kufanya mambo yao kama ambavyo tunafanya. Ndiyo maana nikawashtua wenzangu, Chama cha *CUF*, nikawashtua NCCR Mageuzi; siamini kwamba katika ndoa waliyonayo wanajenga demokrasia. Naamini wanakwenda kuuawa! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaweza kumwona Mheshimiwa Zitto hana akili, yuko peke yake, lakini nawaambia katika miaka ijayo, pengine chama chake ndiyo kitakuwa maarufu kuliko vyama vingine hivyo. Maana kinapata muda wa kufanya siasa. Leo kuna watu wanazuiwa na Mwenyekiti, usiseme; wanakaa kimya. Sema, wanasema! Watu wa namna hii ni watu wanaoendeshwa kwa *remote,* hawawezi kuwa wanasiasa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia Tanzania ina Chama cha Upinzani pengine kimoja tu, *ACT,* vingine vyote ni vyama shindikizo. Ni Vyama vinavyokwenda na hoja. Meli ikizama, wanahamia kwenye meli; ikitokea kashfa, wanahamia kwenye kashfa. Serikali hii inaziba kila kitu. Wamehamia kwenye *tv live*. Hebu ngoja nizungumze kidogo hapa! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi wasomi mnasema nchi ina *Executive*, *Parliament* na *Judiciary*, hebu tujiulize; mbona *Executive* mambo yao hayaoneshwi *live* kila siku? Nayo ndiyo *Executive* inayoongoza nchi! Mbona hatuoni *live* kila siku mambo ya Ikulu? Mbona hatuoni Mahakimu wakiendesha kesi *live* kila siku na wao ni mhimili? Mbona hatuoni Majaji Mahakamani wakiamua mashauri wakiwa *live* na wao ni mhimili? Iweje watu wang'ang'anie mhimili mmoja? Huku ni kufilisika! Watu wamefilisika, hawana nafasi, wanataka kwenda kujitangaza kwa njia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema leo nitoe somo. Katika nchi yenye mfumo wa vyama vingi tuangalie hivi vyama, tuangalie hata aina ya Wabunge. Mimi nawaambia tutakwenda mahali tutajikuta tunatumia *resource* kubwa, kupoteza muda hapa, hatuisaidii Serikali. Kwa hiyo, naomba niwaambie Waheshimiwa Mawaziri, tunapokuja kuwaambia shida zetu na juzi nilisema, hapa mnatukanwa, mnadharauliwa, halafu wakija wanasema naomba maji. Leo nchi ielewe hakuna Jimbo lolote la mpinzani linalopelekwa maendeleo. Maendeleo katika Majimbo yao tunapeleka sisi CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ndio tunakubali bajeti itekelezwe. Leo tunamwomba Waziri wa maji apeleke maji Moshi, Arusha; Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa huo wanakataa. Mwisho wa siku wanasema tumeleta maendeleo. Unaleta maendeleo kwa kusema hapana? Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ifahamu maendeleo yanaletwa na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Ndiyo tunaopambana! Naona Mheshimiwa Msigwa sindano tayari. *(Makofi/Kicheko)*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Aah, niendelee! Niliona Mheshimiwa Mch. Msigwa amesimama nami namheshimu kwa sababu nimeoa kwao. Unajua mimi nimeoa Iringa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watu waelewe hata barabara zilizojengwa Iringa Mjini aliposimama Mheshimiwa Msigwa, mimi nilitetea humu ndani ya Bunge. Maana mke wangu anatoka pale. *(Makofi)*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu!

KUHUSU UTARATIBU

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu! Hebu Mheshimiwa Lusinde keti. Kuhusu utaratibu, Kifungu gani?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Kifungu 68 (7). *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Tisini na ngapi?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: 68(7). *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Nisomee.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Naomba hiyo Kanuni.

MWENYEKITI: Tusomee.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimwa Mwenyekiti 68(8). *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimwa Msigwa, umeomba utaratibu. Kuhusu Utaratibu...

MHE. MCH. PETER S MSIGWA: Ndiyo nasoma, 68(8).

MWENYEKITI: Kaa basi! Kaa kwanza. *(Kicheko/Makofi)*

Kuhusu utaratibu ni 68(1) wewe umesema 68(7). Sasa uliposema (8), inahusu Taarifa, siyo Utaratibu. Tunaendelea, Mheshimiwa Lusinde. *(Makofi)*

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru na nimshukuru hata Mheshimiwa Mch. Msigwa. Mheshimiwa Msigwa na mimi hatujawahi kupingana, sijui leo kimemkuta nini? Mimi juzi nimemwacha ameongea *propaganda* zake hapa, lakini leo yeye kashindwa kuvumilia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Waziri kupitia Bunge hili, aitazame Halmashauri mpya. Tumezungumza kuhusu mgawanyo wa nchi yetu. Tumeomba Halmashauri mpya ya Mtera, lakini atazame hata jina la Jimbo la Mtera. Kata ya Mtera iko kwako, Kijiji cha Mtera kiko kwako, mimi naitwaje Jimbo la Mtera? Haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikasema Mheshimiwa George hakuna sababu ya Jimbo langu kuitwa Jimbo la Mtera. Unanipa jina la utumwani. Mimi ningependa Jimbo langu liitwe Jimbo la Mvumi ambako anatoka Chifu Mazengo. Kwa hiyo, naomba Halmashauri yetu uitazame, Jimbo letu libadilishwe jina, lisiitwe jina la kijiji kilichoko kwako, kwa sababu sisi hatuwezi kuitika kwako. Watu wengi wanafikiri sisi tuko Mtera; Mtera ni ya George Simbachawene. Sielewi mzee alipoiita, aliita kwa sababu gani.

Mheshimiwa Mweyekiti, naomba kwenye Bunge hili uturudishie majina ya kwetu ya asili. Sisi pale tuna Mvumi karibu ziko 20. Kwa hiyo, ungetuita Jimbo la Mvumi ungekuwa umetutendea haki zaidi kuliko kutuita Jimbo la Mtera ambalo liko kwako wewe Mheshimiwa Simbachawene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tunaloliomba, kuna barabara za *TANROADS* na kuna barabara za Halmashauri. Halmashauri nyingi hazina uwezo wa kujenga barabara ndefu.

Kwa hiyo, naomba kwa niaba ya Wabunge wenzangu, angalia kila Jimbo lenye barabara ndefu, badala ya kuiachia Halmashauri ambayo haina uwezo, zipandishwe hadhi ziende *TANROADS* ili ziweze kutengenezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza hivi kwasababu tuna uzoefu; kuna barabara nyingine Halmashauri hazina mapato ya kuweza kutengeneza urefu wa hizo barabara, lakini mkiwapa *TANROADS* wana uwezo. Kwa mfano, chukulia barabara inayotoka Dodoma Mjini. Kuna barabara inatoka Dodoma Mjini, inapita moja kwa moja kwenye Jimbo la Bahi kwa Mheshimiwa Badwel, inaenda moja kwa moja tena kwenye Jimbo langu la Mtera, halafu ndiyo inaenda kupakana ng'ambo kule kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ile barabara tuipandishe hadhi iwe barabara ya Mkoa kwasababu inapita kwenye Manispaa na kwenye Halmashauri mbili. Ukipata hela Chamwino ukitengeneza kipande, wenzako Bahi wanakosa, panabaki mashimo; kunakuwa hakuna mtengenezaji. Kwa hiyo, naomba kupitia Wizara yako, barabara tulizoziombea zipandishwe hadhi, mzipandishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuangalie, kuna Halmashauri nyingine, kata nne Halmashauri; kata tatu Halmashauri; hebu tuangalie, sisi tuna Jimbo lina kata 22. Tumeomba tugawanywe Wilaya, mkasema hapana tutawapa Halmashauri. Tupeni Halmashauri ili tuweze kusukuma maendeleo mbele. Tunataka kuendelea kufanya kazi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tulisema…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Aaah, naendelea, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana…

MWENYEKITI: Mheshimiwa, umemaliza muda wako, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. Naona jamaa wanasema umemaliza. Ahsanteni, nimemaliza. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Vullu. Mheshimiwa Vullu, hayupo! Haya Mheshimiwa Rose Kamili Sukum. Tuna Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Naomba na mimi niwe mmojawapo wa kujadili hotuba na mpango wa bajeti wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Tawala za Mikoa na Utawala Bora, kinachonisikitisha ni kwamba kabla sijajadili kwanza habari ya bajeti, suala la utawala bora haupo kabisa kwa TAMISEMI. Upo kwa maandishi tu kusema

kwamba wanaridhika na kuhakikisha kwamba kwa wakati muafaka wananchi wanapata taarifa zao kwa ubora zaidi na pia kusimamia vyema utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, simlaumu sana Waziri wa TAMISEMI, bali namwambia kwamba watendaji wako au Maafisa Masuuli katika Halmashauri mbalimbali hawako vizuri. Wao hawatekelezi ipasavyo suala la utawala bora. Wananchi katika Halmashauri mbalimbali hawana taarifa kabisa hata ya miradi yao ya maendeleo; hawana taarifa ya fedha ambazo zinafikishwa huko, je, utawala bora hapo uko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine pia kwenye suala la utawala bora inatugusa sisi Wabunge wote wa Viti Maalum. Ninashindwa kuelewa huo waraka uliotolewa na Waziri wa wakati huo ambao siujui kwamba Wabunge wa Viti Maalum hawaruhusiwi kuingia kwenye Kamati ya Fedha ndani ya Halmashauri zao ambazo wanahudhuria. Hii inawagusa Wabunge wote, sio mimi peke yangu. Ni kwa nini hatuhudhurii hizo Kamati za Fedha? Naomba kutambua hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kairuki uko hapo, wewe ni mwanamke na ni Viti Maalum, umeteuliwa kuwa Waziri, kwanini sisi kama Wabunge hatuhudhurii kwenye Kamati za Fedha ambazo ziko kwenye Halmashauri zetu? Napenda kujua kwanini msibadilishe utaratibu huo ambao haufuati utawala bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imesababisha katika Halmashauri nyingi, saa nyingine Waheshimiwa Wabunge hawaingii. Mbunge wa Viti Maalum angekuwepo maeneo hayo, ni wazi kabisa angekuwa mdhibiti wa fedha na mali ya Halmashauri yetu husika au mali ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la utawala bora pia naomba sana TAMISEMI kubadilisha taratibu kuhusu Wenyeviti wa Vijiji na Serikali yao kuweza kupewa posho au angalau hata msharaha kidogo ili waweze kufanya kazi vizuri kusimamia miradi ya maendeleo kwenye vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye suala la Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhusu kuomba tuidhinishe makadirio ya shilingi trilioni 6.023 kwa ajili ya mpango wa maendeleo na makadirio ya fedha kwa mwaka huu wa 2016/2017. Mishahara tu pamoja na matumizi mengineyo imekwenda kiasi cha shilingi trilioni 4.4 lakini fedha za maendeleo ni shilingi trilioni 1.6 tu! Ukigawanya hizi fedha za maendeleo kwa Mikoa 26, kwa Wilaya 139, kwa Tarafa 562, kwa Kata 3,963, kwa Mitaa 4,037 kwa vijiji 12,545 na Vitongoji 64,677 maana yake wastani wake kwa ujumla, kila timu itapata shilingi 18,663,609.95 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu mwangalie kwenye suala la maendeleo kama hizi fedha zinakidhi haja. Kwenye taarifa yao ya fedha wameonesha kwamba wamepewa mikoa kadhaa, wamepewa vijiji kadhaa au wamepewa Wilaya kadhaa. Ina maana fedha za maendeleo hazitoshi hata kidogo! Mimi nadhani ifikie mahali sasa kwamba sisi kama Wabunge waangalie TAMISEMI waweze kupata fedha za kutosha. Ili waweze kukidhi haja ya wananchi kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilienda mbali kidogo kuhakikisha kwamba hebu hata hizi fedha za maendeleo zimekwendaje? Nikachambua programu za maendeleo kadhaa. Nikaenda kwenye programu ya maendeleo ya barabara vijijini, kasma ya 4,170. Unakuta kwamba wameomba fedha shilingi bilioni 224.7, hizi hela ukiangalia kazi yake ni kuratibu na kutekeleza mpango, kufungua barabara za vijijini ambazo hazipitiki ambayo hela yake sasa ukiangalia kwenye mchanguo huoni ni vijiji gani ambavyo wanastahili kufungua hizo barabara na ni hela kiasi gani haikuoneshwa?

Pia kwenye matengenezo ya barabara maeneo ambayo ni korofi kwenye barabara za Halmashuri, haioneshi ni barabara za Halmashauri gani, ni barabara ya wapi ni ya kijiji gani, haioneshwi kabisa. Sasa sisi kama Wabunge tunaidhinisha nini? Tunatakiwa tujue, tuidhinishe kitu ambacho tunajua, kama inaenda kwenye Wilaya ile au kama inaenda kwenye Halmashauri fulani, basi ifahamike kwamba ni Halmashauri kadhaa safari hii wamepata, labda ninyi mkapate mwaka 2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuangalie kwa undani. Pia nilienda moja kwa moja kwenye programu nyingine ambayo ni kasma ya 3,280, programu ya maji safi na usafi wa mazingira vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiit, fedha zimeombwa kuidhinishwa, ni shilingi milioni 412 tu! Hatuna maji, hatuna fedha za kutosha kwenye Halmashauri zetu, hatuna visima. Leo ni shilingi milioni 412, ni kufanya ufuatiliaji wa miradi, tathmini, kuratibu shughuli na kuratibu vikao vya kitaalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunahitaji vikao vya kitaalam au tunataka visima vya maji? Sasa tunapitisha nini? Naomba mkarekebishe hapa! Tena fedha zenyewe zinatoka nje, fedha za ndani hazipo. Tunafanyaje? Miradi itaendeleaje? Ina maana kwamba Watanzania bado wataendelea kukosa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea Hanang. Wana-Hanang tuna upungufu mkubwa sana wa maji. Hata fedha ulizozipeleka Mheshimiwa Waziri safari iliyopita, hakuna maji. Unaenda Gehandu, hakuna maji; sijui Galangala, hakuna maji na fedha nyingi zimeenda; unaenda Garoji, hakuna maji. Hata

Mjini Katesh yale maji ambayo yametengenezwa na Mfuko wa Rais nayo hayapo saa hizi. Visima vipo tu kama sanamu. Kwa hiyo, watu wanaenda kuabudu sanamu, hakuna maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri lazima hilo mliangalie pia kwa upande wa TAMISEMI, mtafanya nini kuhusu masuala ya maji na fedha hizi tunazoziidhinisha sasa hivi, shilingi milioni 412, kweli ni za kufuatilia au tunahitaji visima vya kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitishwa na suala la elimu. Ukiangalia, tunasema kwamba tunapata elimu bure, kupunguza tu ile ada, lakini michango ni mikubwa sana. Nafikiri ifikie mahali sasa TAMISEMI tuangalie suala la michango ile ya ziada ambayo itawasaidia wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mbunge amesema watu walikuwa wanakwenda na maakuli, chakula cha nyumbani. Kipindi hiki magonjwa yako mengi, mwanafunzi hawezi kwenda na chakula kutoka nyumbani kwao. Kitakuwepo kipindupindu, sijui na ugonjwa gani sijui na kitu gani; inatakiwa wanafunzi wale mahali pamoja. Mimi nadhani sasa Serikali ifikie mahali kwamba muangalie suala la chakula shuleni, itolewe na Serikali. Hiyo ndiyo kupunguza adha kwa wazazi kwa ajili ya wanafunzi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kikubwa zaidi ni hela za MMES. Huu mpango wa hela za MMES na MMEM, tunaomba mwangalie utaratibu wa hela za MMEM na MMES. Siyo kupitia tena kwa Wakurugenzi, halafu eti Mtendaji wa Kata ndio anasimamia hizo hela. Ziende moja kwa moja kwenye shule. Sasa zinavyoacha kwenda kwenye shule, wengine wanaanza kumega kidogo kidogo ambapo ukifika, hazipo shuleni tena kwa walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia suala la afya. Hospitali zetu hazina dawa, uchakachuaji umekuwa mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutumbua majipu, lakini nashindwa kuelewa, mnasema kwamba tusimtaje Mheshimiwa Rais hapa, huyu Mheshimiwa Rais anachelewa kutumbua Wakurugenzi kwenye Halmashauri zetu na wengine wanaokula fedha. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, atafuata Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitumie nafasi hii kukushukuru, kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kujielekeza katika elimu. Ni kweli kwamba tumeanzisha programu ya elimu bure; na kimsingi katika hili tunajua kabisa na ndiyo ilikuwa Sera ya CHADEMA kwamba inaenda kuwaondolea wananchi adha mbalimbali. Kuna maeneo ambayo tunataka kushauri na mkubaliane na sisi kama kweli tunataka kuboresha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ubaguzi uliopo katika mfumo wenyewe. Waraka uliotolewa ulionesha kwamba shule za *day* hawaruhusiwi kupata fedha za chakula kwa sababu wanafunzi wanakuja na kurudi nyumbani. Vilevile tufahamu kwamba ni mfumo ndiyo unabagua wanafunzi. Hakuna mwanafunzi anayependa kukaa *day*, wenzake walale *boarding* wasome usiku na watoto wa kike waende nyumbani wakaokote kuni. Ni mfumo! Sasa anapata hasara ya kukaa *day,* lakini bado anaenda shuleni mchana, hapati fedha ya chakula, lakini shule za bweni mnawapa fedha za chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Monduli, ni kweli shule zetu zote ni bweni, lakini ziko shule ambazo ni za *day* katika mazingira magumu. Tuache ubaguzi katika suala hilo, kama tunatoa hela za chakula, tutoe pia kwa wanafunzi wa *day* wakiwa shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tatizo la Shule za Sekondari za Serikali, siyo ada. Siyo shilingi 20,000, naamini wote tunafahamu hata Waziri wa elimu anafahamu. Tatizo siyo shilingi 20,000 kila mzazi angaweza kutoa shilingi 20,000. Tatizo ni mzingira hasa majengo, madarasa, madawati, vitabu, maabara na vitu vingine vinavyosaidia kuboresha elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sisi tuanenda kujificha kwenye kivuli cha shilingi 20,000 hatujawasaidia watoto wetu. Tutakuwa tunazalisha, kwamba tumeingiza watoto 2,000 darasani watatoka 2,000 lakini *empty*. Kwa sababu tunataka kuboresha kweli, tuache kwenda kujificha kwenye shilingi 20,000, twende katika kuboresha miundombinu ya wanafunzi, maabara na mazingira mengine yanayosaidia mtoto aweze kufanya vizuri, pamoja na vitabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tunafahamu kabisa kada ya Walimu ina mazingira magumu sana ya kufanyia kazi. Shule nyingi za kijijini na Wabunge wengi wanatoka kijijini watakubaliana nami katika hili. Walimu wanatembea kilometa nne mpaka tano kwenda shuleni, halafu wanatumia nauli shilingi 2,000,

shilingi 3,000 kila siku kwenda shuleni. Wakati huo huo anapanga mjini kwa sababu kule vijijini hata nyumba ya kupanga hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tunasema atumie mshahara wake kulipa nauli, atumie na kupanga nyumba, halafu unategemea wakati huo huo afanye vizuri, haiwezekani! Kama kweli tunataka kuboresha elimu yetu ni vizuri tukajali mazingira ya walimu kwa kujenga nyumba za Walimu katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wakati Waziri wa Elimu anawasilisha hapa, alisema kwamba ni kwa namna gani mwalimu anaweza akakaa kilometa tano au kumi kutoka shuleni akaondoka asubuhi nyumbani halafu akafanya vizuri na watoto wakafaulu. Tusiangalie watoto tu, lakini tuangalie mazingira ya watumishi wetu wanaofanya kazi katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka tukubaliane kama Bunge. Kama tunasema tunawapima watumishi wa umma kwa *OPRAS,* tuwapime Mawaziri nao kwa mfumo huo huo. Kabla hatujajadili bajeti yoyote katika miaka inayokuja, ni lazima Mawaziri na kila Wizara iwasilishe imetelekeleza kwa kiwango gani bajeti tuliyoipitisha kwa mwaka uliopita. Hii itatusaidia sisi Wabunge kuacha kupiga kelele hapa, kama tunapitisha bajeti ya bilioni tano, halafu Serikali haipeleki fedha, halafu tunakuja kumsulubu Mheshimiwa Waziri hapa, hakuna sababu ya kukaa kupitisha bajeti ambayo hatuwezi kuitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tatizo kubwa kwenye nchi yetu ni mfumo wa upelekaji wa fedha katika miradi ya maendeleo ya wananchi, ndiyo hiyo tu! Sasa kama tunapitisha bajeti lakini hatupeleki fedha, ni kila siku tunasigana hapa maswali, miongozo kwa sababu kile ambacho tumetarajia kupata kwenye Majimbo yetu, hatuyapati. Ni lazima tupige kelele kwa sababu hatujapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kama Serikali itapeleka fedha kwa wakati kwa kiwango kile hata kama ni kidogo, hakuna sababu ya Bunge kupoteza muda. Tungekuwa tunasema hapa tunashukuru kwa sababu tumetekelezewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hamjatekeleza, tutasema hamjatekeleza. Hii ni kwa sababu Serikali haipeleki fedha. Kwa hiyo, nashauri kila Wizara, wakati mwingine inavyopelekewa fedha kuwe na mgawanyo sawa wa kupeleka fedha wakati fedha zinapokusanywa. Siyo Wizara nyingine zinapewa, nyingine hazipewi. Bila hivyo, miradi yetu itaendelea kuwa haifanyi kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni wanyapori katika maeneo yanayopakana na Hifadhi za Taifa. Hili niseme kwa masikitiko makubwa. Katika

Jimbo langu mpaka sasa, tembo wanavamia kila siku zaidi ya heka kumi ya mazao ya wananchi, lakini haturuhusiwi kuwapiga wale wanyama. Baadaye nataka Waziri wa TAMISEMI kwa sababu tunasema tunahitaji kuwa na chakula, lakini wanyama wale wanaharibu sana mazao na wakati mwingine tunasema Serikali ishiriki basi kufanya *patrol* ya kuwarudisha wale wanyama kwenye *park* ili wananchi wetu waendelee kufanya kazi zao kwa amani, lakini haifanyiki hivyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine nitahamasisha kwamba ni bora Wabunge wanaotoka katika maeneo hayo tuungane kuwakataa wale wanyama, kama ninyi Serikali hamwezi kutusaidia kuwarudisha katika *park* hizo, badala ya kuwaacha waharibu mazao ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna magari; hakuna askari, kila siku iendayo kwa Mungu kuanzia mwezi wa tatu katika Jimbo langu, heka kumi zinaliwa na wanyama. Tembo wanavuruga, wanavunja. Ukienda Halmashauri hakuna gari. Kwa hiyo, tunaomba katika hilo mtusaidie ili wananchi wetu, jasho lao lisiende bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji. Mimi katika hili kwa kweli nimshukuru sana Waziri wa Maji kwa kufika Monduli. Baada ya kuingia kwenye Wizara hiyo, tumepata angalau shilingi milioni 700 kwa ajili ya kupunguza madeni ya wakandarasi na sasa kuna maeneo mengine wameanza kupata maji. Nakushukuru katika hilo kwa sababu kwa kweli miradi hiyo imesimama zaidi ya miaka miwili. Mwaka 2015 hatujaletewa hata shilingi ya maji. Umeonesha nia, basi naendelea kukusitiza kwamba bado tunahitaji wanachi wetu wapate maji kwa wakati ambao bajeti yao imeshapitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika hilo la maji, naomba nishauri Serikali ifanye kama inavyofanya *Road Fund*. Ukiangalia Wizara ya Maji yenyewe ni *centralized*, kwamba wanapanga Wizarani bajeti, halafu wanapeleka kwenye Halmashauri. Kwa nini isipangwe kama inavyopangwa miradi mingine fedha zikaanzia kule chini halafu zikaenda zikafanya hivyo? Kwa sababu inaonekana wakati mwingine hata Halmashauri hatujui tunapangiwa nini katika Wizara ya Maji kwa sababu imefanyika *centralization*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la miundombinu. Tunaona hili ni tatizo kwamba kila mtu analalamika miundombinu, lakini ni kweli barabara zetu zimeharibika, hazipitiki. Sasa unakuta katika Halmashauri barabara za vijijini hazipitiki; zahanati hazipo, akina mama wanajifungulia njiani, wengine wanakufa kwa sababu hakuna miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama *dispensary* zetu tunasema katika vijiji 12,500; vijiji 4,000 tu ndiyo vina *dispensary,* halafu barabara hazipitiki, kwa nini watu wasife njiani? Watakufa tu! Kwa hiyo, tunaomba tuzingatie kabisa na ili

tusaidie wananchi wetu ni lazima angalau miundombinu hiyo iwe imeboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la utawala bora. Ni kweli mnasema na sijamwona kaka yangu Mheshimiwa Lusinde, nataka nimwambie, Watanzania wote wanalipa kodi bila kujali vyama vyao na kinachopeleka maendeleo ni kodi ya wananchi na siyo kodi ya mtu mmoja mmoja wala Serikali iliyoko madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine mnazungumza habari ya utawala bora, na mimi niseme, mnasema sisi tunataka tuuze sura kwenye *tv,* siyo kweli! Serikali ilikuja hapa ikasema sababu mbili, kwa nini hawataki kurusha *live*.

Moja, wakasema gharama. *TV* za *private* wakasema tutaonesha sisi kwa gharama zetu. Jambo lingine mkasema watu hawafanyi kazi; lakini niwaulize, hivi wakati wa kufanya kazi ni wa asubuhi wakati wa Bunge au saa hizi wakati kila mtumishi ametoka kwenye Ofisi yake amekwenda nyumbani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli hamna nia ya kudhulumu Bunge hili na kuzuia Watanzania wasijue tunachojadili, badilisheni kipindi cha Maswali na Majibu kiwe giza, halafu kipindi hiki cha mjadala ambao wananchi wanataka kuona kiwe *live,* kama kweli hamna nia mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeamua kujificha kwenye Kipindi cha Maswali na Majibu, kwa sababu kila mtu anauliza swali. Tunataka mijadala hii Watanzania wajue Bunge lao linajadili nini kuhusu maslahi ya maisha yao na mustakabali wa Taifa lao. Kwa nini tunaficha? Leo tumeeleza bajeti nzuri ya viwanda hapa, tunataka Watanzania waone Bunge linasema nini kuhusu habari ya viwanda. Tunaficha nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hakuna *empire* yoyote inayotakiwa misingi yake itikiswe. Serikali ya CCM imetikiswa kwa kutumia Bunge hili. Hawako tayari kuendelea kuona likitikiswa. Tusema hivyo! Huo ndio ukweli! Mnaficha ili wakati fulani msionekane kwamba mmeendelea kuonesha udhaifu kama ambavyo Wabunge wanaendela kusema hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mambo makubwa ambayo amefanya na kwa kipindi kifupi tu. Miaka zaidi ya 30, ameturudishia ekari zaidi ya 12,000 kwa wananchi wa Monduli. Tunakushukuru na tunakuomba uendelee kuyamalizia yale, tunajua kuna figisufigisu zinafanyika lakini tutahakikisha kwamba mashamba yale yote yanarudishwa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, tunakushukuru.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja.

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha, tunaenda na Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya TAMISEMI na Utawala Bora. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha mimi binafsi kuingia katika Bunge lako Tukufu, lakini katika namna ya kipekee kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini ambao wamenipa dhamana hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na miundombinu ya barabara. Jimbo langu kwa ujumla miundombinu ya barabara ni mibovu na kwa sasa barabara nyingi hazipitiki na hasa zile barabara kutoka Nangurukuru kwenda Liwale, haipitiki, ni mbaya. Sasa hivi kutoka Nangurukuru kupitia Njinjo kwenda Liwale, hakupitiki. Hivyo, inalazimika wananchi wanaotaka kwenda huko watembee au wapite katika umbali wa kilometa zaidi ya 400, wakati kutoka Nangurukuru kwenda Liwale ni umbali wa kilometa 230. Naishauri Serikali ione uwezekano wa kujenga barabara hii katika kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuna barabara kutoka Njia Nne kwenda Kipatimo, nayo sasa haipitiki, ni mbovu. Barabara hii inapitia katika Tarafa ya Miteja na Kipatimo. Pia naishauri Serikali ione uwezekano wa barabara hii kuijenga katika kiwango cha lami.

MBUNGE FULANI: Anasoma!

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu lipo katika ukanda wa Pwani. Ukanda wa Pwani una matatizo makubwa ya maji, lakini tunayo fursa ya uwepo wa Mto Rufiji. Naishauri Serikali ione uwezekano wa kujenga mradi mkubwa wa maji katika Mto Rufiji utakaosaidia vijiji na rarafa zilizopo katika Wilaya Rufiji na Jimbo la Kilwa Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye afya. Huduma za afya katika Jimbo langu bado zinalegalega; huduma zinazotolewa ni hafifu, hakuna dawa katika zahanati, hakuna wahudumu. Tuna zahanati kama sita ambazo zimemalizika kujengwa, lakini hazina dawa wala wahudumu, kama zahanati ya Mwengei, Luyumbu...

MJUMBE FULANI: Anasoma huyo!

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Marendego, Kipindindi na Nambondo na Hongwe. Zahanati hizi zimemalizika kujengwa lakini mpaka sasa hivi hazijaanza kufanya kazi. Naiomba Serikali iangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Jimbo langu kuna Hospitali moja tu, hospitali ya *Mission*. Hospitali hii haina *x-ray* na tayari wafadhili wa hospitali hii walitoa mashine ya kisasa ya *x-ray*, lakini kwa bahati mbaya kwa sababu ilichukua muda kupata jengo, ilipata hitilafu na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alitoa ahadi ya kusaidia kufanya ukarabati wa *x-ray* hii. Kwa bahati nzuri ilipofikia mwaka 2013 akatoa shilingi milioni 40 kufanya ukarabati wa *x-ray* hii. Mpaka sasa ninapozungumza *x-ray* hiyo haijakarabatiwa na pesa zile zipo. Naiomba Serikali ifuatilie ili basi wananchi wangu waweze kupata huduma ya *x-ray.(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Kilwa Kaskazini ni dampo la mifugo kutoka Mikoa ya wafugaji. Sasa hivi tuna tatizo kubwa la migogoro ya ardhi, lakini mapigano kati ya wakulima na wafugaji na ni kwa sababu tu wafugaji wote wanaotoka katika Mikoa ya wafugaji wanakuja katika Jimbo langu na kusambaza mifugo yao bila kufuata utaratibu wa matumizi bora ya ardhi.

Naiomba Serikali ihakikishe kwamba inaondoa mifugo yote ambayo ipo katika vijiji ambavyo havikupangwa kuwepo kwa mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni elimu. Tunao mpango wa elimu bure. Huu mpango mpaka sasa naona bado ni kama unalegalega. Mimi binafsi nashauri mpango wa elimu bure uendane sambamba na kuangalia maslahi mapana ya walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bure inazungumzia namna ya kumsaidia mwanafunzi, lakini bado haijamwagalia mwalimu. Napendekeza, mpango huu uendane sambamba na kuangalia uwezekano wa kutoa *teaching allowance* kwa walimu. Walimu wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu, ni vizuri sasa kuangalia maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimia Mwenyekiti, pia kuna majengo ya Shule na Ofisi za Serikali yanajengwa chini ya viwango. Majengo mengi yanayojengwa sasa, hayawezi kudumu hata kwa miaka kumi, hali ya kwamba majengo ya Serikali yanatakiwa ya kudumu kwa miaka 50 na kuendelea. Serikali iangalie uwezekano wa kusimamia ili majengo yanayojengwa sasa yawe ya kudumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la uhakiki wa Watumishi. Suala hili katika eneo langu limezua adha na kuna shida! Tayari Serikali ilifanya zoezi hili kwa mara ya kwanza, lakini sasa inaonekana ni lazima warudie tena kufanya

tena kwa mara nyingine. Sasa inawagharimu wafanyakazi. Kwa mfano, wananchi wanaotoka Kijiji cha Nandete kwenda Kilwa Masoko ni ziaidi ya kilometa 140. Mtumishi huyu tayari alishakwenda kwa zoezi hilo kwa mara ya kwanza, lakini analazimika tena aende kwa mara ya pili. Hii inawasumbua sana watumishi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu maalum. Naomba Serikali kwanza ibaini idadi ya walemavu tujue kuna walemavu wangapi. Serikali ijielekeze kutoa huduma stahiki za walemavu. Kila mlemavu ana hitaji lake kulingana na aina ya ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mlemavu wa ngozi anatakiwa apate mafuta maalum ambayo yatamwezesha kumnusuru na athari za miale ya mwanga. Mlemavu kiziwi, anatakiwa apate shime sikio *(earing aid)*, itakayomwezesha kupata athari za uelekeo wa sauti na mlemavu asiyeona anatakiwa apate fimbo maalum itakayomwezesha kupata uelekeo. Naishauri Serikali, huduma hizi zitolewe bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwasahau walemavu wa viungo, viungo bandia vimekuwa vikiuzwa kwa bei juu, wananchi wetu hawawezi kumudu. Naiomba Serikali, huduma ya viungo bandia itolewe bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naiomba Serikali ianzishe Kurugenzi ya Elimu Maalum. Walimu wanaoshughulikia watoto wenye ulemavu, wanafanya kazi kubwa lakini mpaka sasa hatujakuwa na Kurugenzi ya Elimu Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu limepakana na Bahari ya Hindi, lina wavuvi, mpaka sasa wavuvi wanatumia mbinu za kijima kuvua. Naiomba Serikali iwezeshe vifaa vya kisasa kwa wavuvi wale ili waweze kwenda kuvua kwenye maji ya kina kirefu na basi kuweza kupata tija.

Katika Jimbo langu la Kilwa Kaskazini, kuna Tarafa mbili ambazo zinalima kilimo cha michungwa. Katika miaka ya hivi karibuni michungwa imepata changamoto ya ugonjwa ambao unakausha mimea hiyo. Naiomba Serikali ituletee wataalam watakaofanya utafiti wa kugundua ni tatizo gani linaloisibu mimea hiyo kukauka ili basi wakulima wetu waweze kupata tija ya zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze katika utawala bora. Mpaka sasa tunapozungumza, jitihada za kufikia viwango vya juu vya utawala bora bado zinakwamishwa. Bado kuna figisufigisu nyingi katika suala zima la uendeshaji wa utawala bora. Bunge lako Tukufu mpaka sasa linafanya shughuli zake kana kwamba tuko jandoni; kwa sirisiri! Hii nafikiri haipendezi na haiwezi ikawa na mchango mzuri wa ustawi wa demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mpaka sasa maslahi na matakwa ya maamuzi ya chaguzi zinazofanywa na wananchi hayaheshimiwi. Kilichotokea Zanzibar ni kutoheshimu matakwa ya maamuzi ya wananchi. Naiomba Serikali izingatie utawala bora ili basi matakwa ya maamuzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nashukuru sana. Tunaendelea, tunahamia upande wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Prosper Mbena, hayupo. Mheshimiwa Stanslaus Mabula, atafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga. *(Makofi)*

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi ya kuchangia angalau kwenye Wizara hizi mbili niweze kusema maneno machache.

Kwanza nianze kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano, Mheshimiwa Rais pamoja na Baraza lake lote la Mawaziri kwa namna ya kipekee ambavyo wamekuwa wakifanya shughuli zao na kuwajibika kwa kiwango cha hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kuwashukuru sana wapigakura wa Jimbo la Nyamagana kwa kazi kubwa sana waliyoifanya. Niwahakikishie kwamba ninapokuja Bungeni hapa, nakuwa nimekuja kazini na kazi moja kubwa ni kusimamia na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kuwalipa yale waliyoyafanya baada ya tarehe 25 Oktoba, 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa shughuli nyingi za kimaendeleo ambazo imeendelea kuzifanya katika Jimbo la Nyamagana, lakini yapo mambo machache ambayo tunapaswa kushauriana na kuambizana ili tuweze kuyarekebisha na tuweze kuendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kidogo juu ya habari ya mapato, nizungumze juu ya habari ya ajira kwa vijana, lakini nizungumze juu ya namna ambavyo Halmashauri zinaweza kuongeza mapato kutokana na uwekezaji wa taasisi mbalimbali.

Sote tunafahamu, Jiji la Mwanza ni sehemu ya Mkoa wa Mwanza ambao ni mji wa pili kwa ukubwa Tanzania; lakini ni ukweli ule ule usiofichika kwamba Nyamagana na Jiji la Mwanza ndiyo mji unaokua kwa kasi zaidi Barani Afrika katika nchi yetu ya Tanzania. Tafsiri yake unaipata katika ongezeko la watu; 3% ya kuzaliana na 8.2% ya wahamiaji na wageni wanaoingia kila wakati kwenye Jiji la Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kuikumbusha Serikali yangu, Jimbo la Nyamagana ni sehemu ambayo ni kitovu cha Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Unapoanza kuzungumza habari ya msongamano wa watu, habari ya msongamano wa vifaa wa vyombo vya usafiri, lakini habari ya msongamano wa wafanyabiashara ndogo ndogo ambao kwa kweli huwezi kuwaondoa kwa sababu ndiyo sehemu wanayoweza kupata fursa nyingi zaidi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kuiomba Wizara ya TAMISEMI kwamba Halmashauri peke yake haiwezi kukabiliana na taizo hili, lakini kupitia masuala mbalimbali, kwa mfano, tunapozungumza juu ya uboreshaji wa Miji na upanuaji wa Mji, naiomba Wizara ya TAMISEMI kupitia kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene; mara kadhaa tumekuwa tunazungumza na unanipa ushirikiano wa kutosha, nakupongeza sana. Sina shaka Halmashauri hizi zimepata dawa ambayo kwa kweli ukiendelea hivi, naamini tutafikia kwenye lengo tunalolitazamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tatizo kubwa sana la wafanyabiashara ndogo ndogo na leo nitajikita hapa sana. Bila kutafuta ufumbuzi kutoka juu, bila kuisaidia Halmashauri kuweza kupanua Mji; tunapozungumza kupanua barabara ya kutokea Buhongwa kupita Kata ya Sahwa kwenda Lwanima, kutokea Igoma kuunganisha Fumagila kukamata barabara inayotoka Usagara kwenda Kisesa; tusipopanua Mji hatuwezi kuwaondoa machinga katikati ya Mji! Tusipopanua Mji hatuwezi kupanua fursa za vijana ambao wanapaswa kujitanua na kufuata yaliko makazi! Huwezi kuwaondoa machinga kuwapeleka sehemu ambako hakuna wakazi, hakuna watu, hakuna biashara! Inakuwa ni vigumu sana; lakini ndio wakwetu hawa, wanaingia kwa kasi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakumbuka miaka ya nyuma, ni miaka michache tu iliyopita, watu wengi walitumia nafasi hii kujinufaisha sana kupitia vijana hawa wanyonge na maskini wanaotafuta maisha yao ya kawaida. Kwa sababu waligundua ukweli na kuamini Chama cha Mapinduzi peke yake kupitia watu wake wanaweza kukisaidia, Nyamagana wameamua kufuta habari ya upinzani na wakakirudisha Chama cha Mapinduzi. Sasa ni lazima tuwatendee haki kwa kuwaboreshea miundombinu, kuimarisha maeneo yao ya biashara ili wafanye kazi zao vizuri na Mji ubaki unapumua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba nizungumze juu ya uwekezaji. Tunafahamu Halmashauri hizi hazina mapato mengi. Nawashukuru sana *LAPF* kwa uwekezaji wao mzuri na mkubwa, nafahamu wamefanya Morogoro na baadaye wamekuja kufanya Mwanza. Tumefanikiwa kujenga *Shopping Mall* ya kisasa, *Eastern Central Africa* unaikuta Mwanza peke yake. Hii itatusaidia kuongeza ajira zaidi ya vijana 270.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni nini? Kuwepo kwa *mall* hii peke yake siyo tu kuongeza ajira, inaongeza kipato kwenye Halmashauri kwa sababu Halmashauri imewekeza kupitia ardhi yake, *LAPF* wamewekeza fedha. Kwa hiyo, tunagawana mapato siku ya mwisho na Halmashauri zinaendelea ku-*generate income* tofauti na kutegemea ushuru mchache ambao unatokana na kero mara nyingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la afya. Sote tunafahamu namna ya kumlinda mama na mtoto wakati wanapojifungua. Tunapozungumza kuboresha zahanati na vituo vya afya, tunapozungumzia habari ya maduka ya dawa, tumeanzia ngazi ya juu sana. Hatukatai, ni vizuri hatua zimeanza kuchukuliwa, lakini unapoboresha kwenye Hospitali ya Mkoa ukasahau kuboresha kwenye Hospitali ya Wilaya, tafsiri yake ni kwamba mzigo wote wa Wilayani unaupeleka Mkoani; unaondoa chini huku ambako watu wengi wanahitaji msaada, hatuwezi kufanikiwa. Hii ndiyo maana tunasema, siyo rahisi sana, lakini tunajitahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niwashukuru sana kwa kuanza kupeleka maelekezo kwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Hawa wakiwajibika na wao sawasawa Halmashauri zitapunguza mzigo kwa sababu watakuwa wanashirikiana katika kuhakikisha wanapeleka maendeleo kwa wananchi na mifano mizuri mnayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu, kwenye Jimbo la Ilemela pale kwa mama yangu, Mama Angelina Mabula, iko zahanati moja ya muda mrefu, Zahanati ya Sangabuye. Zahanati hii imeanza kitambo, lakini mpaka leo inapata fedha za zahanati wakati ni kituo cha afya. Halikadhalika zahanati iliyoko kule Nyamuhungolo, hakuna wataalam lakini inavyo vifaa vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie tu kwa kusema nikiwa naendelea na mimi nashangaa sana kwenye suala la elimu; tumesema elimu ni bure, watu wanalalamika. Wakati inaanzishwa, wakati tuko kwenye kampeni, watu walikuwa wanajinasibu kutoa elimu bure, leo wanashangaa Serikali ya CCM kutoa elimu bure, wanasema ni fedha za walipakodi. Unapozungumza elimu bure, tafsiri yake ni nini? Nani unataka atoe fedha mkononi kama siyo Serikali yenyewe? Na mimi nashangaa! Nilikuwa najiuliza, hawa watu ni kiumbe cha namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tukitaka kuangalia hapa; namshukuru sana Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa kuona thamani na umuhimu wa elimu hii ambayo CCM imesema, elimu ya kuanzia chekechea, msingi na sekondari ni bure. Kwake kule kwenye Halmashauri akiwa na mwaka mmoja tu na Chama chake, amesisitiza kuanzia kidato cha tano na cha sita. Ninyi mna miaka 23 mmefanya

nini kwenye elimu kama siyo kulalamika leo? Nimekuwa najiuliza, tunahangaika hapa, kila siku ni kutukana, kulalamika! Tunataka kujua! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ungetusaidia. Mara zote mimi nimejiuliza, hawa UKAWA ni viumbe wa namna gani? Ni chura au ni popo hawa? Maana ndiyo peke yake huwezi kujua! Chura anabadilika kila wakati, lakini kinyonga huwezi kujua! Kinyonga anabadilika kila wakati, lakini popo huwezi kujua kama ni ndege au ni mnyama? Kwa hiyo, hii tunaipata wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 22 Aprili, 2016 hapa Mwenyekiti wao alisema, katika mazingira kama haya, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiko tayari kuendelea kushiriki na uvunjaji wa Katiba, Sheria na haki za msingi za wananchi. Leo wanashiriki hapa, wameungana na sisi, hawajaungana na sisi? Ukishindwa kupambana naye, ungana naye. Hii ndiyo dhana halisi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hawa wameshashindwa kupambana na sisi…

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Nawashukuru kuendelea kuungana na sisi! Na mimi nakushukuru sana. Dhamira ya Chama hiki ni kuendelea kuongoza na kuweka maendeleo sawasawa. *(Makofi)*

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa namalizia, namshukuru sana Waziri wa Wizara ya Michezo, Habari, Sanaa na Utamaduni.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, unavumba eeh!

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Nyamagana tumehangaika kwa muda mrefu juu ya uwanja wetu wa Nyamagana, leo ninavyozungumza tayari nyasi ziko bandarini na muda mfupi kazi inaendelea katika uwanja wa michezo wa Nyamagana. Tafsiri yake, tunataka kuimarisha! Ukiimarisha michezo umekuza ajira kwa vijana. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda umeisha Mheshimiwa! Tunaendelea!

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mwongozo wa Spika!

MBUNGE FULANI: Kaa chini!

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mwongozo wa Spika!

MBUNGE FULANI: *Sit down!*

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mwongozo wa Spika, hapa!

MWENYEKITI: Hapana.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, hutaki Mwongozo eeh! Ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Silanga!

MHE. NJALU D. SILANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nianze kwanza kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kuweza kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na wananchi wanaipokea kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru Wizara ya TAMISEMI kwa kazi kubwa na kwa muda mfupi walioifanya na kuonesha kwa wananchi kwa kuchukua hatua kwa wale wanaofuja fedha za Serikali. Naiomba Wizara hii ijaribu kuangalia maeneo mapya hususan Wilaya ya Itilima, ni Jimbo jipya na Wilaya mpya, takribani miaka 20 liko upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, wananchi hawa wameweza kufanya kazi kubwa ya kutekeleza Sera za Serikali ya Awamu ya Tano. Serikali ya Awamu ya Tano inasema kila kijiji kuwe na zahanati. Tunavyozungumza hivi, tunazo Zahanati 29 na zahanati nane ziko katika hatua za mwisho. Naiomba Wizara iweze kuleta fedha za kumalizia hizo zahanati ziweze kufanya kazi, ukizingatia Wilaya yetu ya Itilima ni Wilaya ambayo haina Hospitali ya Wilaya. Tunategemea sana hizo zahanati zitapunguza kasi katika maeneo ya Maswa pamoja na Wilaya ya Bariadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza tu Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa inayoifanya, vilevile na Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya pamoja na wasaidizi wake. Nataka niwaambieni ndugu zangu, Awamu ya Tano imewagusa Watanzania wote na haya tunayoyazungumza na wao wanasikia. Kwa kweli, kazi inayofanywa, kila mtu anaiona na anaitazama. Ni sehemu pekee kwa muda mfupi wameweza kutekeleza majukumu makubwa na ya msingi kwa kuleta mabadiliko makubwa katika awamu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia suala la madawati, Awamu ya Tano imezungumza kwa mapana sana. Tunaozunguka vijijini unakuta shule moja ina wanafunzi 939, ina madawati 36! Unategemea pale tunatengeneza Taifa la aina gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya Awamu ya Tano kugundua na kutoa maelekezo, bado wenzetu wanaendelea kulalamika, lakini hoja ni nzuri ni kuhakikisha Watanzania, watoto wetu, wanapata maisha bora na elimu iliyo bora. Vilevile itapunguza gharama kwa wazazi wetu kununua mashati pamoja na sketi kwa ajili ya watoto wetu watakapokuwa na madawati bora, natarajia na elimu itakuwa nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe ushauri, kwenye 50%, kwenye suala la shilingi milioni 50 kwa kila kijiji. Wengi wamesema, lakini ikumbukwe, lazima tujenge uwezo katika maeneo yetu ya vijiji. Shilingi milioni 50 tutakapozipeleka bila kuwa na elimu ya kutosha, zile fedha zitapotea na hazitaleta *impact* yoyote katika maeneo husika. Taasisi moja ipo katika maeneo ya Halmashauri inaitwa Idara ya Maendeleo ya Jamii; wale watu wangefanya kazi ya kutoa elimu kwa wananchi kabla fedha zile hazijafika waweze kujua jinsi ya kuzitumia, kuliko kumpelekea mtu lundo la shilingi milioni 50 katika kijiji kimoja, halafu zile fedha zitapotea na hazitakuwa na hadhi yoyote katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo, zile fedha ni nyingi zinaweza zikasaidia na zikatoa umaskini katika maeneo husika. Maeneo yako katika tabaka mbalimbali. Maeneo mengine kuna Vyama vya Ushirika, kuna ma-*godown,* maeneo mengine wanalima korosho, pamba na kadhalika. Ile fedha ikitolewa na Tume ya Ushirika ikiboreshwa vizuri, ni imani yangu ile fedha inaweza ikawa mtaji mkubwa katika vijiji husika na ikaleta maendeleo makubwa sana kama wenzangu walivyochangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, nashukuru sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ili Watanzania waweze kufaidika na hii Awamu ya Tano. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mwongozo wa Spika!

MWENYEKITI: Nakushukuru sana.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mwongozo wa Spika!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, nilisema sitachukua Mwongozo wakati huu kwa sababu nataka nivute kidogo. Nitakuja kuwaachia kama dakika 10 ili mje mtoe mliyonayo. *(Makofi)*

Msemaji wetu anayefuata nadhani ni wa mwisho ili kutoa nafasi ya Mwongozo na matangazo ya Spika ni Mheshimiwa Innocent Bashungwa!

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora). Nianze kwa kuendelea kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Magufuli, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Baraza la Mawaziri kwa kuendelea kufanya kazi nzuri ya kuwaletea matumaini Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia kwangu bajeti ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), ningependa kuchangia katika sehemu mbili; sehemu ya kwanza, ni changamoto za wananchi wangu wa Jimbo la Karagwe na sehemu ya pili ni ushauri kwa Serikali. Kwa sababu changamoto kwenye Jimbo langu la Karagwe ni nyingi, naomba kwanza nijikite kwenye hizi changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene kwa kazi nzuri na kuwa msikivu pale tunapomfuata kuwasilisha changamoto za wananchi wetu. Namshukuru Mheshimiwa Angellah Kairuki kwa kuwa msikivu na kwa kutupa ushirikiano mzuri katika kusikiliza changamoto za wananchi wetu na kaka yangu Naibu Waziri, Mheshimiwa Jafo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Karagwe ina changamoto nyingi, lakini kwanza nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Karagwe kwa kuendelea kuniamini na kunituma hapa kuwa Mbunge wao. Wiki mbili zilizopita Karagwe tulipata janga kubwa, tumepata janga la moto pale Kayanga, maduka zaidi ya 117 yaliungua.

Mhesimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, naomba nitumie nafasi hii kuwapa Wahanga wa moto, wananchi wa Karagwe pole sana na nitumie nafasi hii kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Simbachawene kwa kuwapa pole Wana-Karagwe na kwa kuniahidi kwamba Serikali itaangalia namna ya kuwasaidia hawa wahanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, juzi kulitokea tukio la ujambazi stesheni ya Nyakaiga, majambazi wakaua mwananchi mmoja pale na mwingine wakamjeruhi sana. Pale Nyakaiga ni stesheni kubwa, ina wananchi wengi lakini hatuna huduma ya kituo cha polisi. Napenda kuiomba Serikali itusaidie, pale Mji umekua, Serikali itusaidie kujenga kituo cha polisi ili wananchi waweze kuishi kwa amani na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kuna changamoto nyingi Jimbo la Karagwe, lakini nitaje chache. Nianze na madeni viporo. Pamoja na jitihada ya Serikali kupeleka fedha za maendeleo, bado kuna changamoto ya kuchelewesha hizi fedha.

Katika Halmashauri ya Karagwe, bado tuna madeni makubwa ya wakandarasi, watumishi na wazabuni. Napenda kuiomba Serikali katika kipindi cha mwaka huu wa fedha wa 2015/2016 kabla hatujaenda mwaka wa fedha mpya, Serikali ijitahidi ituletee fedha ambazo tulitakiwa kupata katika kipindi cha mwaka wa fedha ili tuweze kupunguza haya madeni na fedha ambayo imetengwa kwa mwaka wa fedha unaokuja 2016/2017 iweze kwenda kufanya kazi za maendeleo ambazo tumezitarajia katika mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna tatizo kubwa la upungufu wa watumishi katika Jimbo la Karagwe. Kwa upande wa walimu, sekta ya elimu kwa shule za msingi tu, tuna upungufu wa walimu 832. Kwa upande wa shule za sekondari tuna upungufu wa walimu 92.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya afya kwa upande wa upungufu wa watumishi tuna upungufu wa wauguzi 40 na madaktari watano na kwa upande wa kilimo Afisa Ugani tuna upungufu wa watumishi 15 na upande kwa maendeleo ya jamii tuna upungufu wa wataalam 27.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama takwimu zinavyoonesha, Halmashauri yangu ina upungufu mkubwa sana wa watumishi. Napenda kutumia nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri Angellah Kairuki, aione Karagwe. Tunakutegemea sana na tunaamini utatusaidia katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala la madeni ya Halmashauri, napenda kuishauri Serikali, kama fedha kutoka Hazina imekuwa ikichelewa kutolewa kwa miaka mingi, basi tuangalie ule utaratibu wa asilimia 70 ambazo zinatoka Halmashauri kwenda Hazina, tuigeuze ile; zile asilimia 70 zibaki kwenye Halmashauri halafu asilimia 30 ndiyo iende Hazina ili fedha za maendeleo siziwe zinachelewa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna upungufu wa vitendea kazi hasa kwenye sekta ya afya kwenye Jimbo la Karagwe. Karagwe ina watu wasiopungua 350,000 na sisi tumezaa Jimbo jipya la Kyerwa ambalo bado tunaendelea kulihudumia katika huduma za afya kama Wilaya mama ya Karagwe ambayo imezaa Jimbo la Kyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua Kyerwa na Karagwe, tuna jumla ya watu wasiopungua 800,000, lakini bado tuna *ambulance* moja tu ambayo inahudumia vituo vya afya 35 na jiografia ya Karagwe imesambaa sana. Kwa

hiyo, naiomba TAMISEMI itusaidie angalau tupate *ambulance* mbili ili wananchi wa Karagwe wapate huduma ya *ambulance* pale tunapohitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika upande wa afya, tuna hospitali ya Nyakahanga lakini imeelemewa. Kama nilivyosema, Kyerwa bado haijawa na Hospitali ya Wilaya, Karagwe Wilaya mama pia haina hospitali ya Wilaya. Tunategemea hiyo hospitali ya *ELCT*. Natumia nafasi hii kulishukuru kanisa la *ELCT* kwa kuendelea kusaidia wananchi wa Karagwe na hospitali ya Nyakahanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Karagwe tunakua kwa watu wasiopungua 10,000 kwa mwaka; hospitali imekuwepo miaka mingi sana, imefika mahali imeelemewa na inasaidiwa na kituo cha afya cha Kayanga ambacho hivi sasa hakina wodi ya akina mama na watoto. Kina wodi ya wanaume; na kituo hiki hakina wodi ya kulaza wagonjwa wanaofanyiwa upasuaji. Kwa hiyo, napenda kumwomba kaka yangu, Mheshimiwa Simbachawene na Naibu Waziri Mheshimiwa Jafo, mtuangalie katika hili pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna changamoto za barabara ambazo ziko chini ya TAMISEMI. Kuna barabara ya kuanzia Nyakasimbi kwenda Nyakakika, Kibondo, Nyabiyonza, Kiruruma mpaka kwenda kwenye Wilaya ya Kyerwa kupitia Rwabwere, hii ni barabara ambayo inaunganisha Wilaya mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali hii barabara ipandishwe kwenye kiwango wa *TANROAD* kwa sababu kwa kufanya hivi tutakuwa tumeondoa mzigo kwa Halmashauri, itatengenezwa katika kiwango kizuri na itasaidia kuinua uchumi wa wananchi wa Karagwe na Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Rais Magufuli wakati alipokuja Karagwe kuomba wananchi ridhaa ya kuwa Rais wa Tanzania alituahidi barabara ya Nyakahanga kwenda Chamchuzi tuipandishe *TANROAD* na ijengwe kwa kiwango cha lami na tuweke kivuko pale Chamchuzi ili kusaidia kuimarisha biashara kati ya Karagwe na jirani zetu wa Rwanda. Kwa hiyo, napenda kuiomba Serikali itusaidie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimefuatilia Wizara ya Ujenzi wakanielekeza kuwa kuna utaratibu wa kuingiza ahadi za Mheshimiwa Rais kwenye kitabu cha ahadi za Mheshimiwa Rais, lakini mimi ni mwakilishi wa wananchi wa Karagwe, Mheshimiwa Rais alitamka mwenyewe, Mheshimiwa Rais hawezi kusema uongo, na mimi hapa mwakilishi wa wananchi wa Karagwe siwezi kusema uongo. Napenda kuiomba Serikali itumie taarifa hii kama ni rasmi kwamba hili kweli lilitamkwa na watusaidie tupate hii barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. MWITA M. WAITARA: Mwongozo wa Mwenyekiti!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, kwa leo ndiyo tunafikia mwisho kwa uchangiaji. Kwa siku ya leo, nitasema baadaye lakini nilikuwa nimeangalia kwa mujibu wa Kanuni ya 72(1) lazima kiti kiangalie matumizi bora ya muda wa Bunge. Ndiyo maana nikasema suala la Taarifa niliona lina madhara gani, ndio maana leo sikutaka sana kutoa nafasi kwa taarifa. Taarifa hizi zinatolewa na watu wanadharau tu; sichukui! Ni haki ya Kanuni ndiyo, lakini nasema tuanagalie basi matumizi bora ya muda wetu.

Kuhusu Mwongozo, nikasema mwishoni hapa nitoe nafasi, sasa mnaweza kuomba Mwongozo wa Kiti, tuyachukue. Tuanze sasa, Mwongozo!

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakwenda kwenye Kanuni ya 68 (7) na 64(1)(d) kama ilivyotumiwa na mama Jenista wakati akizungumza hoja ya Mheshimiwa Waitara. Hii inahusiana, nitaisoma hiyo 64(1)(d) inasema: "Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge (1)(d) hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo ninaoutaka ni kwamba Bunge lina uhuru wa kujadili na tumeambiwa pale bila kujali Kanuni ya 100 ya Kanuni hii, lakini pia tunaishi kwa Katiba ya nchi.

Sasa kuna utata hapa unatokea mara nyingi, anapotajwa Mheshimiwa Rais na upande huu wa Upinzani, mara nyingi inatumika Kanuni hii. Kanuni hii ina misingi miwili mikuu; kwanza, kumdhihaki Rais, lakini Kanuni ya pili msingi wake ni kujaribu kulishawishi Bunge kuamua kwa namna fulani. Sasa mara nyingi tukiwa *critically* kwa Mheshimiwa Rais, hoja hii inakuja lakini hatukuambiwa kama Rais asitajwe kabisa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni kwamba, kwa mwongozo wako naona kama kanuni inatumika vibaya. Kila tukiwa *critically* kwa Mheshimiwa Rais, kanuni hii inakuwa *raised*. Ama mimi nitakubali ikiwa inatumika dhihaka ichukuliwe hatua, lakini pia hii kanuni inasema ikiwa inapotakiwa kufanywa maamuzi.

Mwongozo ninaoutaka, je, wakati wa mjadala tunafanya maamuzi? Ni kwanini Mheshimwia Rais asitajwe wakati wa mjadala ambapo siyo wakati wa maamuzi? Kama wakati wa maamuzi, kwa nini wale kule wakitumia hoja hiyo hiyo kumsifu Mheshimiwa Rais kutaka kujenga hoja ya maamuzi kwa nini hakutolewi Mwongozo?

Kwa hiyo, wasiwasi wangu ni huo kwamba kanuni hii inatumika vibaya; tunapokuwa *critically* kwa Mheshimiwa Rais inatolewa kanuni hii, lakini je, wakati wa mijadala kama hii ni wakati wa maamuzi? Tunashawishi maamuzi kweli tukisema Mheshimiwa Rais, kumetokea kitu kadhaa kadhaa, Rais kawapigia simu watu, Rais kasema watu wanarekodiwa. Je, tunataka kufanya maamuzi? Huo ndiyo Mwongozo ninaoutaka.

MHE. MWITA A. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia Ibara ya 68 (7) na naomba Mwongozo kwa kutumia Ibara ya 64 ya Kanuni.

Kuna makatazo hapa yametajwa pale, sasa wakati Mheshimiwa Lusinde anachangia, amewaambia Waheshimiwa Wabunge na wewe Mwenyekiti kwamba ni mwalimu wangu kisiasa jambo ambalo siyo kweli. Kwa sababu Mheshimiwa Lusinde alikuwa CHADEMA na mimi nilikuwa CCM wakati huo; na mimi nimekuwa mkufunzi wa CCM pale Chuo Kikuu cha Ihemi, miongoni wa wakufunzi wakati huo wa Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Lusinde alikuwa CHADEMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekutana mara ya mwisho Tarime wakati akiwa Katibu wa Wilaya, mimi nagombea Ubunge nikiwa CHADEMA. Sasa sioni amekuwa mwalimu wangu wapi. Kama anaweza akathibitisha, vinginevyo kauli hii ifutwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo mwingine, wakati Mheshimiwa Mabula anachangia, amejaribu kulidanganya Bunge pia. Anasema, Kiongozi wa Upinzani Bungeni wakati anawasilisha hoja yake, aliona katika mazingira haya hatutajadili. Tulichokubaliana kwenye kikao na wala siyo hoja ya Mwenyekiti peke yake au Kiongozi wa Upinzani Bungeni ni kwamba sisi tulisema hoja ya Waziri Mkuu hatutachangia. Sasa tupo kwenye Ofisi ya Rais na ndiyo maana unaona Wabunge wengi wametoa michango kwa namna mbalimbali. Kwa hiyo, na hilo tungepata Mwongozo wako juu ya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, Mheshimiwa Lusinde alikuwa anajaribu kusema kwamba Majimbo ambayo yanaongozwa na Upinzani yasipelekewe miradi ya maendeleo. Kwa hiyo, naomba Mwongozo wako kwa sababu Majimbo haya hayapelekewi fedha za maendeleo kwa sababu ya utashi wa mtu; Watanzania wote ni walipa kodi na tupo kikatiba kwa mujibu wa

Katiba yetu hii. Kwa hiyo, hakuna habari ya ubaguzi. Kwa hiyo, naomba pia Mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa mwisho ni kwako mwenyewe. Wakati mimi nachangia, ulisema muda wangu umeisha kitu ambacho hakikuwa kweli; kwa hiyo, kwa mazingira hayo, ukanitoa kwenye reli na kwa hiyo, kuchangia kwangu kukayumba kidogo na muda wangu hukuniongezea hata sekunde. Kwa hiyo, nahisi kama ulinipunja muda pamoja na kwamba uliingilia muda wangu wa mazungumzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwasilishe Miongozo yangu hiyo. *(Makofi)*

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mwongozo wa Mwenyekiti!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kanuni ya 68(7) naomba mwongozo wako. Wakati Mheshimiwa Mwita Waitara anachangia, alitumia maneno ambayo ninadhani yanalidhalilisha Bunge hili kwa kusema kwamba Bunge hili limekuwa bubu, butu, kibogoyo, limekatwa meno; ametumia maneno ambayo yanatafsiri hayo machache niliyoyatolea mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mwongozo wako, maneno haya yasipothibitishwa, yasipokanushwa yakaachwa yaendelee hivi, ninaamini yanalivunjia heshima Bunge hili na yanaondoa imani ya wananchi kwa Bunge hili kwamba hapa tumekaa hakuna tunachokifanya, lakini sisi hapa ni vibogoyo, hatuna meno, hatuna tunalolifanya na kwa kweli yanaligeuza Bunge hili kuwa jipu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha hii inayotumika ikiachwa iendelee, inalishushia heshima Bunge hili. Naomba Mwongozo wako, haya maneno aidha ayathibitishe sasa kwa wananchi kwamba ni kweli Bunge hili hapa linakula fedha ya umma bure na hakuna kinachofanyika hapa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wangu ndiyo huo niliowaambia na kwa mujibu wa Kanuni ya 68 inayohusika, kiti hakilazimiki kujibu mwongozo hapo hapo, kinaweza kikafanya hivyo au kikachukua kwenda kutafakati na baadaye kuja kutoa uamuzi; lakini ninavyoyaona haya, naweza nikayafanya machache mepesi.

Nianze na hili la Mheshimiwa Waziri. Ni hoja nzuri ameitoa sasa hivi, lakini kipindi pale aliposimama hakusimama kwa mujibu wa Kanuni ya 63 akaiunganisha na 64, alisimama kwa mujibu wa kutoa taarifa. Ndiyo maana nikasema, taarifa hizi hazingetusaidia kwa sababu nilijua yule angekataa tu. Sasa nawasihi sana tuendelee kuzisoma kanuni hizi. Ukitaka kuingia kwa njia ya kuhusu utaratibu, hiyo ndio inachukua kipaumbele cha kwanza. Lazima tusimamishe shughuli zote kwa sababu Spika kwa mujibu wa Kanuni ya 5 na Kanuni ya 72 ndiyo anatakiwa asimamie kanuni hizi, atilie nguvu.

Ukija kwa mwongozo; na nilieleza Waheshimiwa Wabunge. Naelewa *sometimes* kanuni hizi hatujazipata vizuri; unasema kuhusu utaratibu, Kiti kinakwambia siyo kanuni hiyo, maana ni lazima useme kanuni. Kwa hiyo, ndiyo maana wengi huwa tunajificha kwenye kuomba Mwongozo ambapo hakuna mtu au Mbunge anayesema ili hilo litolewe ufafanuzi kwamba likitokea la namna hiyo ni ukiukwaji wa kanuni namba fulani na fulani au miiko na desturi ambayo Bunge hili limejiwekea. Kwa hiyo, tukienda hivyo kutakuwa hamna tatizo.

Waheshimiwa Wabunge, Taarifa ni nzuri sana kama tulingelikuwa tunazitumia kwa shabaha iliyokusudiwa na kanuni. Nimeanza kuona hata mahali ambapo taarifa inatolewa ni nzuri, anaulizwa na Kiti, unaikubali taarifa hiyo? "Siikubali!" Ndiyo kanuni zinasema hivyo; halafu unaambiwa *message sent*. Sasa mimi hayo yananisumbua sana.

Waheshimiwa Wabunge, hilo la Bunge kukatwa meno, nasema ikija kwa sura hiyo, lakini wote tunajua shughuli ya Bunge hili. Tunafanya mambo makubwa humu, iwe ni ya kutunga sheria, iwe ni ya kupitisha *resolutions*, tunafanya kazi hiyo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, wala hatushinikizwi na mtu yeyote! Wala hilo tusiwe na wasiwasi wowote. *(Makofi)*

Hili la Mheshimiwa Waitara, yawezekana mwishoni na mimi leo kwa sababu ya muda huu, nilikuwa naangalia, maana wachangiaji bado ni wengi tu hapa; yawezekana nimekukwaza kidogo, lakini sikuwa na maana hiyo. Mimi *whether* Mheshimiwa Lusinde na wewe, nani alimfundisha mwenzake siasa, sisi hayo hayatuhusu humu. Hayo mwende mkaelezane huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mabula, napenda sana tujenge hii siasa. Alisema nadhani Mheshimiwa Nsanzugwanko; nafasi ya upinzani katika *democratic government,* mfumo kama tulionao sisi inafahamika ni kuhakikisha kwamba Serikali inatekeleza majukumu yake. Pia upinzani una jukumu la kuhakikisha kwamba mnaipatia Serikali, kwa sababu kupitia chama chake ndio wananchi waliochagua sera zake iweze kutekeleza mipango yake na programu hizo. Ndiyo maana tunasema Bunge, tukiwa pande zote, chama kilicho na uongozi wa Serikali na vyama vingine vya upinzani vinavyowakilishwa Bungeni,

kuiwezesha Serikali iweze kutekeleza majukumu yake, hilo ndilo jukumu la Bunge. *(Makofi)*

Msipoiwezesha Serikali, kama sasa hivi kwenye Bajeti mkainyima fedha, haiwezi ikaenda kutekeleza ahadi ambazo ilitoa kwa wananchi. Ndiyo maana hiyo kwamba pawepo na ushirikiano kati ya Bunge na Serikali iwezeshe lakini kwa hoja. Fedha ya Serikali, fedha ya Umma lazima ije hapa ijengewe hoja na ndiyo maana Serikali inafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ally Saleh, lini tunafanya maamuzi? Hoja hizi kesho ndiyo tunahitimisha. Mchango huu ni *warming up* wa kwenda kufanya maamuzi.

Kwa hiyo, ndiyo maana kile kifungu cha 64 (1)(d), unapoanza kushawishi, watu wakuunge mkono kwa njia hii, ndio maana inakataza. Ni katazo hilo! Upande huu unatoa hoja kwamba hoja hii ni nzuri kwa sababu haya na haya kwanza yanazaliwa na Ilani ya Chamailichoenda kuomba kura na wengine na wananchi wakakubali. Wanasema tuliahidi tuyafanye haya na haya na haya na Mheshimiwa Rais ndiyo anatoa maelekezo hayo.

Waheshimiwa Wabunge, ushawishi ndiyo hujenga hoja. Ndiyo nilikuwa nasema, mimi hili siwezi kuseme *monopoly* ya *knowledge,* lakini Mwongozo wangu katika hilo ni kwamba hapa tunaelekea kesho kuhitimisha hoja hiyo. *(Makofi)*

Waheshimwa Wabunge, sasa baada ya kusema hayo, nina matangazo, mniwie radhi muda hauko rafiki na mimi.

Kesho tunaendelea na Bunge na wachangiaji mtaambiwa kesho. Matangazo yangu ni kwamba Waheshimiwa Wabunge siku ya Jumapili ni siku ya *May Day*, ni siku muhimu sana duniani na nchini hapa.

Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wabunge, tunaombwa sana tujitahidi wote tuwe uwanja wa Jamhuri na mgeni rasmi atakuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mwisho, kwenye *pigeonholes* zetu ili kuleta ufanisi baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hatutoi kwa haraka *documents,* kwa hiyo, inakuwa ni vigumu sana mnapotaka kuongezewa *ducuments.* Wanaomba sana tujitahidi haraka iwezekanavyo kutoa nyaraka zetu kwenye visanduku hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, baada yakusema hayo, muda wangu ndio huo. Naliahirisha Bunge hili hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 2.00 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi,
Tarehe 30 Aprili, Saa Tatu Asubuhi)